# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

### Kikao cha Arobaini na Saba – Tarehe 20 Juni, 2022

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali, Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba, sasa aulize swali lake.

Na. 411

**Kutenga fedha kwa ajili ya kujenga barabara ya Wino-Ifinga**

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kutengeneza barabara ya Wino hadi Ifinga ambayo wakati wa masika haipitiki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Madaba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini kwa maana ya *TARURA*, Halmashauri ya Wilaya ya Madaba, imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kuboresha barabara ya Wino – Ifinga yenye urefu wa kilomita 57 ili iweze kupitika majira yote ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 barabara ya Wino – Ifinga ilitengenezwa jumla ya kilomita 21 kwa kiwango cha changarawe kwa gharama ya Shilingi Milioni 398.00 na katika mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya kilomita 15 zimejengwa kwa kiwango cha changarawe kwa gharama Shilingi Milioni 360.46.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga Shilingi Milioni 380.00 kwa ajili ya kujenga kilomita 10.5 kwa kiwango cha changarawe na ujenzi wa maboksi kalavati matatu. Serikali itaendelea kuboresha

Miundombinu ya barabara za Halmashauri ya Wilaya ya Madaba kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara hii kwa kipindi cha miaka mitatu imetumia zaidi ya Bilioni Moja kuijenga na Serikali imeashaweza kutoa fedha hizo, hii ni dhahiri kwamba Serikali imedhamiria kumaliza tatizo la barabara hii. Haa hivyo, barabara hii bado kuna kipande cha kilomita 18 kutoka Ifinga Mjini kuelekea Kitongoji cha Muungano na Ruhuji kilometa 18.

Je, ni lini sasa Serikali itaifungua barabara hii kuelekea eneo hilo la Ruhuji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Madaba, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inafanyakazi kubwa na kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ameomba ongezeko la eneo la barabara la kilomita 18 kutoka Ifinga kwenda kwenye Kitongoji cha Muungano, basi naawagiza *TARURA* Mkoa wa Ruvuma pamoja na

Halmashauri ya Madaba waende wakapitie barabara hiyo na wafanye tathmini na baada ya hapo watuletee fedha ili tuweze kui-*extend*. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini sasa aulize swali lake.

Na. 412

**Hitaji la Soko Mji Mdogo wa Chala – Nkasi**

**MHE. VINCENT P. MBOGO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga Soko katika Mji Mdogo wa Chala Wilayani Nkasi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ipo katika hatua za awali za kupata eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 12,140 kwenye eneo la gulio lililopo katikati ya Mashete na Namanyere na ambalo litatosheleza mahitaji ya ujenzi wa soko katika Mji Mdogo wa Chala.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri itakapokamilisha taratibu zote za kupata eneo hilo na kuandaa andiko na gharama za mradi huo itatenga fedha kwenye bajeti ya mwaka 2023/2024 kwa ajili ya ujenzi wa soko hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Sabu swali la nyongeza. Waheshimiwa Wabunge ukiwa na swali la nyongeza unasimama, ukiwa umekaa maana yake umeridhika na majibu ya Serikali. Sasa kwa sababu nilishamwita Mheshimiwa Sabu nitarejea kwako. Mheshimiwa Lucy Sabu swali la nyongeza.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa fursa hii, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itajenga soko la kisasa katika Wilaya ya Bariadi, Mkoani Simiyu ukizingatia Wilaya ya Bariadi ni Makao Makuu ya Mkoa wa Simiyu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Lucy Sabu, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tulishatoa maelekezo katika Halmashauri zote ambazo zinahitaji miradi ya kimkakati kuandika maandiko ili Ofisi ya Rais TAMISEMI tutafute fedha na kuileta katika hayo maeneo ili waweze kupata masoko ya kisasa ikiwemo hiyo Halmashauri ya Bariadi. Kwa hiyo, niwape tu hilo agizo kwamba walete hayo

maandiko yao nasi tutayafanyia kazi. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Vicent Mbogo swali la nyongeza.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, katika swali langu la msingi naomba kuongeza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Wampembe ina Kata Nne ambazo kuna biashara kubwa sana ya samaki ambayo inafanyika na nchi jirani hakuna soko. Je, ni lini Serikali itawajengea soko kwa ajili ya biashara zao za samaki Kata ya Wampembe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mimi ningemuomba Mheshimiwa Mbunge, kwanza tumalize soko la Chala halafu baada ya hapo kama vipaumbele vinavyofuatia, maana yake linalofuatia ni hilo eneo ambalo amelifikisha hapa Mheshimiwa Mbunge. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba Ruhoro swali la nyongeza.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba sasa kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itaanza kuwajengea wananchi wa Jimbo la Ngara soko la kimkakati eneo la Kabanga? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Ndaisaba George, Mbunge wa Jimbo la Ngara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninatambua kwamba Halmashauri ya Ngara imeshaleta andiko lake na wataalam katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI wapo kulipitia ili tutafute fedha kwa ajili ya ujenzi. Kwa hiyo, niwaagize tu wafanye haraka kwenye mapitio ya hilo andiko na kutafuta fedha ili eneo hilo la Mheshimiwa Mbunge alilolianisha waweze kujengewa soko. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 413

**Hitaji la maji vijiji 46 Wilaya ya Rungwe**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaharakisha na kumaliza upembuzi yakinifu kwa ajili ya mradi wa maji katika vijiji 46 Wilaya ya Rungwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Marryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda Mbunge Viti Maalum, Mkoa wa Mbeya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 utekelezaji wa miradi ya maji unaendelea katika vijiji 15 na kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji kwa wastani wa asilimia 70. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 kazi za usanifu kwa vijiji 31 itakamilika na kuanza ujenzi wa miradi, matarajio ni kuhakikisha wananchi wa vijiji 155 Wilaya ya Rungwe wanapata maji kwa lengo la kufikia asilimia 85 ifikapo mwaka 2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza:-

Swali la kwanza, tunashukuru kwa Shilingi Bilioni 1.1 ambayo Wilaya ya Rungwe ilipata kati ya Shilingi Bilioni Nne ambayo ilikuwa ni bajeti. Sasa Serikali haioni umuhimu wa kuhakikisha angalau tunapata nusu ya bajeti ambayo ilikuwa iliombwa ili kuwasaidia watendaji kufanyakazi yao vizuri?

Swali la pili, kumekuwa na ahadi za viongozi mbalimbali wanaokuja kwenye Wilaya zetu na kuahidi wananchi kupata maji kwa wakati. Sasa Serikali haioni umuhimu wa miradi ile inayoahidiwa na viongozi iweze kufanyika haraka na watu waweze kupata maji kama ambavyo watu walipata ahadi hasa katika hivyo vijiji 155 vya Rungwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kupokea kwanza shukrani na anayeshukuru anaomba tena ndiyo swali lako la pili linapoelekea. Ni kweli tumefika Wilaya ya Rungwe na tumeahidi na tunakwenda kutekeleza ni suala la muda tu Mheshimiwa Mbunge naomba utupe nafasi tufanyekazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza swali la nyongeza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba kufahamu ni lini Serikali itaanza Upembuzi yakinifu katika mradi wa maji katika Kijiji cha Lukululu uliopo katika Jimbo la Vwawa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juliana Shonza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upembezi yakinifu tunatarajia kuanza mwaka ujao wa fedha na kadri fedha itakapopatikana kasi itakuwa ni kubwa, lengo ni kuwafikia wananchi wote ili waweze kupata maji safi na salama bombani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Monni swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kuna vijiji vya Machiga na Chandama kuna mradi wa maji ambao tayari Kandarasi yake ilitangazwa na Mzabuni akapewa lakini mpaka leo hayupo *site*. Nini kauli ya Serikali kuhusu Mzabuni huyu kuwepo *site*? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Monni, Mbunge wa Chemba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wakandarasi wote ambao tumesaini nao mikataba wanafahamu sheria na taratibu na tayari Mheshimiwa Waziri ameshaongea mara nyingi, hatutakawa na mzaha na wale Wakandarasi ambao

wanachelewa kufika *site* hivyo Mheshimiwa Mbunge hili nimelipokea na tutalifanyia kazi kwa karibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Abdul-hafar Idrisa Juma, Mbunge wa Mtoni sasa aulize swali lake.

Na. 414

**Ucheleweshaji wa fedha za Mfuko wa Jimbo**

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA** aliuliza: -

Je, ni lini majimbo ya Zanzibar yatapata fedha za Mfuko wa Jimbo kwa wakati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa Juma, Mbunge wa Mtoni, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, fedha za Mfuko wa Jimbo kwenda Majimbo ya Zanzibar hupelekwa kwa wakati na kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za fedha, ambapo fedha hizo huamishwa moja kwa moja kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenda Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, katika mwaka

2021/2022 fedha za mfuko kiasi cha Shilingi Bilioni 1.4 zimeshatolewa kwa ajili ya Majimbo ya Zanzibar. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdul-Hafar Juma swali la nyongeza.

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali lakini ningependa kujua:

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na Maafisa Maalum walio chini ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania watakaokuwa wanasimamia fedha hizi kwa upande wa Zanzibar badala ya kutegemea Maafisa wa Serikali ya Mapinduzi ambao hawawajibiki moja kwa moja katika Bunge letu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abdul-hafar Idrissa Juma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali hilo, kwa ruhusa yako naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Abdul-hafar kwa namna anavyopigania Mfuko wa Jimbo kwa Jimbo lake na majimbo mengine ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Sheikh Abdul-hafar swali lako kama ushauri tumelichukua tunakwenda kushauriana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tuone kama ufanisi utapatikana zaidi kwa kuweka Maafisa kule basi Serikali yako ni sikivu na inaweza ikafanya hivyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate.

Na. 415

**Stakabadhi ya mashine za *EFD* kufutika ndani ya muda mfupi**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE K.n.y MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha stakabadhi za mashine za *EFD* ili zisifutike baada ya muda mfupi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kufutika kwa stakabadhi za mashine za *EFD* baada ya muda mfupi kumesababishwa na matumizi ya karatasi zenye ubora hafifu. Aidha, karatasi zinazopaswa kutumika ni zile zenye ubora wa "*thermal paper*".

Mheshimiwa Spika, baada ya kubaini changamoto hiyo, *TBS* kwa kushirikiana *TRA* imeshatengeneza viwango vya ubora wa karatasi hizo vinavyotakiwa na sasa wanaendelea na usimamizi kuhakikisha karatasi zote zinakidhi ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo *TRA* imeboresha mfumo wa usimamizi wa mashine za *EFD* kwa kuwezeshe kupokea taarifa zote za kila risiti inayotolewa na kuitunza katika *saver* zake na hivyo kuwezesha nakala ya risiti hizo kuweza kupatikana wakati wowote inapohitajika. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bilakwate swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Wananchi na wafanyabiashara wamekuwa na mwamko mdogo wa kudai risiti.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu ili wananchi na wafanyabiashara wawe wanadai risiti?

Swali la pili; Wafanyabiashara wengi hawana mashine hizi za *EFD* pia zilizopo nyingi ni mbovu, unapokwenda madukani unakuta hawana mashine.

Je, Serikali sasa ina mpango gani wa kununua mashine kusambaza kwa wafanyabiashara wote ili kuongeza mapato? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Innocent Bilakwate kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wananchi wengi wana mwamko mdogo wa kudai risiti na baadhi ya wafanyabiashara wanakuwa wazito kutoa risiti. Mikakati ya Serikali ni kutoa elimu, kuendelea kuhamasisha na nitoe wito kwa *TRA* kuendelea kutoa elimu kupitia vyombo vya habari vyote ndani ya nchi ikiwezekana hata nje ya nchi, vile vyombo ambavyo huwa vinasikilizwa sana. Pia ninawaomba Wabunge wenzangu kutoa taaluma hiyo kwa wananchi wetu kudai risiti baada ya kununua bidhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, tunaliangalia kwa kweli kutoa mashine za *EFD* tunaweza tukatoa hivyo hapo baadaye, kwa mwaka huu wa fedha hatutaweza kutoa lakini tutalingalia baadaye ikionekana ipo haja na fedha ipo ya kutosha basi tutatoa mashine hizo kwa wananchi wetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Benardeta Kasabago Mushashu swali la nyongeza.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mashine za *EFD* ni za gharama sana lakini mtu akibadilisha biashara kwa maana ya *TIN* analazimika kununua mashine mpya. Kwa nini Serikali isiweke utaratibu wa badala ya kununua mashine mpya

wakaondoa ile *program* akaendelea kutumia mashine ile ile kwa kubadilisha tu *program*? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Mbunge huo ni shauri tunauchukua na tunaufanyia kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 416

**Kuboresha mifereji Bonde la Mto Pangani**

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itasaidia kukarabati mifereji ya Marwa, Kwasita, Magereza, Gunge na Kirua katika Bonde la Mto Pangani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Bonde la Mto Pangani katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Bonde hili ni pamoja na skimu nyingine pia linajumuisha skimu za Kirya, Marwa, Kwasita, Magereza, Gunge, Kirua na Ruvuna kwa upande wa Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inaendelea na ujenzi wa skimu ya Kirya ambayo inatarajiwa kukamilika mwaka 2022/2023. Katika mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Skimu za Marwa, Kwasita, Magereza, Gunge na Kirua ili kujua gharama halisi za ukarabati na ujenzi wa skimu hizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. La kwanza; ningemuomba Mheshimiwa Waziri pengine baada ya Bunge tuweze kutembelea katika skimu hizi ili tuweze kuziona zile ambazo kwa kweli ndizo zinazotakiwa zitengewe fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Spika, la pili, katika Kata ya Makanya kuna korongo ambalo wakati mvua inanyesha ndilo linategemewa sana katika umwagiliaji. Ningeomba Serikali, hasa Waziri tuweze kutembelea naye pamoja ili

aweze kuliona hilo Korongo ili na lenyewe liwekwe katika mpango wa kufanyiwa upembuzi yakinifu ili wananchi wa Makanya waweze kupata chakula kwa mwaka mzima. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, Dkt. David Mathayo David, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nipo tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge kwenda kutembelea skimu hizo kuziangalia na ukarabati ambao unahitajika. Vilevile kwa sababu nia yetu ni kuhakikisha hatupotezi maji, Kata ya Makanya kwenye eneo ambapo kuna korongo kubwa ambalo linatuamisha maji tutakwenda pia kuona. Lengo letu ni kuyatumia maji ipasavyo kwa ajili ya kilimo cha nchi yetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Mto wa Motale unahudumia Kata ya Masama Magharibi na Masama Kati na ni skimu kubwa sana inayotegemewa ndani ya Jimbo la Hai. Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati wa skimu hii ikizingatiwa sasa hivi ndani ya Jimbo la Hai kuna changamoto kubwa ya ukosefu wa mahindi? Kwa hivyo, mto huu unaweza kutumika kuweza kufanya kilimo cha umwagiliaji. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunafahamu umuhimu wa Mto Motale katika kuhakikisha kwamba wakulima wa Wilaya ya Hai wanafanya kilimo cha umwagiliaji. Jambo alilolisema la ukarabati, namwahidi Mbunge kwamba mimi, yeye na watalaam wetu tutaongozana kwa ajili ya kwenda kuangalia eneo husika. Baadaye baada ya kushauriwa vyema, basi tunaona namna ya kuingiza katika mpango wa Serikali ili wananchi wa Hai waweze kunufaika na kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA RASHID KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, ni lini watakamilisha Mradi wa Umwagiliaji wa Bonde la Liuni ambao ulianzishwa muda mrefu lakini haujakamilika Likonde na kufanya ukarabati katika kilimo cha umwagiliaji Kijiji cha Nambecha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyatamka ni maeneo ambayo yapo katika

mkakati wa Wizara kuhakikisha tunawezesha wakulima wa eneo hilo kulima kupitia kilimo cha umwagiliaji. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutatuma wataalam wetu kwenda kuyaangalia maeneo hayo ili baadaye tuingie katika mpango wetu wa Serikali kuhakikisha kwamba tunakarabati skimu hizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali la nyongeza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mradi wa Chela ni mradi wa muda mrefu sana. Swali langu, je, ni lini sasa Serikali itakwenda kuweka fedha za ukarabati wa Mradi wa Umwagiliaji wa Chela pia na kukarabati mitaro ile na miundombinu kwa ujumla?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Iddi Kassim, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hili naomba niliseme katika Bunge letu Tukufu kwamba, kwa kutambua kuna umuhimu mkubwa sana wa ukarabati wa miradi mbalimbali ya umwagiliaji; Wizara tumeiagiza Tume ya Maendeleo ya Umwagiliaji kuhakikisha inaipitia miradi yote nchi nzima kwa ajili ya kufanya tathmini na kujua *status* zake, tujue ipi inahitaji ukarabati mkubwa, ipi inahitaji ukarabati mdogo, ipi inatakiwa tuanze upya, lengo letu ni kuhakikisha miradi hii inafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa Mheshimiwa Mbunge nimwaahidi tu kwamba, katika hayo ambayo

ameyasema pia tutaingiza katika mpango wetu ili tuhakikishe kwamba wananchi wake wananufaika na kilimo cha umwagiliaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 417

**Kukamilisha Vituo vya Rasilimali za Kilimo**

**MHE. YUSTINA A. RAHHI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha uwekaji wa samani na vifaa vya kufundishia katika Vituo vya Rasilimali za Kilimo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilijenga Vituo vya Rasilimali za Kilimo vya Kata 289 katika Halmashauri 184 kati ya mwaka 2007 na 2011. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imeanza uwekaji wa samani na vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya kufundishia katika vituo hivyo na kwa mwaka huu wa fedha Wizara itawezesha Vituo 34 vya Halmashauri 27 za Mikoa ya Dodoma, Singida, Morogoro, Tabora, Simiyu, Mwanza, Geita, Lindi, Mtwara, Mbeya, Songwe na Iringa. Kwa ufupi, Wizara itaendelea kuweka

samani na vifaa vya kufundishia katika Vituo vyote vya Rasilimali za Kilimo vya Kata vilivyojengwa nchini na kutumika kama *Centre of Excellence*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali langu la kwanza; ni vituo vingapi vya rasilimali za kilimo vilikwishabadilishwa matumizi katika Serikali za Mitaa na kwa maagizo sasa ya Waziri ni vingapi sasa vimerudishwa ili kuendelea na matumizi yake ya kawaida?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; Serikali ina mpango gani sasa kuwateua waratibu watakaoratibu mafunzo katika Vituo hivyo vya Rasilimali za Kilimo ili kuratibu mafunzo kwa wakulima na wafugaji na kwamba vitengewe bajeti kidogo ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri swali la nyongeza la kwanza linahitaji takwimu, kama unazo takwimu utamjibu Mheshimiwa Mbunge, kama huna takwimu kanuni zinakuruhusu kumpatia Mbunge baadaye. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, ni kweli nahitaji takwimu, nitaomba nimpatie Mheshimiwa Mbunge

takwimu sahihi baada ya kuwa nimejiridhisha ni vituo vingapi ambavyo vimebadilishwa matumizi. Hata hivyo, tayari tumeshawaandikia wahusika kwa maana ya kurudisha vituo hivi kurudi katika matumizi yake ya awali kwa ajili ya kuwa ni sehemu ya rasilimali za kilimo. Kwa hiyo, baadaye nitampatia taarifa sahihi Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, la pili la kuhusu uteuzi wa Waratibu, tunapokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, tutalifanyia kazi ili kuwepo na waratibu katika vituo hivi na lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba tunatoa elimu ambayo itamfikia mkulima kwa wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pale Jimboni Kibaha kwenye Kitongoji cha Disunyala kipo Kituo cha Rasilimali za Kilimo kilichoanza kujengwa tangu mwaka 2007 na mpaka leo hakijakamilika kujengwa. Je, nini mpango wa Serikali kumalizia kituo kile?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Michael Mwakamo, Mbunge, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, jambo hili Mheshimiwa Mbunge alishalileta ofisini, tumezungumza na tulimpa ahadi ya kwamba lengo letu ni kuhakikisha kwamba tunakamilisha

Vituo vyote vya Rasilimali za Kilimo vipo katika Kata ili mwisho wa siku tuweze kuwafikia wakulima kwa ukaribu. Katika baadhi ya maeneo tumelenga kuvifanya vituo hivi kuwa ni *mechanization center* ambayo itasaidia wakulima kwenda kukopa au kukodisha vifaa vya kilimo kupitia *centers* hizo. Kwa hiyo, nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, pale kwake pia tutakamilisha ili mwisho wa siku malengo yaliyokusudiwa yaweze kutimia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Madini, Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlagila, Mbunge wa Kyela, sasa aulize swali lake.

Na. 418

**Utafiti kuhusu uchimbaji madini na upungufu wa samaki katika Mito na Maziwa**

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE** aliuliza:-

Je, uchimbaji wa madini kando ya mito na maziwa ni chanzo cha upungufu wa samaki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Steven L. Kiruswa, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila, Mbunge wa Jimbo la Kyela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kuwa uchimbaji wa madini umegawanyika katika aina kuu mbili, uchimbaji juu ya ardhi na ule wa chini ya ardhi *(surface and underground mining)* na unafuata Sheria ya Madini, Sura 123 ambayo hairuhusu uchimbaji wa madini katika vyanzo vya mito na maziwa. Endapo shughuli za uchimbaji zitafanyika kando ya mito au maziwa, zitafanyika umbali wa mita 60 kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, aidha, kabla ya shughuli za uchimbaji wa madini kufanyika katika eneo husika tathmini ya mazingira hufanyika na kutathmini athari za kimazingira ikiwemo viumbe hai pamoja na vyanzo vya maji. Hivyo, hakuna uhusiano wa moja kwa moja kwa uchimbaji wa madini na upungufu wa samaki katika mito na maziwa. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Anyugulile Jumbe Mlaghila, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanyika Aprili, 2018 huko Tennessee Marekani, unaonesha kwamba sehemu zenye machimbo ya makaa ya mawe karibu na mito kuna upungufu wa viumbe wa majini kwa asilimia 53 wakiwemo samaki. Swali la kwanza; je, sisi Serikali yetu imefanya utafiti huo na kuja na majibu haya?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, sasa hivi tunaanza kuchimba makaa ya mawe Kiwira *Coal Mine* na Mto Kiwira na Mto Songwe vimeathirika kwa namna hiyo. Je,

ni hatua gani zinazochukuliwa kwa Serikali ili kusiendelee kupatikana kwa athari hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Ally Mlaghalila, Mbunge wa Kyela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa taarifa anayosema kwamba kuna tafiti za kidunia zinazothibitisha kwamba uchimbaji wa makaa ya mawe una uhusiano na kupungua kwa samaki katika maziwa na mito; nikiri kwamba sisi hatuna *scenario* kama hiyo katika Nchi yetu ya Tanzania kwa sababu hatuna uchimbaji katika maeneo ya karibu na mito ambayo ina samaki au maziwa ambayo kuna upungufu uliobainika kwa tafiti za kisayansi.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba katika eneo la machimbo ya makaa ya mawe lililoko Kiwira na Kabulo tuna Mradi unaoitwa Kiwira-Kabulo *Coal Project* ambao uko chini ya taasisi yetu ya *STAMICO*. Katika eneo Kasumulu, Wilaya ya Kyela ilianzishwa *site* ndogo ya heka mbili kwa ajili ya kuwa *selling point* ya yale madini kutokana na shida ya barabara ya kutoka Kabulo kwenda Kiwira kuliko na kituo kikubwa cha makaa ya mawe ya *STAMICO*. Kwa sasa hivi, barabara hiyo ya kilomita saba ilishakamilika na utaratibu wa kuhamisha kile kituo umeshafanyika na kuna tani 1,200 za makaa ya mawe mpaka kufikia mwezi Agosti, 2022 yatakuwa yameondolewa yote, ila tahadhari zote zilichukuliwa.

Mheshimiwa Spika, kwanza; kulingana na Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004, Kifungu 57(1) hairuhusiwi kufanya shughuli za kibinadamu ndani ya mita 60 kutoka ukingo wa mto. *Site* iliyotengwa kule katika mradi huu wa makaa ya mawe kule Kasumulu upo mita 120; lakini kana kwamba hii haitoshi makingamaji ya kuchepusha maji yasielekee mtoni yamejengwa na kuna mashimo makubwa kama mvua itanyesha na maji yakatiririka yakaingia mle yakakaukia humo. Pia kana kwamba hiyo haitoshi, kulingana na Kifungu cha 57(1) cha Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004, sisi kama Wizara ya Madini tunazingatia sana suala la utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria hiyo, Kifungu cha 107(2) cha Sheria ya Madini Na. 123, kinazingatia utunzaji wa mazingira kwamba baada ya ile *site* kuachiwa tutapenda kuirejesha na kuzungushia *fence* na kutumika kwa matumizi ya kufundisha wananchi wa eneo la Kyela na Ileje namna ya kutengeneza makaa mbadala ya makaa ya mawe yanaitwa *Coal Breakage*. Kwa hiyo, hakuna athari ya mazingira na sisi tupo makini. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe huwezi kupewa nafasi tena ulishauliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu, sasa niwatangaze wageni tuliopo nao Bungeni siku ya leo. Kwanza ni wageni wa

Bunge kutoka Kilimanjaro *International Leather Industries Company Limited* ambao ni Ndugu Donald Hosea Nkomavantu ambaye ni Meneja Masoko na Mauzo. Yupo pia Ndugu Fredrick Njoka ambaye ni Afisa Mwasiliano na Masoko. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wetu hawa kutoka Kilimanjaro *International Leather Industries Company Limited* watakuwa na maonesho hapa Bungeni kule nyuma ya Ukumbi wa Msekwa, wameleta bidhaa mbalimbali za ngozi ambapo wanatamani Waheshimiwa Wabunge mzione, lakini muone namna ambavyo ninyi wenyewe mnaweza kuzitumia lakini wapiga kura wenu mnaweza kuwashawishi waanze kutumia bidhaa zetu za ndani na zina viwango vya kutosha. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tukazitazame hizo bidhaa wamekuja nazo kwa wingi kabisa na Kauli Mbiu yao inasema "*Ngozi Zetu Bidhaa Zetu*". Kwa hiyo, karibuni sana wageni wetu na Waheshimiwa Wabunge mnaombwa mkatazame hayo mambo mazito yaliyoletwa na hawa ndugu zetu wa *International Leather Industries Company Limited.*

Wabunge ni pamoja na Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, maana ninyi mna taasisi ambazo mnazinunulia huko vifaa vya kutendea kazi. Kwa hiyo, ni muhimu badala ya kuagiza kule mbali mkishaziona hizi bidhaa mnaweza kuagiza sasa hapa nchini kwenye viwanda vyetu wenyewe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wa Wabunge mbalimbali ambao wapo hapa. Karibuni wote wageni wa Waheshimiwa Wabunge tusimame sote kwa pamoja. Karibuni sana Bungeni wageni wetu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, kwanza ni wanafunzi 120 na Walimu 10 kutoka Shule ya Msingi Chang'ombe ya Jijini Dodoma karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wanafunzi 70 na Walimu 10 kutoka Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Arusha *City Boys* ya Olasiti ya Jijini Arusha. Karibuni sana na tunawatakia kila la kheri katika masomo yenu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, tunaendelea na ratiba iliyopo mbele yetu.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

## Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**na**

## Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, na hapa ninayo orodha ya Wabunge ambao wameomba kuchangia. Tutaanza na Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, atafuatiwa na

Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Kabudi na Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar ajiandae.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Vile vile kwa namna ya pekee namshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa Watanzania na kutufanya sisi Watanzania leo kutembea kifua mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vitabu vyetu vya dini vinasema, mtu asiyemshukuru mtu, basi hamshukuru Mungu. Kwa sababu mtu anamwona, na kama hamshukuru, basi hawezi kumshukuru Mungu ambaye hamwoni. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Mama Samia kwa kila jambo jema analolifanya katika nchi hii. Mwenyezi Mungu atampa heri, atampa umri mrefu na atamjalia kila jambo jema katika maisha yake yote. Amina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kitabu cha bajeti cha Wizara ya Fedha ukurasa wa 75 mstari wa tano kutoka chini, Waziri wa Fedha anasema, namnukuu: "nitumie nafasi hii kuwahakikishia Watanzania kuwa tutaweka nyasi bandia kwenye viwanja vitano kwa kuanzia Mwanza, Arusha, Tanga, Dodoma na Mbeya kwa ajili ya kukuza michezo." Huu ni mpango.

Mheshimiwa Spika, pia ukichukua kitabu cha bajeti cha Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, ambayo inaeleza dhamira, napenda kumnukuu Waziri na ningependa angekuwepo lakini hayupo, bahati mbaya sana; anasema yeye, katika kuhakikisha Tanzania inakidhi vigezo vya kuandaa mashindano ya Kimataifa na Kikanda, Serikali katika mwaka 2022/2023 imetenga kiasi

cha Shilingi bilioni 10 kwa ajili ya viwanja vya Dodoma, Sheikh Amri Abeid, Sokoine Mbeya na pia Uwanja wa Uhuru pamoja na Benjamin Mkapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa malengo na mpango haviendani, ni vitu viwili tofauti kabisa. Kwa sababu leo kwenye soko ukienda kununua *artificial turfs* (nyasi bandia), kwenye soko leo ukiangalia unakuta *square foot* moja ya hizo *turfs* ambazo ni *supreme* utaipata kwa Dola 3.39, na hizo ndiyo zenye kiwango cha juu kabisa. Kwa kiwango cha chini kabisa ambayo tunaita *TFD* utaipata kwa Dola 1.65. Maana yake nini? Maana yake, uwanja mzima wa mpira *una-square feet* 76,900, maana yake itakuwa ni sawa na Dola za Kimarekani 260,691, na hiyo nyingine itakuwa kama Dola 126,885. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa *ukizi-convert* hizo zinakuwa kama Shilingi milioni 600 kwa *supreme,* na mpaka tufanye *installation* kwenye viwanja, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nasema na wewe! *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ngwali!

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Sawa, sawa!

**SPIKA:** Mheshimiwa Ngwali!

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Ah, nazungumza Mheshimiwa. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Unasikilizwa.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Aah, sawa.

**SPIKA:** Unasikilizwa.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Sawa, sawa.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Wewe unazungumza na mimi humu Bungeni, huzungumzi na Waziri. Hata ukiwa unaongea nitazame mimi hapa, ndiyo kazi yangu kukusikiliza. *(Makofi)*

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Spika, haya sawa. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, kwa kiwanja kimoja kuwekwa hiyo *artificial turfs* ni kama Shilingi milioni 800 na kidogo hivi. Sasa ukivichukua viwanja vyote ambayo Serikali wameeleza kwamba wataweka hizo nyasi bandia, utakuta sasa, ukiweka hizo nyasi bandia *(artificial turfs)* katika hivyo viwanja, hivyo viwanja huwezi kutumia katika *international level.* Kwa hiyo, kama una lengo la kuandaa *AFCON* hivyo viwanja vitakuwa havifai kwa sababu *Regulation* za *FIFA* haziruhusu *artificial turfs* kufanyika mashindano ya *international level*. Kwa hiyo, lengo ni kuweka fedha katika hivyo viwanja na utakuwa huna kiwanja, maana yake viwanja vyote vya Jamhuri, Sokoine, CCM Kirumba, Mkwakwani, vyote hivyo ukiviweka nyasi bandia, maana yake umebakiwa na kiwanja kimoja cha Benjamin Mkapa. *FIFA* wanatumia *natural.* Kwa hiyo, hata kiwanja chako cha Sokoine kitakuwa hakiwezi kuchezewa katika *international level*. Kwa hiyo, malengo na mipango ni tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi tu *FIFA* wamekataa viwanja *artificial.* Marekani Canada pamoja na Mexico wanaandaa hiyo *World Cup* ya mwaka 2026 na *CAF* wanafuata viwango vya *FIFA* vya viwanja. Viwanja vilivyokataliwa naomba nivitaje; *MetLife Stadium* ya *New York* pamoja na *New Jersey* imekataliwa kwa sababu ina-*artificial*. *SoFi Stadium* ya Los Angels imekataliwa kwa sababu ina-*artificial.* Tena wamewataka Marekani wabadilishe. Siyo wamevikataa kabisa, wabadilishe kupeleka katika *natural*. *Levi's Stadium* ya *San Francisco* viwanja 11 vimekataliwa. *Lumen Field* ya *NRG Stadium* ya *Huston* imekataliwa. *Lincoln Financial Field* ya *Philadelphia* imekataliwa, yaani viwanja 11 vimekataliwa na *FIFA* kwa sababu *FIFA* wanatumia *natural* na *CAF* wanatumia viwango vya *FIFA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata uwanja wa *Azam Complex,* ule *preliminary* unaruhusiwa kucheza, lakini hauruhusiwi kucheza robo fainali. Ukifika kiwango cha robo fainali ule uwanja haufai kuchezea. Kwa hiyo, ukiweka nyasi bandia *(artificial turfs)* unazuia huo uwezekano wa Tanzania kuwa mwenyeji au *ku-host* mashindano ya *AFCON*. Ndiyo maana nasema mpango na dhamira ni vitu viwili tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona wametaja viwanja vingi ambavyo watavifanyia ukarabati, siyo ukarabati huo wa kuweka nyasi bandia, nitatoa ushauri baadaye; lakini kwa nini Zanzibar, *Amani Stadium* na Gombani Pemba havipo? Tena napendekeza hivyo viwanja Mheshimiwa Waziri vikae katika mpango wako. Kwa sababu kile ni kituo na pia ni kituo rahisi, na vile viwanja ni vya Serikali, hatuna haja ya *ku-negotiate* na mtu yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Zanzibar ni viwanja vya Amani pamoja na Gombani Pemba kama kituo, basi viweke katika mpango wako Mheshimiwa Waziri, lakini siyo mpango wa kuweka nyasi bandia. Kwa sababu uwanja wa Amani hauwezi kutumika sasa hivi katika *international level* kwa sababu una nyasi bandia, tena *grade four,* kama shamba la bibi; na kama ambavyo kiwanja cha Gombani Pemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba, kuna njia mbili tu, au kuna njia moja ya kufanya, kwamba, *high brick system* ndiyo inayotumika sasa hivi hasa kwa viwanja vya *IPL*. Maana yake na *FIFA* wanavitambua kama ni *natural turf*. Unachukua *grass master* ndiyo walioweka *turfs* zile katika uwanja wa *Stamford Bridge* na *Emirate* pamoja na viwanja vingi vya Uingereza. Pia *Swiss grass* wao ndio walioweka *turf* katika uwanja wa *Man City* ambapo wao ndio walioshinda Kombe la Dunia *last time* kuweka viwanja vya Urusi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia *Atlas Turf International,* wao ndio wameshinda *Qatar* kuweka *turfs* ambapo aina zao za nyasi wanaziita *Platinum TE Paspalum*. Hizo ndiyo nyasi ambazo wanatumia. Kwa hiyo, tutumie makampuni makubwa ya nje yaje yaweke nyasi katika viwanja vyetu hivi. Siyo nyasi bandia watutengenezee hivi viwanja, tutangaze tenda *international*, kwa sababu hakuna watu wa ndani ambao wanaweza *ku-deal* na huo utengenezaji wa viwanja ili tukidhi hicho kiwango cha *FIFA* na *CAF* wanachokitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa kwa sababu alikuwa anazungumzia michezo, ngoja nitangaze hapa matokeo ya mechi zilizofanyika tarehe 18 Juni, 2022 na kwa sababu kuna watu walipigwa magoli hapa, ngoja nisimame. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, siku ya tarehe 18 Juni, 2022 kulikuwa na michezo kati ya *Bunge Sports Club* na Waandishi wa Habari katika michezo ifuatayo:-

Mpira wa Pete: Bunge *Sports Club* walishinda 15 kwa 13, na nyota wa mchezo huo nilikuwa ni mimi hapa. Jamani sijajua vigezo, kwa sababu wanaosema ni wale waliokuwa nje. Kwa hiyo, nitakuwa nimewawakilisha vizuri. Kwa hiyo, kwa upande wa mpira wa pete, Bunge iliwashinda Waandishi wa Habari. Upande wa mpira wa miguu, timu ya Waandishi wa Habari za Michezo iliwafunga kwa taabu sana timu ya *Bunge Sports Club* magoli mawili kwa nunge. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tuendelee kufanya mazoezi. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Kabudi, atafuatiwa na Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar na Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika ajiandae.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia katika bajeti hii ya Serikali ya mwaka 2022/2023. Nachukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu Rahim kwa kunijalia

uhai, na kwa kunipa afya ya kuniwezesha kusimama hapa leo ili nami nitoe mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa uongozi wake madhubuti, kwa uongozi wake bora na kwa mwaka huu kutuletea mapendekezo ya bajeti yanayoakisi maslahi na matlaba yaani *expirations* za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nichukue fursa hii kumpongeza sana Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, Naibu Waziri Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Katibu Mkuu wa Wizara na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Bwana Emmanuel Mpawe Tutuba na Manaibu Katibu Wakuu na wote katika Wizara ya Fedha kwa kutuletea bajeti nzuri yenye ubunifu na inayozingatia mahitaji na matarajio ya wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba yangu binafsi na ya wananchi wa Jimbo la Kilosa ambalo nimepata heshima ya kuwawakilisha, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan kwa fedha nyingi ambazo ametupatia wana Jimbo la Kilosa katika mwaka huu wa fedha 2021/2022 katika sekta ya afya, elimu, maji, barabara, madaraja, mawasiliano vijijini, kilimo cha umwagiliaji na kadha wa kadha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutupatia jumla ya Shilingi 2,347,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Berega ambayo tumepata Shilingi bilioni moja. Shule ya Sekondari ya Berega itakuwa ni ya aina yake. Kwa

upande wa *O'Level* ni shule ya Kata kwa upande wa *A'Level* wao ni shule ya Kitaifa kwa ajili ya wavulana Bweni, Sayansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutupa Shilingi milioni 470 kujenga Shule ya Kata ya Maguha. Wote mnaosafiri kwenda Dar es Salaam, mara baada ya kupita Mtumbatu ambako mnanunua nyanya, vitunguu, maharage na vinginevyo, mtaiona Shule ya Berega na mtaiona Shule ya Maguha. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa jumla ya Shilingi bilioni 2.405 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya na zahanati. Namshukuru kwa namna ya kipekee kwa kutoa jumla ya Shilingi milioni 900 kujenga kituo cha afya katika milima ya Uponera. Wale wanaoifahamu milima ya Uponera haifikiki kwa urahisi. Kutoka Gairo mpaka Uponera ni muda wa saa nne. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Maisha ya akina mama wengi waliofariki wakati wa kujifungua wakishuka kwenda Mamboya mwendo wa saa nne au kwenda Gairo mwendo wa saa tano, sasa yanakwisha kwa Shilingi milioni 900 ambazo Mheshimiwa Rais ametoa kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Uponera katika Kata ya Mamboya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nashukuru kwa kituo cha afya cha Kata ya Chanzulu Ilonga; Shilingi milioni 515 na Kituo cha Afya cha Ntembo Kata ya Mabula Shilingi milioni 450; pia kwa Shilingi milioni 200 kwa ajili ya kujenga *ICU* katika hospitali ya Wilaya ya Kilosa, bila kusahau zahanati mbili za pembezoni mwa Jimbo letu ambalo ni kubwa sana,

yaani Zahanati ya Unone Kata ya Rudewa Shilingi milioni 80 na Zahanati ya Lumbiji kwa Shilingi milioni 80.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madaraja, namshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa upendeleo wa aina yake. Kwanza kwa kutupa fedha ya kujenga daraja la Berega katika Mto Mkundi ambalo linagharimu Shilingi 7,900,000,000/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni kuenzi jitihada alizozifanya Rais wa Awamu ya Pili, Benjamin William Mkapa aliyejenga daraja, kwa bahati mbaya likasombwa na maji; pia Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete aliyejenga daraja ambalo bado lipo lakini limevunjika. Kwa hiyo, Shilingi bilioni 7,900,000,000/= zitajenga daraja hilo, nasi kwetu tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kwa ajili ya Shilingi milioni 500 kwa ajili ya kujenga daraja la Masombawe Kata ya Berega; na Shilingi milioni 160 kwa ajili ya kujenga daraja la watembea kwa miguu, bodaboda na baiskeli kwa Kijiji cha Ruwemba ambacho kukifikia unatumia mwendo wa saa nne kupita wilaya tatu ili kufika Kijiji cha Ruhemba katika Kata ya Kidete. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tunamshukuru kwa fedha aliyotupa kwa ajili ya miradi ya maji hasa katika Mji Mdogo wa Dumila. Kwanza alitupa Shilingi 1,200,000,000/= na sasa ametupa Shilingi bilioni 530 ili kuhakikisha Mji wa Dumila unapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru pia Mheshimiwa Rais kwa Shilingi milioni 700 kwa ajili ya

kujenga tanki la maji na mfumo wa maji katika Kata ya Rudewa katika Jimbo la Kilosa. Hii ni baadhi tu ya miradi ambayo imepatiwa fedha na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan katika mwaka huu wa fedha na katika mwanzo wa uongozi wake. Sisi wana Kilosa tunamshukuru sana na kwa lugha ya Kikaguru nimwambie Kwimage Lugano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nategemea kabisa katika bajeti hii tunayoijadili sasa barabara ya Rudewa kwenda Kilosa itakamilika kwa ujenzi wa madaraja manne yaliyosalia; daraja la Mto Kobe, daraja la Mto Kilonga na daraja la Mazinyungu na hatimaye daraja kubwa la kuvuka Mto Mkondoa kwenda Mikumi na baadaye kwenda Iringa, Mbeya, Tunduma na Zambia. *(MakofI)*

Mheshimiwa Spika, vile vile tunashukuru sana kwa fedha ambayo tunajua imepangwa kwa ajili ya kuanza kujenga barabara ya Kilosa kwenda Mikumi. Barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu na itasaidia sana katika utalii, na pia katika mazao ya miwa na mazao mengine yanayolimwa katika Jimbo la Kilosa na Mikumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa bajeti tunayoijadili, napenda sana kumshukuru Waziri wa Fedha, kwa kupendekeza kusamehe kodi ya ongezeko la mtaji, *(Capital Gain Tax)*, kwenye uhamishaji wa haki na taarifa za madini kwenda kwenye kampuni za ubia zinazoundwa baina ya Serikali na wawekezaji na uhamishaji wa hisa, *(Free Carried Interest)* kutoka kampuni ya ubia kwenda kwa Serikali. jambo hili litarahisisha utekelezwaji wa mikataba hiyo, pia litarahisisha mazungumzo kwa sababu lina faida kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami nichukue nafasi hii kumshukuru tena Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa heshima kubwa sana aliyonipa na kwa kuniamini kwa kiasi kikubwa sana kunikabidhi majukumu ya kuwa Mwenyekiti wa Timu Maalum ya Rais ya Majadiliano ya Serikali, yaani kwa kiingereza *(Special Presidential Government Negotiation Team)*. Ni heshima kubwa sana ambayo sitaisahau katika maisha yangu yote nitakayokuwa duniani. Sijawahi kupata heshima kama hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua hizi ambazo Waziri wa Fedha amezichukua kwenye suala hili la *capital gain tax* litatusaidia sana. Tuna aina mbili ya *free carried interest* na ningeomba nitumie nafasi hii kuzifafanua. Iko aina ya *free carried interest,* yaani hisa ambazo Serikali inapewa bila kulipiwa za aina mbili, iko ambayo ni *diluted free carried interest shares na iko* ambayo *ni non dilutable free interest carried shares;* nini tofauti yake?

Mheshimiwa Spika, ile ya kwanza ambayo siyo *dilutable,* kila mwekezaji anapoongeza hisa wewe usipoongeza mtaji thamani ya hisa zako inashuka na mwisho inaweza kufifia kabisa. Tanzania tumechukua aina ya pili ya *non dilutable free carried interest* maana yeke nini? Yeye kila anpoongeza mtaji wewe unabaki na asilimia 16 ileile katika ule mtaji ulioongezeka. Maana yake thamani ya hisa zako haishuki. Nchi nyingi za kiafrika na ninaomba nisizitaje kwa heshima ya nchi hizo, zilichukua aina ya kwanza ya *dilutable* ndiyo maana nyingine zilianza na asilimia 50 leo zina asilimia Mbili. Nyingine zilianza na asilimia 20 leo zina asilimia Tano, lakini sisi kwa aina hii ya hisa tutaendelea kuwa na asilimia

hiyohiyo katika maisha yote ya mgodi au mradi huo bila hisa hizo kupungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo tumelifanya katika Mabadiliko ya Sheria ya 2017 ya kuunda kampuni za ubia za madini kati ya Mwekezaji na Serikali. mara nyingi tunasahau jambo hili muhimu sana, iko tofauti kati ya rasilimali na mali. Madini ni rasilimali, lakini ili yawe mali ni lazima yatolewe leseni kama ambavyo ardhi ni rasilimali, lakini ili ardhi hiyo iwe mali ni lazima upewe *Tittle Deed,* yaani Hati ya Umiliki. Huko nyuma sisi tulibaki na rasilimali, lakini *license* au leseni zilipewa kampuni za nje. Kwa hali ya sasa katika majadiliano yote yanayoendelea leseni sasa zinamilikiwa na kampuni ya umoja ya ubia. Maana yake sasa unamiliki leseni ambayo ni mali na madini ambayo ni rasilimali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hilo ningependa nifafanue, ile *free carried interest* sio kwai le kampuni hodhi ni kwa mgodi husika na mradi husika. Kwa hiyo, kwa mfano katika kampuni ya *Twiga Minerals* Serikali ina asilimia 16 katika Mgodi wa Bulyankulu, *ring fenced,* asilimia 16 katika Mgodi wa *North Mara, ring fenced,* na asilimia 16 katika Mgodi wa Buzwagi ambao unakaribia kufungwa, *ring fenced* na asilimia 16 katika Kampuni ya pamoja. Maana ya ku-*ring fence* ni kwamba, faida au hasara ya mgodi mmoja haiwezi kuathiri faida au hasara ya mgodi mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumefanya pia hivyo katika Kampuni ya *Tembo Nickel,* itayaoanza kuchimba madini ya *nickel* ambayo ni madini ya kimkakati kule Kabanga. Serikali ina asilimia 16 kwenye Mgodi wa Kabanga, lakini pia ina asilimia 16 katika *smelter* itayaojengwa Kahama,

pia ina asilimia 16 katika kampuni hodhi. Hivyohivyo ndivyo tumefanya kwa kampuni nyingine za *Nyati Sand Minerals,* lakini pia Kampuni ya Faru itakayochimba madini ya *graphite* huko. Kwa hiyo, maamuzi hayo yaliyochukuliwa na Waziri wa Fedha yanatusaidia kutoka katika kawaida tuliyoizoea ambayo imekuwa haitupi faida zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona kengele ya pili imegonga. Na nisikuweke mahali pagumu kuamua nikae au nisikae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nitachangia katika maandishi tofauti ya aina tatu za mikataba ya *concession* ya *PSA* na mikataba ambayo sasa tunaingia. Hiyo, nitachangia kwa maandishi au nikipata nafasi nyingine wakati wa bajeti hii kabla ya kupiga kura, kama inaruhusiwa, nitaomba tena nipate nafasi nilieleze hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa heshima hii na ninamshukuru sana Waziri wa Fedha kwa ubunifu na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa heshima aliyonipa, lakini kwa upendo kwa wana-Kilosa. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar, atafuatiwa na Mheshimiwa Deogratius Philip Mwanyika. Mheshimiwa Tauhida Galos Cassian Nyimbo ajiandae.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ninakushukuru siyo tu kwa sababu ya kunipa nafasi hii, lakini pia kwa namna bora ambavyo

unaongoza Bunge hili kwa hekima na busara nyingi sana. Kwa hiyo, nikupongeze sana na nikushukuru sana kwa namna bora ambavyo unaongoza Bunge letu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza na ninamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa namna anavyoendelea kutupigania Watanzania na maendeleo ambayo anaendelea kutuhangaikia na tunavyopiga hatua hizi za kimaendeleo. Bajeti hii ambayo iko mbele yetu ni bajeti ambayo inaenda kutatua changamoto za Watanzania, inaenda kumgusa kila Mtanzania. Bajeti hii imewagusa wamachinga, bajeti hii imewagusa wakulima, bajeti hii imewagusa watumishi wa umma, lakini bajeti hii imeyagusa makundi yote, vijana, walemavu, wanawake, hata wanamichezo bajeti hii haiwaacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunasema kwamba, bajeti hii imekuja katika *right time,* lakini pia ni bajeti ambayo inaenda kutatua changamoto za Watanzania. Nikupongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha, wewe na timu yako, kwa namna ambavyo umewasilisha na umeandaa bajeti hii nzuri sana kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya *industry* ambayo inakua kwa kasi ya kiuchumi sasa hivi duniani ni *Islamic Financing System. Islamic Financing System* sasa hivi inakadiriwa taasisi karibia 400 duniani tayari zinafuata mfumo wa *Islamic Financing* duniani, lakini pia inakadiriwa ukuaji wa *system* hii kwa mwaka ni karibia asilimia 20 kwa mwaka, lakini na nchi nyingi ambazo sasa hivi zinatumia siyo tu zile nchi za kiislamu, lakini hata nchi ambazo siyo za Kiislamu zinatumia mfumo huu. Ukienda *South Africa* wanatumia

*Islamic Financing System,* ukienda *UK,* ukienda Nigeria na nchi za Afrika nyingi hata Kenya wanatumia mfumo huu, lakini kwetu sisi Tanzania bado hatujaweza kuu-*recognize* mfumo huu uweze kutumika katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, bado tunahitaji kufanya mabadiliko kwenye sheria zetu. Kwa mfano, *Banking Act,* hii inatakiwa pia ifanyiwe marekebisho ili kuutambua mfumo wa *Islamic Financing* ili uweze kutumika Tanzania kwa sheria, pia tufanye marekebisho kwenye *Insurance Act* ili pia iweze kutambua *takaful* kama ni *Islamic Insurance* ambayo inakwenda kutatua matatizo mbalimbali yanayohusiana na insurance za kiislamu, pia tunahitaji tufanye mabadiliko kwenye *capital market and security* ili kuweza kutambua *Islamic bond* ambayo inaitwa *sukuk* ambayo itawawezesha wawekezaji wengi ambao hawatumii mifumo iliyoko sasa, wanatumia mifumo ya Kiislamu kuja Tanzania kupiga hodi na kuweza kuwekeza kwa *bond* hizo ambazo na zikonchi nyingi ambazo zinatumia *Islamic Bond* kuweza kutekeleaa miradi yao mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda Nigeria wanatumia mfumo huo, ukienda *UK* pia wanatumia mifumo hii ya *Islamic Bond* ambayo ni *Sukuk,* lakini Tanzania bado hatujaweza kuitambua mifumo hii kisheria. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri tuende tukapige hatua.

Mheshimiwa Spika, siyo kwamba tunakwenda kulitekeleza jambo hili *from nowhere,* kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ukienda Ibara 159(f) imezungumzia juu ya mifumo ya *Islamic Finance* na CCM imeahidi kwamba, ifikapo 2025 jambo hili tayari litakuwa

limeshafanyiwa kazi. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, nakupongeza sana kwa sababu umeshapiga hatua kwenye bajeti yako hii umeweka, umefanya *amendment* kwenye *TRA Act* ile ya mwaka 2008 tayari kuna kipengele umekiweka pale, lakini kile kipengele bado hakijatosha. *Financing System* ina faida kubwa sana kwa Tanzania, lakini pia ina faida kubwa sana kwa uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna hofu sana kwenye jambo hili na Watanzania wengine wanahofu kwamba, aah, kwa nini *Islamic System? Islamic System* hizi benki ni huduma kama huduma nyingine. Ukienda kwa Tanzania tunazo *system* za kidini ambazo zinafanya kazi bila ya ubaguzi na zinatumika kwa watu wote. Ukija tuna shule mbalimbali za kikristo, tuna shule pia za kiislamu, lakini tunasoma kwa pamoja bila ya kubaguana. Pia, tuna hospitali na vituo vya afya mbalimbali ambavyo ni vya kidini, tunaenda kutibiwa kwa pamoja bila kubaguana kidini. Hii pia ni huduma kama huduma zingine na watatumia watu wote au yule ambaye anahitaji na ambaye hahitaji halazimiki kutumia huduma hii. Ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu 2025 tutaenda kuhojiwa na Watanzania kwamba, kwa nini hatukutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwenye jambo hili. Nikuombe sana tuende tukalitekeleze jambo hili kama ambavyo limeahidiwa na Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa nini sasahivi mifumo hii inakwenda kwa kasi sana? Ni kwa sababu ya faida zinazopatikana kwenye *products* ambazo zinazalishwa kwenye *Islamic Banking*. Kwa mfano, miongoni mwa *products* ambazo zinazalishwa kwenye *Islamic Banking* ni *product* ambayo inaitwa *Mudharaba*. *Mudharaba* ni *product* ambayo benki wanampa mtaji mteja anaenda

kufanya biashara, lakini kwa kugawana faida. *Product* kama hii ipo kwenye *conventional bank* kwa maana wao wanapewa mkopo, wakishapewa mkopo wanachokijua wao ni *riba* na marejesho ya mkopo ule. Hawashughuliki na biashara yako wanavyofanya, vyovyote itakavyokuwa, umepata hasara, umepata faida ni wewe mwenyewe, lakini *mudharaba* ambayo ni *product* ya *Islamic* hii benki na wewe, benki na mteja wanashughulika pamoja kwenye biashara yako na mwisho mnagawana faida.

Mheshimiwa Spika, endapo imetokea hasara kwenye biashara yako hiyo, haulazimiki kulipa isipokuwa kwamba, isiwe *negligence* ya kwako wewe kama mteja, lakini kama imekwenda vizuri biashara kwa misingi ambayo mmekubaliana na benki na haikutengeneza faida, hulazimiki kulipa. Leo ukiangalia mifumo yetu ya *conventional* kama hukwenda kulipa ama watakuja kukufilisi au watakupiga mnada yale ambayo umeweka kama dhamana ya mkopo wako, lakini kwenye *Islamic Banking* haipo hivyo, kama umepata hasara, ukipata faida mnagawana na benki na hiyo ni moja katika *product*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini zipo *products* nyingi. Kuna *mudharaba,* kuna *musharafa,* lakini pia kuna *murahaba,* ziko nyingi sana. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri jambo hili tulifanyie kazi na tulifanyie kazi kwa wakati na kwa haraka sana.

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye suala la ushirikiano au ushirikishwaji wa taasisi zetu za Serikali zote mbili; ziko taasisi za Zanzibar ambazo sasahivi zinafanya kazi zake huku Tanzania Bara. Kwa mfano

tunayo taasisi ya *ZIC, Zanzibar Insurance Company,* lakini pia tunayo *PVZ* ambayo pia inafanya kazi huku tunakuomba sana Serikali kwa pamoja tuendelee kushirikiana na taasisi hizi, bado mashirikiano ya taasisi hizi kwa taasisi ambazo ziko Bara ni madogo sana. Kwa hiyo, nikuombe sana na niiombe sana Serikali tuongeze ushirikiano kwenye taasisi zetu hizi za Zanzibar kwa sababu zote hizi ni taasisi za Serikali na zinamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100 kwa hiyo, hatuna haja ya kuziwekea hofu au kuzijengea hofu. Tuzitumie taasisi hizi kama ni taasisi zetu za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie jambo moja, kuna suala la *Foreign Currency Exchange Market.* Ni jambo ambalo limefungiwa sasa kwa muda mrefu na sasa hivi huduma hii inahitajika sana. Mama Samia amekwenda mbio sana amefanya *Royal Tour* kutangaza utalii, watalii watakuja na wameanza kuja, kwa hiyo, tunaziomba hizi taasisi za *foreign exchange* kwa maana ya *Bureau De Change* zirudi na zirudi katika masharti ambayo siyo yale kandamizi kama ambavyo yako sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano eneo maalum la Zanzibar, kumuwekea mzanzibari mtaji wa Bilioni Moja ndiyo aanzishe taasisi hii ya *Bureau De Change* kwa kweli, si jambo rahisi kwa wazanzibari kwa mujibu wa uchumi ambao tukonao bilioni moja ni hela nyingi sana hatuwezi tukapata hata kampuni moja ambayo itaweza kufungua, itakidhi sharti hili la kuweza kufungua hii *Bureau De Change* kwa Zanzibar. Kwa hiyo, nikuombe sana masharti haya yalegezwe, hasa kwa upande wa Zanzibar, kwa kweli Bilioni Moja ni nyingi sana kuweza kufungua *Bureau De Change* kwa upande hasa wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, ninaunga mkono hoja hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deogratius Philip Mwanyika, atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeres. Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina ajiandae.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninaomba nifanye marekebisho ya jina, naitwa Deodatus, ukipenda Deo.

Mheshimiwa Spika, nianze moja kwa moja kwanza kwa kusema kwamba, ninaunga mkono bajeti hii. Bajeti hii ni nzuri na niseme bila kificho nampongeza sana Waziri wa Fedha kwa kutuletea bajeti hii inayojaribu kuakisi wapi nchi hii inakwenda na wapi imetoka. Ni bajeti ambayo inajaribu kutilia maanani matatizo ya wananchi, inajaribu kuleta vilevile *balance* kwenye uwekezaji. Tumeona hatua nyingi za kikodi ambazo zimechukuliwa katika kuifanya sekta ya uwekezaji katika kilimo na viwanda iweze kuwa na hali nzuri zaidi, kwa hiyo nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa nampongeza Mheshimiwa Rais. Kwa kweli, kwa haya ambayo yanafanyika inaonesha kabisa ni uthubutu wa hali ya juu kabisa wa kutaka ku-*address* matatizo ya Watanzania. Tumeona mengi ambayo yamefanyika na hatuwezi kuyataja yote hapa maana muda hautatosha, lakini itoshe kusema nchi yetu imekuwa *stable* kiuchumi, *macro-economic indicator* zote zinaonesha tuko katika hali nzuri tunawazidi wenzetu majirani kwa kiasi kikubwa,

*inflation* iko *within reach* katika *single digit,* Shilingi imeimarika, *reserve* ziko kwenye *4.8* na iko *within reach.* Haya yote ni maendeleo makubwa ni maeneo ambayo yanazidi kufanya uchumi uendelee kukua.

Mheshimiwa Spika, vilevile kipekee nipende kushukuru Serikali,kilio kikubwa cha wananchi ili kuwafanya wawe na hali nzuri tumeona Serikali imejaribu kuweka hiyo ruzuku katika mafuta ni jambo jema, lakini nipende kusisitiza na kusema kwamba, kama kuna eneo tutawasaidia wananchi ni kwenye mbolea.

Mheshimiwa Spika, tunaelewa fika kabisa Serikali ina mpango mahususi wa kutoa ruzuku kwenye mbolea. Niseme wazi kabisa wananchi wamepata matatizo makubwa sana kwa kulima bila kutumia mbolea, hasa maeneo ya kule Njombe, tunahitaji sana ruzuku ya mbolea. Na niombe sana Mheshimiwa Waziri aliwekee mkakati vizuri, Waziri wa Fedha ndiyo mtu ambaye sasa atatoa hizo fedha ili ziweze kwenda kwenye ruzuku. Kuwe na uratibu mzuri wa kuhakikisha ruzuku hii inawafikia wananchi kwa wakati na kusiwe na janja-janja ambayo itawafanya wafanyabiashara waweze kupata faida katika mwenendo wa ruzuku kwa hiyo, niombe sana jambo hili.

Mheshimiwa Spika, nikiwa kama Mjumbe wa Kamati ya Viwanda tulifanikiwa kutembelea baadhi ya viwanda na hasa tulitembelea viwanda vya chuma. Dhima ya bajeti hii ni kuwa na bajeti ambayo itafanya uchumi shindani, viwanda vya chuma kwa ujumla wake bado vina matatizo makubwa sana ambayo yanatokana na ushindani ambao hauko sawa au hauko linganifu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kusema ni vizuri, na ninashukuru Mheshimiwa Waziri amechukua baadhi ya hatua nyingi za kikodi na za kiutawala ili kusaidia viwanda hivi vya chuma, lakini bado kuna maeneo ambayo naona yanahitaji kuangaliwa kwa karibu ili yaweze kusaidia katika kuimarisha sekta. Sekta hii inaajiri karibu watu elfu 10, watu elfu tatu moja kwa moja na waliobaki wote ni mawakala na watu mbalimbali. Vijana wengi, machinga, wako katika sekta hii ya chuma kwa hiyo ni sekta muhimu sana kwenye kutengeneza ajira.

Mheshimiwa Spika, pia kuna maeneo ya kodi ambayo yalitakiwa yabadilishwe na *recommendations* zilitolewa. Kwa mfano, ukiangalia *HS Code 7210.3* na *722599* unaona bado eneo hili lipo *duty* kwenye 25. Ilipendekezwa iwe 35, sasa wale wanaoingiza bidhaa nyingine za chuma ambao wale wanatengeneza migongo tu, hawa wanakuwa na *advantage* kubwa katika biashara hii na kwa hiyo, wana-*affect* wazalishaji. Kwa hiyo, iko haja ya kuangalia kwa karibu sana.

Mheshimiwa Spika, kuna eneo moja kwa sababu ya muda niliongelee, ni eneo la kitu iinaitwa *PED* ambayo ni *Pre-Engineered Design Structures.* Hizi *structures* ni muhimu sana kwa kilimo, ni *structures* ambazo ndio wafugaji hutengenezea mahema, maghala, viwanda na *show rooms.* Hizi *structures* zinaweza zikaagizwa kirahisi na watu ambao wanazileta kwa sababu kodi iliyowekwa hapa inawa-*encourage* wao kuzileta badala ya kampuni zetu kubwa za chuma ambazo zingeweza kutengenezwa hapa. Kampuni hizi zilikuwa zimeomba zipewe *remission* kwenye suala hili ambalo haijafanyika, ningependa sana kumuomba Mheshimiwa Waziri aliangalie lina-*impact* kubwa sana kwenye uzalishaji, kwenye kilimo na kwenye

ufugaji. Kwa hiyo ni vizuri akaangalia hizo ni *H Code* 94062090.

Mheshimiwa Spika, nipende kuongelea kilimo, sisi wananchi wa Njombe ni wakulima wakubwa na tunashukuru sana kwamba kumekuwa na hatua mbalimbali ambazo zimepunguza baadhi ya kodi hasa kwenye misitu, sasa tunakwenda kwenye asilimia tatu ya *cess,* kwa hiyo hilo ni jema, tunamshukuru. Hata hivyo, tuangalie vile vile kwamba sisi tunalima chai kwa wingi sana pamoja na *avocado*. Njombe ina *grow* kubwa avocado *hub* lakini ukiangalia miundombinu na *infrastructure* bado iko nyuma sana.

Mheshimiwa Spika, nimeangalia kwenye bajeti ya Wizara ya Ujenzi, nimeangalia bajeti ya Wizara ya Kilimo, nimeangalia bajeti hii, sisi Njombe tunahitaji kuwa na Uwanja wa Ndege kwa sababu kwenye bajeti tunaongelea ndege tano zitaingizwa au zimeshalipiwa, lakini katika hizo tano moja ni ya mizigo. Hiyo mizigo inatakiwa itoke Njombe, tuna *hub* kubwa sana ya uzalishaji wa parachichi na itakuwa ni *hub* kubwa sana huko mbele ambayo inahitaji usafiri. Katika mipango ya Serikali hatulioni kabisa hilo likijitokeza, kwa hiyo niombe sana liangaliwe tena upya na Njombe iweze kuonekana ikipewa eneo hili.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni Liganga na Mchuchuma. Limeongelewa sana sana katika Bunge hili, mara ya mwisho tulivyoongea tuliambiwa kwamba mazungumzo yamefikia mahali pazuri, wengine wangeweza kusema yamefikia patamu. Hata hivyo, kinachojionyesha ni mradi wa mkakati ambao hakuna mkakati wowote ambao upo kwa sababu hakuna taarifa

tunazopewa kwamba mazungumzo yamefikia wapi. Mradi ule una Liganga na una Mchuchuma, Mchuchuma ndiko ambako kuna makaa ya mawe, makaa ya mawe bei yake imepanda. Sisi Watanzania ni watu wa ajabu, tuna makaa ya mawe ambayo bei yake ni nzuri, lakini bado tunafanya mchezo na mradi huu.

Mheshimiwa Spika, nasema ni mchezo kwa sababu hatuelewi umefikia wapi, tunafahamu Mungu ametupatia haya makaa kwa muda mrefu na makaa haya sasa yana bei nzuri sana. Shirika letu la Maendeleo ambalo limepewa hili jukumu la kuendeleza huu mradi, tunaona kwamba aidha, halina uwezo au watu wetu wanao-*negotiate* hawajafika mahali ambapo wanaweza wakatuambia tatizo ni nini? Tunahitaji kama Watanzania na wananchi wa Mkoa wa Njombe kuelewa Mradi wa Liganga na Mchuchuma umefikia wapi. Nimwombe Mheshimiwa Rais aweke mguu kwenye mguu huu kama alivyofanya kwenye masuala ya gesi na *LNG* ili mradi huu uweze kukwamuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi huu una tatizo lingine ambalo ni kwamba, tunafahamu kabisa *Paris Climate Agreement* inafikia mwisho 2030 sasa tuna makaa ya kuzalisha kwa miaka 140 kwa tani milioni tatu kila mwaka, maana yake tuna tani zaidi ya 428 lakini tuna miaka nane tu ya uzalishaji kama tungekuwa tumeanza kuzalisha leo. Kwa hiyo unaona bado tuko katika maeneo ambayo hatuoni kwamba tuna mali inayoweza ikawaondolea umaskini watu wetu mpaka leo. Niombe sana Serikali iliangalie hili kimkakati na isiliangalie hili kama jambo ambalo liko kwenye bajeti na halifanyiwi kazi yoyote.

Mheshimiwa Spika, niongelee kwa haraka haraka Sekta ya Madini kama muda utaniruhusu. Nimemsikia Profesa Kabudi akiongelea, ukiangalia sekta hii uzalishaji wake umepungua katika bajeti hii kwa kiasi cha asilimia 7.2. Ukweli wa mambo ni kwamba ni kweli tulifanya mambo makubwa, tukabadilisha sheria zetu, lakini baada ya miaka mitatu ni wakati sasa wa kuziangalia hizo sheria kwa makini zaidi kwa sababu tulifanya haya mambo kwa haraka na kulikuwa na sababu za muda kwa nini yalifanyika yaliyofanyika, lakini ukweli ni kwamba wawekezaji walio wengi wakati na wa juu na hata wadogo bado wana matatizo makubwa sana. Sekta hii haikui kwa sababu moja hakuna migodi mipya na migodi ambayo itakuwa mipya inaongelewa pengine itafunguliwa 2025 ambayo utafiti wake ulifanyika zamani. Hakuna utafiti unaofanyika sasa hivi *especially* kwenye maeneo mapya ya *green field*.

Mheshimiwa Spika, vile vile *financing* kwenye Sekta ya Madini imekuwa ni ngumu kutokana na sheria ambazo zipo. Hatusemi hizi sheria zote ni mbaya, tunasema tukae chini tuangalie upya na ikiwezekana watu waziangalie hizi na jicho lingine, kwa sababu hasara mwisho wa siku ni kufanya utafiti ili uweze kuzalisha, ili uweze kuwasaidia wananchi wako kuondoa umaskini. Sasa kama hatuwezi kufanya hivyo, tunashukuru kwamba tuna sheria ambazo ukizalisha tuna uhakika na sisi tutapata kitu fulani kwa maana ya hizo hisa.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye *regulations* mbalimbali za *local content* zinaongelea masuala yote ya *procurement*. Kwenye Serikali tumeanza kuangalia upya *procurement* kwa kiasi gani inazuia au inachelewesha miradi mingi, hata huku kwenye madini

kuna hayo matatizo. Mfumo mzima wa manunuzi unatakiwa uangaliwe upya, ni vizuri kuwa na *local content* lakini tuiangalie isiwe na athari kwenye uzalishaji. Tumepunguza mapato kwenye Sekta ya Madini moja ya sababu ni kwa sababu uzalishaji umepungua. Uzalishaji umepungua kwa sababu kuna *drawbacks* nyingi katika mfumo, kwa hiyo kuna *economics sense*, kuna *legal sense* ya kuweza kuangalia upya. Ukiangalia kwa mfano sheria inayozungumzia *participation* ambayo Profesa ameiongelea, ni sheria inatupa Serikali 16%, ni jambo jema, jambo lenye afya, lakini *wording* ya *section* inayoongelea suala hilo, ukiangalia kwa makini sana ina *ambiguity* na kwa mwekezaji mpya yoyote akiisoma anaangalia kwamba inaweza ikawa *interpreted* kwamba hata ukiomba mkopo na mkopo ule ukiwa unarudishwa au ukiomba *financing* aina yoyote ikiwa inarudishwa, Serikali inatakiwa ipate 16% ya mkopo unaorejeshwa ndiyo sheria ilivyoandikwa na ndiyo ambavyo inaweza ikawa *interpreted*.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa mtu ambaye yuko nchini anaweza akaliangalia aka-*assess risk* akaona ni sawa, lakini kwa mtu ambaye anataka kuja Tanzania, anataka kutafuta fedha awekeze, atakuwa na kigugumizi kikubwa kuendelea kufanya kazi au kuja kukiwa na *ambiguity* kama hiyo.

Mheshimiwa Spika, ameongelea pia *ring fencing,* ni tatizo lingine kubwa, ni kitu kizuri kilifanyika katika Sheria ya Madini lakini kilifanyika katika Sheria ya Kodi ya mwaka 2004. *Ring fencing* ina-*apply* vizuri na ina-*make sense* pale ambapo una uzalishaji, ukiweka *ring fencing* kwenye *exploration* ni kwamba unaua utafiti, hakuna mtu anakuja kufanya utafiti asiweze ku-*recover* gharama

zake. Kwa hiyo ni vizuri tukawa *sober,* tukarudi nyuma kidogo, tukaangalia haya mambo kwa jicho lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Deodatus, nikuombe radhi kwa kukosea jina lako hapo mwanzo, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, atafuatiwa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege ajiandae.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu. Nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu Mheshimiwa Lameck Nchemba, Naibu Waziri na watendaji wote wa katika Wizara na Taasisi ambazo zinaongozwa na Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kuitangaza Tanzania katika ramani ya dunia kiutalii kupitia filamu ya *Royal Tour*. Nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kusisitiza kwa *TRA* na Wizara kuona kwamba wafanyabiashara katika nchi hii hawarudishwi nyuma katika kodi zao zaidi ya mwaka mmoja, lakini vile vile kutokufungiwa kwa akaunti zao. Vile vile nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuondolewa ada ya *form five* na *form six*. Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuona kwamba siku za nyuma hela ambazo hazitumiki ikifikia mwezi Juni zinarudi lakini sasa hivi inaonekana zitaendelea kubakia, lakini vile vile wananchi wale

ambao walikuwa wananyimwa hela kwa kupata hati chafu ambayo ni ukosefu wa watendaji, safari hii wataendelea kupewa, ni kielelezo tosha kwamba kuna utaratibu ambao Mheshimiwa Rais ameufanya kwa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, nitoe ushauri kwa Serikali na niseme kwamba naunga mkono hoja. La kwanza kwenye upande wa *Royal Tour,* Mheshimiwa Rais ameshakamilisha kazi yake, sasa hivi kilichobakia ni jukumu la Wizara ya Utalii, Wizara ya Ardhi, na Wizara ya Miundombinu kuhakikisha kwamba tunakwenda kule katika maeneo mengine ya utalii. Katika kipindi kilichopita utalii ulikuwa zaidi kaskazini, lakini utalii uko Morogoro kupitia Hifadhi ya Udzungwa, Hifadhi ya Mikumi na hifadhi ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambayo ni hifadhi kubwa katika nchi hii. Vile vile utalii uko Katavi kupitia Hifadhi ya Katavi

Mheshimiwa Spika, niombe Mawaziri wenye dhamana waendelee kutangaza hifadhi hizi ili ziendelee kutoa fedha na tija kwenye bajeti ya Serikali na kuleta maendeleo kwa Watanzania. Niipongeze Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi na Wizara ya Fedha kupitia Wizara ya Ujenzi na Mheshimiwa Rais, katika bajeti ya mwaka huu barabara ya Bigwa - Kisaki tumepata kilometa 78 ambayo ndiyo barabara inayokwenda kwenye Hifadhi ya Mwalimu Nyerere tumepata kilometa 78 ambazo zitajengwa kwa kiwango cha lami, lakini tumepata kilometa 11 kutoka Ubena Zomozi kwenda Ngerengere - Mvuha nayo inajengwa kwa kiwango cha lami na barabara hii inakwenda mpaka kwenye Hifadhi ya Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Serikali na kwa kupitia Wizara ya Fedha kwa kuwa tushapitisha fedha hizi ambazo fedha hizi zitakwenda kutengeneza miundombinu ambayo itakuwa rahisi kwa wananchi, lakini vile vile kuwawezesha watalii kufika kwenye Hifadhi ya Mwalimu Nyerere, ambapo ndani ya hifadhi hiyo kuna Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo ni bwawa kubwa katika Afrika, linaweza nalo likawa ni kivutio kikubwa kwa watalii na kuleta fedha nyingi kwa Wizara ya Maliasili na kwenye Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe tu sasa hivi barabara hizo zikatangazwe mara moja tukimaliza bajeti, wakandarasi wakaingie kazini, tupunguze watalii kutembea kiwango kirefu cha kilometa 142 mpaka kwenye geti, maana yake tutakuwa tayari tumesha-*cover* kilometa 78. Niiombe vile vile Serikali, hizi kilometa zilizobakia 64 kutoka Mvua mpaka kwenye lango la geti la Mwalimu Julius Kambarage Nyerere nazo zipangiwe utaratibu wa kupangiwa fedha ili barabara ifike pale, kuwe na urahisi wa kuwafikisha watalii kule. Hifadhi ile vile vile ni mpya na ndani yake kuna mito mikubwa; kuna Mto Kilombero, kuna Mto Ruaha, kuna Mto Rukulunge, ningependa Serikali itenge fedha ili kuweza kujenga madaraja ili hifadhi hiyo iweze kuunganishwa katika maeneo yote na kuweza kuleta tija tunayoitaka.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la kodi, ushauri wangu kwa Serikali, agizo la Mheshimiwa Rais la kusema kwamba *TRA* wasifunge akaunti, *TRA* wasirudishe kodi nyuma, hili kama kiongozi wa nchi ninachoona ni agizo kwa Bunge na ni agizo kwa Wizara husika ya Fedha. Hawa watu wa *TRA* wanaweza kuwa wanagombana na wafanyabiashara, lakini uhalisia wanafunga akaunti

wanarudia nyuma kwa sababu kuna sheria ambazo wanazo ndiyo zinazowapa mamlaka ya kufunga akaunti au kurudia makisio ya wafanyabiashara katika miaka ya nyuma. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Mwigulu kama Waziri lakini sisi kama Bunge, hizo sheria ambazo zinaonekana zinawapa mamlaka hao ziletwe Bungeni tuzijadili…

**SPIKA:** Mheshimiwa Kalogeris weka vizuri hicho kisemeo chako. Ahsante sana.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Spika, nimesema, hizo sheria ambazo ziko zinazowapa mamlaka watu wa TRA kufunga akaunti, lakini vile vile kufanya marejeo ya zaidi ya mwaka mmoja kama matakwa ya Mheshimiwa Rais wetu ambaye anaona kwamba siyo haki, ziletwe Bungeni tuzijadili, tuzifanyie utaratibu na uhalisia ili ziendane na matakwa ya mama na pia ziendane na uhalisia wa watu katika kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, la pili, nimwombe Mheshimiwa Waziri kuna hili suala ambalo nalo ni kikwazo katika kusababisha madeni yawe makubwa kwa walipakodi. Kuna viwango ambavyo vinatengwa kwa Mameneja wa Mikoa kwamba Morogoro tufanye, unatakiwa utoe bilioni 200, je, kuna uhalisia na hawa wafanyabiashara waliokuwa hapo Morogoro? Matokeo yake nini? Meneja wa Mkoa kwa sababu anataka kuendelea kubaki kwenye nafasi ile atakachofanya ni kuendelea kubambikiza kodi ili abaki pale na tunaenda kuumiza watu wetu. Kwa hiyo ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri, hebu waliangalie kwa undani, tunapofanya makisio mwaka huu inawezekana hatukufanya hivyo, lakini mwakani tunapofanya makisio, twende na usahihi wa

wafanyabiashara wetu waliokuwa pale na uwezo wao wa kulipa kodi ili kodi ilipike na naamini dhamira ya Serikali kama mama anavyosema anataka wafanyabiashara walipe kodi na naamini wafanyabiashara wanataka kulipa kodi, ila kinachoonekana kodi inawabana kutokana na sheria ambazo tumezitunga.

Mheshimiwa Spika, kingine, mimi ni mfanyabiashara, kuna suala hili la kodi ya zuio ambalo wanatozwa wafanyabiashara, hakuna mfanyabiashara katika nchi hii naamini ambaye anapata zaidi ya 10% katika mradi anaoufanya. Leo hii mfanyabiashara mfano kwenye kandarasi za barabara, za ujenzi wa maji au ujenzi wa umeme, anapotoa *certificate* anakatwa kodi ya zuio ya 5%, maana yake nini? Kama ana bilioni moja atakatwa milioni 50 zinakaa *TRA*, muda wa kulipa kodi anaambiwa lete hiki, lete hiki, lakini mwisho wa yote anaambiwa kwamba haya unalipa milioni 30, milioni 20 ya zuio inaendelea kubaki kwenye *TRA*. Huku ni kuwarudisha nyuma wafanyabiashara, dhamira ya Serikali ni kujenga uchumi wa nchi, lakini kujenga uchumi wa watu wake vile vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ombi langu kwa Serikali, ikiwezekana tutoe zuio hili la kodi. Sasa hivi kama tulivyokwenda kwenye utaratibu wa kwenye mabasi na kwenye malori tunasema tutalipa milioni mbili, milioni tatu na kwa wafanyabiashara hawa wanaofanya kandarasi na Serikali tukubaliane tu kwamba faida atakayotegemea kuipata ni kati ya 10% na 15%, tufanye 12% tutengeneze utaratibu, huyu mfanyabiashara kila anapokatwa *certificate* katika madai yake ikatwe asilimia ya fedha zake, naamini tutaweza tukafika mahali, kama

huyu mtu alikuwa alipe milioni 30 atalipa milioni 30 yote milioni 20 yake atabakia kujenga uchumi na kujipanua kibiashara ili afanye biashara zaidi, nchi ipate fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, niende sambamba na hii sheria wafanyabiashara wamebambikiziwa kodi kubwa sana wamerudishwa nyuma kwa miaka saba mpaka 10, matokeo yake nini ninavyosema? Sasa hivi wafanyabiashara wana kilio kikubwa nchini, kila mwezi wanaambiwa kodi ambayo imepita nyuma ambayo tayari alikuwa haijui, lakini kodi hiyo vile vile hailipiki, maana yangu nini kusema hailipiki? Huyu mtu anapochelewa kulipa anapigwa na riba, unapigwa riba kwenye kodi ambayo huijui matokeo yake kuna maumivu makubwa kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Serikali mama amesema hataki kodi ya dhuluma, basi hizi kodi ambazo wafanyabiashra wamepigwa za dhuluma zifutwe ili watu wajenge uchumi, waanze kupanga upya, wakafanye kazi za biashara za kusaidia kuleta uchumi katika nchi yetu, au kama Serikali ikishindwa kuzifuta, basi zitoke riba na waambiwe walipe kidogo kidogo kuliko sasa hivi, umefungiwa akaunti, ghafla umeitwa unaambiwa ulipe milioni 20 kama vile fedha hiyo unayo ndani. Hii inaumiza na inafanya uchumi wa nchi wakati mwingine ushindwe kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nizungumzie kwenye suala la *CSR (Community Social Responsibility),* mimi natoka kwenye Halmashauri ya Morogoro Vijijini, kuna Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Mradi ule ndani ya mkataba kuna kipengele cha 4% kupewa wananchi

ambao wako kwenye Halmashauri ya Morogoro Vijijini na Halmashauri ya Rufiji, mpaka dakika hii hakuna. Nimejaribu kuliuliza kwenye *RCC* na hata kwenye ripoti ya *CAG* ilionekana fedha hiyo haijatoka. Kwa hiyo naomba wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up,* atupe *status* ya jambo hili kiserikali, wananchi wa Halmashauri ya Morogoro Vijijini, wananchi wa Halmashauri ya Rufiji wana haki ya kupata fedha hii kwa sababu ni haki yao ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, tuna matatizo ya *ambulance*, tuna matatizo ya barabara, tuna matatizo ya vituo vya afya, tungepata fedha hii kwa sababu katika trilioni saba ya mradi huu halmashauri zinatakiwa zipate bilioni 280, tukigawanya bilioni 140 katika halmashauri, kuna mambo makubwa yatafanyika. Upo uwezekano wasituletee *ambulance* na ikanunuliwa *ambulance* kupitia fedha hizo, wasitujengee vituo vya afya, tukajijengea vituo vya afya kupitia fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimwombe Waziri, tumeliuliza kwenye *RCC* na kuna kipindi hata Mheshimiwa January alipokuja kwenye ukaguzi nilimuuliza, akasema Serikali inalifanyia kazi, tunataka tupate majibu, ni kazi gani ambayo Serikali inaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kufuta ada ya *form five* na *form six.* Ombi langu kwa Serikali kuna kundi kubwa la vijana linabakia, wanaomaliza *form four* ambao wanakwenda kwenye vyuo…

**SPIKA:** Weka kisemeo chako vizuri Mheshimiwa.

Mheshimiwa Spika, kuna kundi kubwa la vijana wanaomaliza *form four* ambao hawaendi *form five* na *form six* wanakwenda kwenye vyuo vya kati na vyuo vya *VETA*. Ombi langu kwa Serikali, kama tumeweza kufuta ada kwa huko, tufute vile vile ada kwenye vyuo vya kati, tufute ada kwenye vyuo vya *VETA*, tupate vijana wengi ambao watakwenda kusomea ufundi na kuja kujiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege na Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, ajiandae.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi uliyonipa. Awali ya yote, nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya maisha ya wazazi wangu. Vile vile nachukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, ndugu jamaa na marafiki, viongozi wa madhehebu ya dini, Baba Askofu Peter Kisenha na Mtume Boniface Mwamposa, kwa maombi na Faraja; pia viongozi wengine wote wa dini kwa namna katika kipindi chote hiki cha msiba ambavyo walinitia moyo na kunifariji. Wazazi wangu; Mama Ceflen Kabula Masaga na baba, Mzee Mpina, Mwenyezi Mungu awapumzishe kwa amani. Amina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimepitia hotuba ya Waziri hapa, nimesoma vitabu vyote viwili vya hali ya uchumi na bajeti yake. Kuna mambo mazuri ambayo ni ya kupongezwa na hii Serikali ya Awamu ya Sita ambayo inaongozwa na

mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Kuna mambo mengi ambayo yamefanyiwa maamuzi lakini mambo mazuri ya kupongezwa ni ule uwezo wa kusimamia fedha yetu ya Kitanzania, kuimarika kwa wastani wa 0.03 kuimarisha kwa uimarikaji chanya, ni jambo zuri sana la kupongezwa kwa Serikali yetu. Pia kuna mipango mizuri pale ambapo tumeweza hata kulipia *advance* ya ndege tano ikiwemo ndogo ya mizigo, ombi ambalo tuliliomba kwa muda mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jambo zuri na la kupongezwa sana katika maamuzi ya Serikali yetu. Pia pongezi kwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba. Hapa ameweka bayana, kuna mambo ambayo hayatajwi na watu wengine, yeye ameamua kuyasema. Katika ripoti yake ameweka wazi juu ya udhaifu wa baadhi ya watendaji wa Serikali ambavyo wanatumia vibaya na kufuja mali za umma. Ametueleza hata namna baadhi ya watendaji wanavyoitumia Sheria ya Manunuzi kupora fedha za umma; ameweka wazi hilo. Pia ameeleza hata baadhi ya mashirika ya umma kugeuzwa kuwa mali ya watu binafsi. Ni maneno ambayo sio Mawaziri wengi wanaoweza kuyataja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wapo Mawaziri wenzake ambao baadhi ya Wabunge walipojaribu kueleza baadhi ya changamoto za Serikali waliambiwa hawaipendi Serikali ya Awamu ya Tano, waliambiwa ni wapotoshaji. Sasa hali hii ya Waziri wa Fedha kusema huu udhaifu ambao ni lazima tuuseme ili tuurekebishe tuweze kupata namna ya kuendelea ni uzalendo na kielelezo cha hali ya juu sana. Hongera sana Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunayo mambo tuliyoyazungumza hapa, nami nataka nianzie na suala la mapato. Suala la mapato hapa, Waziri wa Fedha wewe unajua, watu wamepiga sarakasi hapa, watu wamelia hapa kwenye Bunge, watu wamepiga magoti hapa kwenye Bunge lako Tukufu; hii yote ilikuwa ni hali ngumu ya mahitaji ya fedha kwa wananchi wake. Tuna bajeti ndogo sana ambayo haiwezi kukidhi mahitaji ya wananchi wetu. Sasa tunatokaje hapo? Nimesoma hotuba ya Waziri wa Fedha juu ya namna ya kukusanya mapato inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, sisi sasa hivi tuna *average* ya kukusanya mapato ya Serikali asilimia 11.4 ya pato la Taifa. Wwenzetu wa Rwanda na Kenya wanakusanya hadi asilimia 16 ya pato ya Taifa. Nini kinachotukwaza kufikia hapo?

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengi hapa. Kwa mfano, suala la malimbikizo ya madeni. Ni jambo la ajabu na la kusikitisha, tumefikia hatua malimbikizo ya madeni, zile *arrears* kufikia Shilingi trilioni 7.54 kwa mwaka wa fedha. Unawezaje kuwa na *arrears* za Shilingi trilioni 7.54 halafu ukaweza kukusanya mapato ya kutosha ku-*support* bajeti yako?

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tuna kesi zilizoshikiliwa na mamlaka ya rufani trilioni 5.19, nazo hizi ni kesi ambazo zinatakiwa kuamuliwa tu, lakini haziamuliwi, matokeo yake mapato haya ya Serikali hayawezi kukusanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulisema mwaka jana na sasa tunaendelea kusema kwamba tuna makampuni ya 504

*(multinational companies)* ambazo *assessment* yake ya kodi ni lazima uwe na wataalam ambao wanaweza ku-*assess properly* ili uweze kukusanya kodi *properly*. Uwezo wetu sasa hivi ni asilimia 1.2 wa kuya-*asses* haya makampuni. Maana yake ni kwamba hayawezi kulipa kodi *properly*. Sasa ni lini utakusanya mapato ya kuwatosheleza wananchi wako?

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kama una mapato ambayo hayajakusanywa kwa maana ya *arrears,* kwa maana ya kushikiliwa na mamlaka za rufani, ni Shilingi trilioni 12.6 hazijakusanywa. Fedha hii zingeweza kutusaidia kupiga hatua kubwa sana, lakini hayo yote hayajafanyika. Sasa Waziri wa Fedha ni vizuri akajipanga vizuri zaidi katika kushughulikia hili suala.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kidogo kuhusu marekebisho ya sheria na ni zungumzie eneo la Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ambapo 5% zinapendekezwa kwenda kujenga miundombinu ya masoko ya wamachinga. Hapa suala langu ni moja. Hizi fedha zilikuwa zinakopwa kwa ajili ya mitaji. Asilimia 10 yote hii ilikuwa inakwenda kwenye mitaji; na hawa wamachinga walikuwa wanakopa kwenye hizo asilimia 10, unaenda kuzipunguza fedha za mtaji kuzipeleka kujenga miundombinu, halafu miundombinu unayokwenda kujenga unasema tu asilimia tano. Unajua Meatu kuna machinga wangapi? Unajua wanahitaji soko lenye ukubwa gani? Unajua *nature* ya biashara wanazozifanya? Unaidhinisha tu asilimia tano ziende huko, nadhani hii siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtaji tungeuacha, asilimia 10 ziende kwenye mtaji. Kama tunahitaji kujenga

miundombinu ya Wamachinga na masoko tutafute vyanzo vingine vya fedha tukajenge na tufanye tathmini ya uhakika tunaenda kujenga eneo lenye ukubwa wa aina gani? Pia tuzifahamu biashara. Muuza soksi huyu anayetaka kutembea kuwapelekea wateja wake unamjengea jengo! Ni lazima pia tujue watu tunaowajengea *nature* yao tujue tunawajengea miundombinu ya aina gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni deni la Taifa. Deni la Taifa hapa limeelezwa katika hotuba ya Waziri wa Fedha, limeongezeka kwa Shilingi trilioni 8.72, unajiuliza maswali, deni la Serikali linaongezekaje? Limeongezeka kwa Shilingi trilioni 8.72. Kama deni la Serikali limeongezeka kwa Shilingi trilioni 8.72 katika mwaka mmoja wa fedha, wakati katika mwaka husika deni hilo tulili-*service* kwa zaidi ya Shilingi trilioni 7.2? Kama ndiyo hivyo, maana yake tumekopa kuliko tulivyoahidi hapa Bungeni. Maana yake tumekopa mkopo mkubwa wa zaidi ya kile tulichoji-*commit* hapa Bungeni. Kama tulifanya hivyo, ni kwa ridhaa ya nani? Kwa ajili ya kazi gani?

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakapokuja hapa atueleze vizuri katika hili suala la Deni la Serikali ili kuondoa mkanganyiko uliopo. Kwa sababu ukifanya hesabu za kawaida, tumekopa zaidi ya Shilingi trilioni 15, wakati huku tunaelezwa kwamba tumekopa kama Shilingi trilioni 9.3. Sasa huu mkanganyiko wa takwimu unatokana na nini? Ni lazima Waziri wa Fedha aeleze vizuri juu ya jambo hili ili kuujua usahihi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni ranchi ya Kongwa kugeuzwa kuwa shamba la alizeti. Hili shamba lilianzishwa

kwa ajili ya ranchi za mifugo, kuendeleza kosafu bora ya mifugo, kuendeleza mifugo, na kama shamba darasa la mifugo. Leo tunaenda kulibadilisha eti kuwa shamba la alizeti kwa sababu mifugo humo ni michache. Anayesema hayo ni Waziri wa Fedha. Kama mifugo ni michache, si upeleke fedha ukaongeze tu mifugo mle? Kuna tatizo gani? Kama mifugo ni michache katika ranchi ya Kongwa, kwa nini usiongeze mifugo humo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna miundombinu ya maji mle, tuna miundombinu ya majosho, tuna miundombinu ya malisho, tunaenda kuibomoa tugeuze kuwa shamba! Kwani hakuna mashamba mengine yaliyo wazi alizeti ikaenda kulimwa katika nchi hii? Mbona tunaelezwa mapori kwa mapori! Hii yote ni kutokuona umuhimu wa mifugo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huku tunasema tunaongeza fedha kwenye mifugo, huku unaenda kunyang'anya mashamba ya wafugaji kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha alizeti. Mbona hamjaenda Tabora; mashamba ya mifugo yapo mengi ambayo hayajalimwa, ni mapori, kwa nini msiende mkafyeke mapori huko mpande alizeti? Kwa nini mkapande alizeti kwenye shamba la mifugo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Wabunge kataeni mpango huu na msikubali mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni hili la sheria. Waziri wa Fedha anapendekeza kupewa mamlaka ya kutoa vivutio vya ziada vinavyotokana na vikao vya *NISK,* anaweza kusamehe *VAT,* anaweza kusamehe kodi ya mapato kwa ajili ya wawekezaji mahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tujue tuna ushindani sawa katika biashara *(fair competition)*. Kuna watu walioweka viwanda hapa. Leo unasema tu, huyu ni mahiri anakuja, tunamsamehe; hawa waliowekeza mapema unawapeleka wapi? Tuna hiyo *fair competition* ambayo ni *global issue* ambayo ni lazima ui-*tackle globally!* Unakuja huyu una m-*exempt* kwa makundi ya watu. Tunapotaka ku-*exempt* ni lazima tuwe na ile *exemption* ya pamoja. Kwamba hili kundi lote tumelisamehe, lakini hizi *exemption* za mtu mmoja mmoja hazitufikishi mahali popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami naomba sana, Waziri wa Fedha sio leo atakuwa Waziri wa Fedha wa kudumu, watakuja Mawaziri wa Fedha wengine; tusikubali na Waziri wa Fedha asikubali kuingizwa kwenye mitego ya kutoa *exemption* ya *group* la watu. Asikubali! Nasi Wabunge tusikubali kuruhusu sheria ya namna hiyo ikaingia hapa Bungeni ya kumruhusu Waziri wa Fedha hapa eti hawa ni mahiri tunawasamehe, wakati tuna wawekezaji wengine wana viwanda hapa nchini, wasiposhindana kwa haki si watafunga viwanda kwa ajili ya huyo uliyem-*favour* wewe! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukatae sheria hizo na tuzikatae hapa Bungeni, Kwa kweli *Finance Bill* itakapokuja, tuta-*move amendment* kuhakikisha kwamba sheria za namna hii hazipati nafasi kwenda kuharibu uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa kabisa, sikuwepo, lakini nimefuatilia sana katika *Hansard* mjadala wa Bunge baada ya kumaliza msiba. Naomba tu kusema kwa kifupi

kwamba, kuna maeneo muhimu sana ambayo ni lazima tu twende kwenye kuunda Tume ya Bunge. Nami nakuomba ukubali uweke hii rekodi, utashukuru. Utakapounda Tume ya Bunge, utakayoenda kuyaona na mchango utakaoleta kwenye Taifa, utanishukuru kama mmoja wa Wabunge wako waliokushauri hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, moja ya jambo ambalo naomba liundiwe tume ni ucheleweshaji wa ukamilishaji wa mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. La pili ninaloomba liundiwe tume ni kupanda kwa bei za mafuta kwa kisingizio cha vita ya Ukraine na Russia; na tuweze kujua yale makandokando mengine yaliyomo humo ndani ambapo mchezo uliofanywa wa bei za mafuta kupanda nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka liundiwe tume ni bei za mbolea nchini na biashara inavyofanywa. Tulikuwa tunafanya vizuri sana zamani, tulikuwa na mpango wa kufanya *requalification,* tulikuwa tuna-*visit* hata viwanda vinavyozalisha mbolea. Tulikuwa tunatumia mfumo wetu ule wa *bulk procurement system* tukawezesha mbolea kuagizwa kwa bei ndogo na kusambazwa kwa bei ndogo. Mfumo huo umeuawa. Sasa leo hii tukajue kwamba hizi bei za mbolea tunazopewa hapa nchini, kweli zina uhalisia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili suala la mbolea nataka liundiwe tume kwa sababu moja, hata Waziri wa Kilimo mwenyewe alivyoingia hapa Bungeni, mchana akatoka na takwimu nyingine, kwenye kuhitimisha akatoka na takwimu nyingine. Kwa hiyo, tutakuja tuone ukweli na uhalisia wa mbolea wanazouziwa wananchi imekaa vipi hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nataka tukaangalie suala la malimbikizo haya ya kodi, hivi ni kweli taasisi zetu za kodi wanafikia mpaka malimbikizo ya Shilingi trilioni 7.54 za kodi, mnashindwa kukusanya, halafu uwezo wa kukusanya hizo kodi ukawa asilimia 10 tu, halafu tunakaa kimya katika hilo! Hili jambo ni kuhusu malimbikizo ya kodi na mapingamizi yaliyopo kwenye Mahakama ni muhimu sana yaundiwe tume sasa, kwa sababu Serikali kila tukiiambia haitekelezi hilo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, atafuatiwa na Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, ajiandae.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie katika hotuba ya Serikali. Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kunijaalia uhai kuweza kusimama hapa leo.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa bajeti nzuri ambayo hakika inaenda kutibu kiu ya Watanzania. Pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, wamekuwa wasikivu kweli kweli, nasi ambao tumepata nafasi ya kuwasikiliza kwenye Kamati ya Bajeti, hakika wamekuwa waki-*accommodate* mawazo ambayo yanatolewa na Wajumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kipekee kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo ameitendea haki sekta ya utalii. Utakubaliana kwamba *Royal Tour* duniani zimefanyika katika maeneo machache na Tanzania ikiwa mojawapo. Inahitaji ujasiri kwa Mheshimiwa Rais kushiriki. Kimataifa nchi ambazo zimeweza kufanyiwa na huyu Bwana Peter Greeberg ni pamoja na Israel, New Zealand, na kwa Afrika ni Rwanda na Tanzania. Kwa hiyo, hizi kelele ambazo unazisikia nyingine zinaanzia ndani na nyingine zinatoka nje ni kwa sababu ya mafanikio ambayo tunaenda kuyapata kutokana na utangazaji ambao umefanyika. Tuna kila sababu ya kumuunga mkono Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni wajibu sasa kwa Wizara; Mheshimiwa Rais ameonesha njia, tunayo maeneo mengi sana ya vivutio ndani ya nchi yetu, tuna vivutio vilivyozoeleka na sasa ni *high time* twende na maeneo mengine, twende Mbeya, Songwe, na Rukwa, vipo vivutio vingi, ili watalii kama ambavyo wamekuwa wakienda nchi kama Israeli, waweze kuja Tanzania. Itakuwa siyo rahisi kumwomba tena Mheshimiwa Rais ashiriki *Royal Tour* nyingine; ameonesha njia, ni kazi ya Wizara husika kuhakikisha kwamba kazi nzuri ambayo imeanzishwa na Mheshimiwa Rais inaenda kuleta mafanikio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema bajeti hii ni ya kimapinduzi, maana imepeleka fedha kwenye kilimo, kutoka shilingi bilioni 294 mpaka shilingi bilioni 954. Tumekuwa tukisema Bunge la Kumi na Mbili linatakiwa liache *legacy* yake ya kuhakikisha kwamba *transformation* inafanyika kwenye kilimo ambapo kwenye kilimo huku ndiko tunaajiri Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania wanashiriki kwenye shughuli za kilimo, lakini kilimo kimekuwa kama vile mtu ambaye anakosa kazi ya maana ndiyo anaambiwa aende kwenye kilimo, lakini kwa uwekezaji wa fedha hizi na ambavyo tumeambiwa na Serikali kwamba bajeti itaendelea kukua hadi kufikia asilimia 10, hakika kilimo kitakuwa kivutio na Watanzania wengi wataona namna pekee ya kuwa na uhakika wa kiuchumi ni kujiingiza kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, ni wakati muafaka wa kuhakikisha kwamba benki ya Kilimo inafufuliwa, inawezeshwa kimtaji ili Mtanzania ambaye anaenda kukopa kwa ajili ya kilimo waongee lugha ya kuelewana. Tukiongea *digit* moja katika *interest* iwe ni jambo linaeleweka kiurahisi, ukitaka kilimo kikakopewe kwenye *Commercial Bank,* hakika hatuwezi kufika.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kushirikiana na Waziri wa Kilimo, ni muda muafaka kama siyo bajeti hii, katika bajeti zinazokuja tuhakikishe kwamba benki ya kilimo inawezeshwa kimtaji na pia kuwa na *manpower* na *structure* ya kutosha ambayo itahakikisha kwamba siyo lazima mwananchi atoke Kalambo aje hadi Dar es Salaam au Mbeya ndiyo aweze kusikilizwa kwa ajili ya masuala ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, naiomba Serikali yangu, tuna wajibu wa kufufua benki ya kilimo, lakini benki yetu ya *TIB,* hapa katikati imeunganishwa na Benki ya Posta, ni vizuri kama Serikali tukawa na benki yetu ambayo tuna uhakika kama ambavyo benki nyingine katika nchi kama za China, kuna benki ya Serikali ambayo muda wote Serikali inaweza ikaiwezesha na

wakati mwingine inakwenda yenyewe kukopa. Ni wakati muafaka kuhakikisha kwamba Benki ya *TIB* pamoja na Benki ya Posta, kwa jina lolote lile ambalo mtakuja nalo, kuhakikishe kwamba inawezeshwa kimtaji na kimuundo ili Watanzania au Wakandarasi wadogo wadogo wawe na uhakika kwamba wanaenda kukopa na kufanya miradi kwa ajili ya Taifa leo.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niongelee suala la *TRA*. Naomba niipongeze *TRA,* imekuwa ikifanya vizuri mwaka hadi mwaka, wamekuwa wakiongeza makusanyo katika mapato yao; lakini itoshe, ifike wakati kwamba ni vizuri kama Taifa tuhakikishe kwamba tunawekeza kwenye mifumo.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuwapongea vijana wa Kitanzania ambao wamekuwa wakiibua mifumo mizuri ya Kimataifa. Ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba vijana hao wa Kitanzania ambao wanaibua mifumo na inakubalika Kimataifa, wanalindwa na wanakuwa *motivated,* kwa sababu anayefanya vizuri, hakuna dhambi ya kuhakikisha kwamba unampa *incentive*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haipendezi wanafanya kazi nzuri lakini huoni namna ambavyo Serikali inawapa motisha ili waendelee kuwa Serikalini na badala yake baada ya muda mfupi, wanaondoka kwenda kwenye *private* sekta, kwa hiyo, inakuwa kila wakati Serikali inakuwa na kazi ya ku-*train* wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niiombe *TRA, top management system* ambayo imekuwa ikifanyika katika kukusanya kodi imeonesha ufanisi mkubwa, hasa maeneo ya Majiji,

bahati nzuri mmepata watumishi kama 2,000, hakikisheni kwanza mnaanza kuwatumia hao katika maeneo ambayo ni oevu kwa maana ya uhakika wa fedha kwenda huko tuhakikishe kwamba tunapata mapato mengi kabla ya kuanza kuwatawanya. Ikiwezekana hebu tuanze na hili eneo ambalo linaonekana kwamba halijafanya vizuri, katika *property tax,* kwa kushirikiana na TAMISEMI huku kuna fedha za kutosha. Tuondokane na ule utaratibu wa *flat rate,* kwamba mwenye ghorofa na nyumba ya kawaida eti wanachangia kiasi sawa, hii siyo sawa hata kidogo. Ni kukiuka sheria za kodi, kodi inataka uwe *progressive* na yule ambaye ana kingi achangie kingi, aliyekuwa na kidogo achangie kidogo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo naomba niongolee, nilikuwa naongea na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, nalirudia kwa mara nyingine. Namna pekee ya sisi kama Taifa la Tanzania kuweza ku-*access Congo DRC,* ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na njia iliyokuwa fupi kuliko njia zote. Na ikiwezekana twende Congo tukitoka Tanzania bila kulazimika kupita nchi nyingine na *route* nilishawapa.

Mheshimiwa Spika, upo uwekezaji ambao umefanywa na Serikali unakwenda mpaka Kasanga *Port* na pale kuna maboresho makubwa sana ya Bandari. Ukivuka *straight* bila kugusa nchi nyingine yoyote unakwenda eneo la Mlilo ambalo tayari utafiti ulishafanyika, panafaa kuwa na bandari.

Mheshimiwa Spika, siyo lazima kwamba Serikali ndiyo iende kuwekeza, ni *private sector* kwa sababu malori yakipita nchi nyingine yanaacha Dola 700 kwa kila lori moja. Kwa hiyo, hata kama tukawa na *straight* njia na

wakawa wanalipishwa hata Dola 400 wataona ni nafuu kwa sababu kwanza wamepunguza umbali, lakini wakati huohuo tuna-*access* Congo ya Lubumbashi ambayo ndiyo iliyokuwa na madini.

Mheshimiwa Spika, narudia kwa mara nyingine, Mheshimiwa Waziri, ulisema ni-*share* na wewe *documents,* nita-*share* na wewe ili muone kama Serikali, kwa kushirikiana na Serikali ya Congo tunakwendaje Congo ya Katanga kwa maana ya Katanga Province na kule kwingine ili kama tunajenga reli kwenda upande wa chini kule sawa, lakini Congo ya Lubumbashi namna pekee ya kufikia huko ni kwa kupitia Katanga na jiografia haiongopi. Kwa hiyo ni vizuri tusije tukashindwa kwenda na jiografia inavyotutaka.

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine ambalo limeibuka kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri na ikaleta kelele kweli. Inaonekana kwamba sasa hivi kodi eti mtu kuanzia umri wa miaka 18 inabidi apate *TIN Number* kwa sababu inabidi aanze kuchangia kodi, jambo ambalo siyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, hakuna kodi yoyote duniani ambayo ilishawahi kutozwa kwa ku-*base* kwenye umri wa mtu. Kinachotozwa ni fedha. Kwa hiyo ni vizuri Serikali mkafafanua vizuri, kwamba hata angekuwa mtoto mdogo amerithi kampuni ambayo ina *wealth,* anatozwa kodi. Kwa hiyo kinachotozwa kodi siyo umri wa mtu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kumekuwa na *misconception* kwamba umri wa miaka 18 watu wawe na *TIN* ni kwa sababu ya takwa la kisheria tulilonalo sasa hivi kwamba kitambulisho cha *NIDA* anapewa mtu mwenye

umri kuanzia miaka 18. Kwa hiyo, upotoshaji ambao umekuwepo kwamba eti sasa Watanzania *whether* ana kazi, ana kipato au hana kipato akishafika umri wa miaka 18 anaanza kutozwa kodi siyo sahihi. Kinachotakiwa ni kwamba anayetozwa ni yule ambaye ana kipato, kinachotozwa ni kipato na siyo umri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba niunge mkono hoja, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas ajiandae.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na wewe nikushukuru sana kwa kunipa fursa ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu leo kwa ajili ya kuweka mchango wangu kwenye Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, leo nimepanga kuzungumzia mambo matatu. Jambo la kwanza ni kuhusiana na hili ambalo limewasilishwa kupitia bajeti hii kwa maana ya kupunguza gharama za uendeshai Serikalini. Kupitia fursa hii naomba nimpongeze sana Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa maono, namna ambavyo bajeti hii imeletwa na kukidhi mahitaji ya maeneo mengi, hasa kwa watu wale wenye kipato kidogo kwa maana ya wenzetu kule chini.

Mheshimiwa Spika, ukizungumzia kupunguza gharama za uendeshaji maana yake unataka kuleta tija katika wale ambao wanategemea huduma za kijamii

zinazotolewa na Serikali huko kwenye ngazi za chini. Nimeona katika bajeti hii, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, amekuja na mkakati wa kupunguza matumizi Serikalini kwenye magari, kwa watumishi, vilevile jambo kubwa ambalo nimeliona ni lile la kupunguza vikao na kuhamia kwenye TEHAMA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhamia kwenye TEHAMA kwa ulimwengu tulio nao sasa ni kama vile tumechelewa, ni jambo ambalo ningeshauri liende kwa spidi kubwa sana. Nitakupa mfano, wakati wa maandalizi ya bajeti zetu za halmashauri, halmashauri zetu *almost* zote huwa zinahamia Dodoma.

Mheshimiwa Spika, wanakaa kwa zaidi ya wiki tatu, wiki tano na wengine miezi miwili, hapa Dodoma kwa ajili ya maandalizi ya bajeti, jambo ambalo lingeweza kufanyika huko kwenye Halmashauri zao taarifa zikaletwa kwenye Kamati za Bunge, michakato ikaenda kimtandao kutumia TEHAMA na mwisho wa siku tukatengeneza tija kubwa sana na tukabana matumizi, fedha hizi tukapeleka kwenye maeneo mengine ambayo yana uhitaji. Kwa hiyo, ninaipongeze sana Serikali na Wizara ya Fedha kwa kuona namna gani tunaweza tukabana matumizi kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Spika, kipindi kifupi kilichopita tuliona Katibu Mkuu Hazina alitoa tangazo la kuongeza hizi posho za viongozi. Hizi ukiziongeza na bado ukaendelea ku-*entertain* vikao vingi, tunapeleka mzigo mkubwa sana kwa Mtanzania. Ili kuweza kupunguza huu mzigo, pamoja na kwamba hizi posho zimeongezwa, ni vizuri sana Mheshimiwa Waziri akaona namna nzuri ya kutekeleza hili jambo kwa haraka kuleta tija na nafuu ya maisha ili

kuendeleza kupeleka fedha kwenye miradi ya maendeleo na kuboresha maisha ya Watanzania zaidi.

Mheshimiwa Spika, eneo hili naona changamoto moja tu, kwamba tumezoea kutumia mtandao wetu kwenye mawasiliano ya Serikali, hata kwenye mifumo ya fedha tunatumia *TTCL,* lakini *TTCL* haifanyi vizuri sana, maeneo mengine hayana mtandao kabisa, maeneo mengine mtandao ni hafifu, jambo ambalo litatusababishia sasa kusuasua tunapokwenda kutekeleza vikao kwa kutumia TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ili tuende kwa ufanisi, jambo la kwanza ningeishauri Serikali kuangalia namna bora ya kuboresha mfumo wa mawasiliano kupitia *TTCL.* Wakiboresha mtandao wa *TTCL* ukawa unapatikana, bado itakuwa tena ni fursa, badala ya fedha kutumika kwenye mitandao mingine ya kibiashara, hiyohiyo fedha ambayo tunakwenda kufanyia TEHAMA itarudi tena kwenye Mfuko wa Serikali kupitia *TTCL. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninapenda kulizungumza siku ya leo ni namna ya kuongeza mapato. Wakati inawasilishwa Bajeti ya Afya nilisimama katika Bunge lako na nikaiomba sana Serikali kuangalia namna ya kuboresha huduma ya mama na mtoto.

Mheshimiwa Spika, katika kuzungumza hayo tuliona mifano mbalimbali, kwamba pamoja na sera nzuri za Serikali na maelekezo ya Wizara kwamba akina mama na watoto wapate matibabu bure, lakini maeneo mengi akina mama wanafanyiwa operesheni kwa gharama kubwa sana wanapojifungua, watoto bado wanatozwa,

ukiuliza wanasema ni uwezo mdogo wa kifedga lakini muda mwingine vituo vyetu vinakosa kabisa dawa.

Mheshimiwa Spika, namna bora ambayo nimeiona ya kwenda kuongeza mapato kwenye vituo vyetu vya kutolea huduma za afya ni kufunga mfumo wa *GoT-HoMIS*. *GoT-HoMIS* ni mfumo ambao unaunganisha utoaji wa huduma kwenye kituo cha afya tangu mgonjwa anasajiliwa mpaka anakwenda kwa daktari, anakwenda maabara, mpaka anarudi tena kwa daktari kwa ajili ya majibu. Kwa hiyo, huo mfumo ukiwekwa vizuri maana yake hakutakuwa na uvujaji wa mapato kwenye kituo cha afya.

Mheshimiwa Spika, tumeona kwenye maeneo mengi ambapo huo mfumo umefungwa mapato yameongezeka zaidi ya mara tano, mara sita. Kituo ambacho kilikuwa kinakusanya 100,000 kwa siku kikifungiwa *GoT-HoMIS* kinakusanya mpaka 500,000, 600,000 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, jambo hili likiwekewa mkazo, pamoja na maelekezo ya Serikali, lakini bado Halmashauri hazijatekeleza vizuri huu mfumo, yakipelekwa maelekezo mahususi wakafunga huu mfumo, ninaamini hata yale malalamiko ya kukosekana kwa dawa au kutozwa fedha kwenye vituo vya afya yataondoka kwa sababu tayari kutakuwa na uwezo wa kupata fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninataka kulizungumza siku ya leo ni hii asilimia 10. Naifahamu dhamira njema sana ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, kwamba angetamani kuwawezesha na

wamachinga, na mimi najua. Kwenye asilimia 10 ya halmashauri imewataja akina mama, vijana na watu wenye ulemavu, kwenye kundi la vijana wametajwa wenye kuanzia miaka 18 mpaka miaka 35 wakati Baba kwa maana ya mwanaume ambaye anatamani kupata huo mkopo wa halmashauri wa asilimia 10 lakini hawezi kuupata kwa sababu tayari pengine amevuka miaka 35. Changamoto inakuja hapa, Baba mwenye miaka 35 akikosa huo mkopo nadhani inawezekana ndiyo sababu Serikali imefikiria sasa waone namna ya kutengeneza miundombinu kwa ajili ya wamachinga na watu wa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambie, chanzo cha mikopo hii ya wanawake na vijana ilianzishwa mwaka 1993 na Kanuni zake nadhani zilianza mwaka 1994, lakini maboresho yaliyofanyika 2018 na kanuni za 2019 yalitoa malengo kwamba kwa mwanamke siyo mtu ambaye ana msuli, baba kwenye familia au kijana mwenye nguvu angalau hawezi kufa njaa kwa sababu ana uwezo wa kwenda kubeba gunia, ana uwezo wa kwenda kuchimba sehemu kazi yoyote ya kutumia msuli na akawezesha familia yake kupata mlo wa siku hiyo. Lakini kwa mama uwezo huo hana.

Mheshimiwa Spika, sasa ili aweze kujikimu, aweze kuendeleza familia, mama ambaye anategemewa na familia, ilionekana ni vyema apewe mkopo ndiyo tukaenda kutenga hizo asilimia 10 tukazigawanya zilivyogawanywa kwa ajili ya kuwezesha yale makundi maalum.

Mheshimiwa Spika, sasa changamoto inayokuja hapa ni kwamba hii fedha haitoshi, kuna halmashauri za

pembeni, kwa mfano Halmashauri za Wilaya za Lushoto, Kilindi, Korogwe, Mkinga na kadhalika na pengine nchini halmashauri nyingi ambazo pengine kwa mwaka hata zinakusanya chini ya Bilioni Moja. Sasa kama mapato ya ndani yako chini ya Bilioni Moja, maana yake ni kwamba asilimia 10 inaweza isifike hata Milioni 200 lakini wananchi wanaohitaji pale ni zaidi ya inavyotegemewa, kwa hiyo mwisho wa siku wanazigawanya zile fedha kwa kuwakopesha wengine Milioni Moja, Milioni Mbili, hela ambayo haileti tija au tija yake inachelewa sana kwa sababu mkopo huo unakuwa na fedha kidogo.

Mheshimiwa Spika, sasa nini kifanyike? Kwa kuwa mwaka 1993 lengo lilikuwa ni vijana na akina mama, na kwa sababu mwaka 1993 ulianzishwa mfuko wa vijana na unafanya kazi mpaka leo kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, ninashauri kwamba pamoja na asilimia 10 kubaki kama ilivyo kwenye Halmashauri zetu kwa ajili ya kuwasaidia akina mama, vijana na watu wenye ulemavu, lakini uanzishwe Mfuko mwingine na uwe unatengewa fedha kama unavyotengewa huu wa vijana kwa kila bajeti kwa ajili ya kuwasaidia hawa wamachinga kujenga miundombinu, vilevile mfuko huo uwasaidie akina mama kupata mikopo kama ambavyo wanapata hili kundi la vijana, kwa sababu wanapata ile asilimia 10 ya halmashauri, *at the same time* wanapata mikopo kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninapenda kulizungumza siku ya leo ni upande wa watumishi. Ni dhahiri kwamba tuna upungufu mkubwa wa watumishi katika sekta mbalimbali, Wizara imeona na imeleta namna ambavyo wanaweza wakakabiliana na namna ambavyo wanaweza wakaajiri kadri muda

unavyokwenda *gradually*. Mimi naona kuna haja ya kufanya kitu kwenye eneo hili. Kwa mfano, unakuta kwenye Halmashauri ya Wilaya tunazo taasisi zetu kama Halmashauri, kuna *RUWASA, TARURA,* kuna taasisi nyingi zipo kwenye Halmashauri, unaweza kukuta pengine kuna Mhandisi wa Ujenzi mmoja yupo pale Halmashauri pengine upande wa *RUWASA,* ni vizuri tukaenda kwenye kanuni zetu za utumishi wa umma tukaangalia namna ya kuwaazima watumishi kwenye taasisi zingine waende wafanye kazi kwenye taasisi mojawapo ili kuweza angalau kupunguza upungufu wa watumishi na mwisho wa siku kuleta tija katika utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, vilevile inaenda pamoja na upande wa Madaktari. Tumezoea kuona Madaktari wengi wameajiriwa kwenye hospitali zetu za Serikali, wakimaliza ule muda waliopangiwa kuwepo pale unamkuta yuko *part-time* kwenye hospitali binafsi, lakini huwezi kumkuta yuko *part-time* kwenye hospitali nyingine ya Serikali. Kwa nini, pengine kuna mgongano hapo wa kikanuni na kimaadili kwenye Kanuni za Utumishi wa Umma, kwa hiyo tuki-*harmonize* haya mazingira ya utumishi wa umma tutawaruhusu watumishi wetu kutumika kwenye taasisi au kwenye maeneo zaidi ya moja na mwisho wa siku kupunguza uhaba katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, nimeliona hili kwa upande wa *TRA* pia. Kwa mfano, unakuta kwenye maduka yetu anakwenda kutembelea mtu wa *TRA* kwa ajili ya kukagua kama kuna *EFD machine* inatumika vizuri, lakini kama huyo mwenye duka analipa kodi vizuri, akitoka anakwenda mtu wa mapato wa Halmshauri, anachokwenda kufanya yeye ni kuangalia *service levy*

peke yake, akitoka atakwenda Afisa Biashara, anachokwenda kufanya ni kuangalia leseni peke yake, akitoka ataenda mtu wa Zimamoto anakwenda kukagua mtungi peke yake, sasa badala yake yangeunganishwa haya yote akienda mmoja wao akapewa nafasi ya kukagua hayo mengine yote kuliko kulazimu kila ofisi, kila idara, kila taasisi kutembelea duka moja. Hii naona kama vile ni matumizi mabaya ya ofisi na kushindwa kutumia watumishi wachache tulionao, ku-*utilize resources* tulizonazo katika kuleta tija kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninapenda kuzungumzia, hapohapo kwenye utumishi wa umma, tuna idara kwenye elimu inaitwa *Quality Insurance* (Wathibiti Ubora wa Shule). Kwa mujibu wa Waraka wa 2015 hawa ni watumishi viongozi na waraka umewaelekeza kwamba wao watalipwa mishahara yao kwa *LSSE* II lakini….

Mheshimiwa Spika, naomba sekunde mbili tu niweze kuhitimisha.

**SPIKA:** Endelea.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, mpaka tunapozungumza sasa wao hawajapelekwa kwenye hiyo ngazi mpya ya mshahara. Ninaiomba Serikali ione namna ya kuwatia moyo watu hawa. Kwa sababu Waraka umetoka tangu 2015, ni nini kinazuia hawa watu wasipelekwe kwenye mishahara mipya kwa miaka Sita ya kubaki kwenye mishahara ya zamani?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mheshimiwa Hawa Mwaifunga ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii kuchangia kwenye bajeti.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuleta bajeti nzuri sana, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mwigulu, kwa kuileta hii bajeti hapa Bungeni. Kusema ukweli hii bajeti imekidhi ni nzuri sana kwa wananchi wote, wote wanaipenda sana.

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la kuondolewa ada kwa kidato cha tano na sita. Hii imepokelewa vizuri na inaonekana kuwa wanafunzi watasoma bure bila ya kulipa ada kuanzia shule za msingi mpaka Kidato cha Sita, hii ni nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, inaonekana kuwa mikopo ya Vyuo Vikuu imeongezewa fedha katika bajeti hii. Kwa hiyo, jambo ninaloomba na kushauri ni kwamba vyuo vya kati viangaliwe ili na vyenyewe ulipaji wa ada uweze kuwa nafuu kwa wanafunzi hawa na kwa wazazi. Kwa hiyo, huo ni ushauri wangu, kuwa na vyenyewe viangaliwe, visiachwe katikati peke yao.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo ninapenda kuongelea ni kuhusu hii asilimia 10. Kwa kweli hii asilimia 10 Mheshimiwa Waziri ukija kuhitimisha naomba uitolee ufafanuzi ili tuweze kuelewa. Hii asilimia 10 umesema

kwenye hotuba yako kwamba asilimia tano imependekezwa kuwa iende kwa wamachinga ili kuboresha miundombinu. Miundombinu hiyo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa masoko.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Wamachinga tayari kuna fedha ambazo zimeshatengwa, lakini hii asilimia 10 umesema asilimia mbili ndiyo itakwenda kwa vijana na asilimia moja ndiyo itakwenda kwa watu wenye ulemavu kwa kweli hapo haieleweki!

Mheshimiwa Spika, ninachoomba hii asilimia 10 ibaki kama ilivyokuwa, kuwa asilimia nne ibaki kwa akinamama, asilimia nne ibaki kwa vijana na asilimia mbili ibaki pia kwa wale watu wenye ulemavu. Kwanza kilichokuwa kinaombwa hapa ni kuongeza hii bajeti kwa upande huu wa asilimia 4:4:2, sasa badala ya kuongeza inaonekana kuwa inapunguzwa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri aingalie vizuri sana kusudi isipangwe kama anavyokusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la kufurahisha kwa wananchi wote na hasa wakulima na wafugaji na wavuvi ni kujali sekta za uzalishaji na hizi sekta za uzalishaji hasa ni Sekta ya Kilimo, Sekta ya Uvuvi na Sekta ya Mifugo ambapo asilimia 65.5 ya wananchi inategemea kilimo. Asilimia 100 ya chakula tunachokula Watanzania inategemea kilimo. Kwa hiyo, kwa kuongeza bajeti ya kilimo kutoka bilioni 274 mpaka bilioni 954, ni jambo la neema sana. Pia fedha za mifugo kutoka bilioni 168.2 mpaka 268.2, nalo ni jambo safi kabisa na hapo hapo kuna mchanganuo kuwa bilioni 92 ni fedha za mifugo na bilioni 176.2 ni fedha za uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye kilimo jambo linalotakiwa hapa ni kilimo chenye tija, ufugaji wa tija pamoja na uvuvi wenye tija. Kwa upande wa kilimo nashauri na nampongeza Waziri wa Kilimo kama walivyosoma sekta zao pamoja na uvuvi na mifugo. Nashauri mipango iliyopangwa kwenye Wizara hii iende kama hivyo hivyo ilivyopangwa. Jambo la muhimu ni utekelezaji, ufuatiliaji na kuona kuwa mipango yote inaenda kama ilivyopangwa. Kwa mfano, nikija kwenye upande wa kilimo cha mbegu, sasa hivi tunamashamba ya mbegu 17 lakini unakuta mashamba mengine hayafanyi kazi vizuri. Kwa hiyo, nashauri mashamba yote ya mbegu yafanye kazi vizuri na yaweze kutumia kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi mashamba hayatumii kilimo cha umwagiliaji, naamini tukizalisha mbegu sisi wenyewe za hapa ndani tutatokana na tatizo la mbegu. Kwa mfano, mbegu za alizeti na michikichi, Tanzania tuna ardhi kubwa sana hatuna sababu ya kuagiza mafuta ya kula kutoka nchi za nje, tunaweza kulima mbegu zetu za alizeti, tukaweza kuwatosheleza wakulima wote, tukaeneza elimu ya kulima michikichi kwenye mikoa ambayo imepangwa na tukaweza kuzalisha kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kilimo cha ngano; tuna ardhi, tuna mikoa ambayo pia bado haijaangaliwa kuwa inaweza ikalima ngano. Kwa hiyo, hakuna sababu ya kutoa ngano kwenye nchi za nje, tunaweza tukalima sisi wenyewe tukajitosheleza. Nashukuru Wizara ya Kilimo ambayo tayari imetoa vitendea kazi kwa Afisa Ugani. Kwa hiyo, Maafisa Ugani hawa wakisimamiwa vizuri naamini kuwa tutaweza kutoa na kuzalisha mbegu za

kutosha na kuweza kujisimamia kupata mafuta ya kutosha ya kula badala ya kupeleka fedha zetu kununua mafuta nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nikija kwa upande wa mifugo, tayari kuna elimu ya uimilishaji; wananchi wengi hawatumii elimu hii, elimu hii ni nzuri sana ikitumika vizuri bajeti itakwenda vizuri na watu wataweza kupata mazao bora ya mifugo. Kwa upande wa uvuvi nilikuwa nataka wananchi waweze kufundishwa vizuri elimu ya ufugaji wa samaki.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye ukusanyaji wa mapato; mapato mengi yanapotea tungeweza kupata fedha nyingi za kutosha kwenye ukusanyaji wa mapato. Tuje kwenye ukusanyaji wa mapato, hata sisi tulio humu ndani tunasema yule anayeuza aweze kutoa risiti na yule anayenunua aweze kudai risiti, lakini unakuta hiyo njia haitumiki. Kwa hiyo, naomba uwepo mfumo mzuri kama ulivyo kwenye sheli zetu za kuuzia mafuta, *whether* unaomba risiti, huombi risiti, lakini tayari mahesabu yanaonekana kuwa umechangia Serikali. Kwa hiyo, hata kwenye maduka yetu ya wafanyabiashara ionekane kuwa hizo *EFD machines* zinafanya kazi na zimewekewa mfumo wa kukusanya ada zetu ambazo tunaweza tukaongeza bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo naongelea ni kuhusu TEHAMA. Hii TEHAMA ikienda mpaka vijijini vijana wetu kupitia kilimo, mifugo na uvuvi wanahitaji kutumia TEHAMA, wanahitaji kutumia umeme, wanahitaji maji safi na salama, wanahitaji mambo ya afya. Naamini hivi vyote vikiwa huko vijijini vijana watatamani kukaa vijijini na wataweza kuendesha maisha yao huko vijijini,

watajiajiri huko vijijini, hakutakuwa na sababu ya kuvutiwa kuja mijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo naomba kuongelea baada ya kuwavutia vijana kukaa huko vijijini, nashukuru kwa upande wa kilimo, tayari na uvuvi na mifugo wameshaweka mazingira mazuri ambayo yatawavutia lakini yasimamie kwani kuwatengea ardhi, kuwapa matrekta ya kulimia ni jambo zuri ambalo litawavutia hawa watu hukohuko.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo naomba kuendelea ni kuhusu miundombinu ya *SGR*. Nashauri Mheshimiwa Waziri anasema *SGR* inakwenda vizuri, naipongeza Serikali ujenzi wa *SGR* unakwenda vizuri kipande cha Dar es Salaam kuja Morogoro kinakwenda vizuri, Waziri amesema kuwa tumefika asilimia 96.5. Kwa hiyo, naomba kipande hicho kiweze kukamilika na kiweze kufanya kazi kusudi na vipande vingine viendelee vizuri. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, lakini mambo hasa niliyosema kuwavutia vijana ikiwemo TEHAMA na kila kitu, hivyo naomba kifanyiwe kazi.

**SPIKA:** Muda wako umeshaisha Mheshimiwa.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja na bajeti

hii ni nzuri naomba itekelezwe na isimamiwe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga na Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, ajiandae.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya bajeti. Awali kabisa nipende kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu yeye ndiyo msimamizi mkuu aliyeweza kubuni mambo kama haya ambayo yamo katika bajeti hii inayomgusa mwananchi moja kwa moja. Vile vile nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake na hasa Mheshimiwa Waziri kwa kazi ambayo ameifanya namwona anafaa kabisa kuwemo ndani ya miongoni mwa wananchi. Hongera sana kwa Mheshimiwa Mwigulu kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu nitaulenga katika uchumi wa Taifa letu na nitajaribu kuupima na mapato ya kodi ya Serikali. Nimevutiwa sana kuona kwamba mapato ya kodi yameongezeka kwa asilimia18.5 ukilinganisha mwaka jana kuanzia Julai hadi Aprili na kipindi kama hicho cha safari hii na nikavutika kusema kwamba hebu niangalie mafanikio haya ya ongezeko la kodi za Serikali dhidi ya kitu wanaita *Tax to GDP*. Nilikuwa najaribu kuangalia huu uwiano wa kodi zinazokusanywa dhidi ya pato la Taifa, kwa sababu huko duniani hiki ni kipimo ambacho kinachotumiwa ili kuweza kuangalia kwamba Serikali inakusanya vya kutosha ili kuweza kuhimili matumizi yake ya Serikali pamoja na

kuiletea maendeleo nchi hiyo na kuondoa au kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, nikaona kwamba kulinganisha vitu hivyo viwili huo uwiano wa hivi viwili nikarejea kwenye andiko, kuna taasisi moja inaitwa *Action Aid,* hawa walitoa andiko niliwahi kulisema linaitwa *ceiling the gaps report* la mwaka 2021, ambapo wao wanasema Tanzania yawezekana kuna trilioni 17.4 haikusanywi, wao wanasema hivyo. Sasa katika hilo nikajaribu kulinganisha pato la Taifa kwa miaka kadhaa kuangalia ukuaji wake, je, unaakisi ukusanyaji wa kodi. Nikaangalia mwaka 2015 Pato la Taifa lilikuwa trilioni 111. Nikaja 2016 trilioni 116, mwaka 2017 trilioni 124, mwaka 2020 trilioni 145 na kote huko maana yake kulikuwa na ongezeko mwaka hadi mwaka, lakini ukienda kwenye makusanyo bado tumebakia asilimia 11, sasa hii ikanionyesha nini?

Mheshimiwa Spika, hii ikatafsiri kwamba kipato cha mwananchi wa kawaida kinaongezeka na kwa kuwa kipato kinaongezeka hebu tuangalie mwaka 2015 pato la Mtanzania lilikuwa *US Dollar* 943 sawa na Sh.2,180,000.00, ukienda mwaka 2020 pato la mwananchi liliongezeka kwenda *USD* 176. Sasa kwakuwa kipato cha mwananchi kimeongezeka ni dhahiri kabisa ingeweza ika-*translate* kuongezeka vilevile kwa makusanyo ya kodi za Serikali lakini hatukusanyi vile inavyotakiwa tumebakia 11 kwa kipindi cha miaka 10. Sasa hali hii inaonyesha kwamba hatuwezi tukafikia malengo yetu ya kukuza uchumi ipasavyo, lakini vilevile kupunguza umaskini wa watu wetu, itatupa tabu sana. Nilikuwa nikiangalia Benki ya Dunia inasema nini? Benki ya Dunia inasema angalau watu wakusanye asilimia 15 ya pato la Taifa kama kodi ili tuweze kufikia malengo yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa ukiangalia ulinganishi huo na sisi tunahitaji kuifanya nchi iwe ni *competitive* kwa maana tuvutie wawekezaji, tunatakiwa tufanye nini? *TRA* wao walikuwa wanaangalia mifumo yao, wanasema tuboreshe mifumo. Hili jambo tumelizungumza sana, mifumo ya TEHAMA izungumze, kwenye kila eneo ambalo linahusiana na ukusanyaji wa mapato, hilo nakubaliana nao. *TRA* wanasema waboreshe shughuli za forodha na hiyo ni kweli tunahitaji kuboresha shughuli za forodha kwa maana ya vitu vinavyoingia, utunzaji kodi wake na uandishi wake kwa kupitia TEHAMA hiyo ni sahihi.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo pia la matumizi ya *EFD* tumelizungumza sana masuala ya *EFD* kuhakikisha migogoro ya kikodi tumeizungumza sana fedha zilizopo kule kwenye mahakama trilioni tano na ushee, nyingine zilipo kwa Kamishna *General* wa *TRA,* zipo nyingi tu kule zaidi ya trilioni 300, sijui, zinazosemwa, elimu ya kodi hiyo inafanyika, lakini haya mambo yalikuwa yamezungumzwa humu yapo yanafanyika, lakini hatupigi hatua sasa tunataka tufanye nini?

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, nilikuwa naingalia Sheria ya *Tax Administration,* utaniruhusu niseme *tax administration* inahitaji kufumuliwa ili iwepo mipango bora ya kuhakikisha kwamba tunatanua wigo wa walipakodi. Suala hapa si kuongeza vima, tatizo la sisi wananchi wa Tanzania hasa upande wa Serikali wanam-*target* yule anayelipa kodi wanayemwona leo hiyo ni asilimia 10, kesho ni asilimia 12, asilimia 13 kama njia ya kupandisha mapato ya Serikali. Huo utaratibu ni mbaya kwa sababu watu wengi na watalaam wanasema *less is more,* weka vima vidogo ili iwe rahisi kufanya *compliance* na wengi

wataweza kulipa kodi. Ukiwawekea vima vikubwa Watanzania sisi tunaitwa wabongo, tutafuta njia ya kupenya na kupenya kwenyewe aidha tusilipe kodi, tukimbie ama tutafute njia nyingine ambazo si sahihi kwa mujibu wa sheria. Hivyo, Serikali iangalie utaratibu mzuri, tanua wigo, kodi iwe chini, hapo utawapata wengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima tuwekeze katika mifumo na namshukuru sana mwananchi Mheshimiwa Mwigulu, kwamba tulivyolisema hili mara ya kwanza wakati nipo katika kujadili hotuba ya Waziri wa Fedha katika Wizara yake nililizungumza hili na nafurahi kuona *TRA* walitufanyia semina juzi tu hapa juu ya mifumo na ule mfumo wa *IDRAS* ambao nilikuwa nauzungumzia wameuchukua kwa nguvu sana na wamekwenda kuufanyia kazi. Kwa hilo niipongeze Serikali na wawekeze katika mifumo mingine ili mifumo hii iweze kuongea.

Mheshimiwa Spika, nataka niongezee neno lingine, waboreshe mifumo ya *property tax,* mambo ya mfuto tuachane nayo yalishazungumzwa hayo sitaki niongeze sana, lakini tuthaminishe majengo ili kila mtu alipe kwa uwezo wake. Tuwekeni *scanners* huko kwenye maeneo yetu ya mipakani na naamini kabisa kutakuwa na ufanisi mwingine.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo ambalo linazungumzwa sana, ni uzito wa kufanya biashara na nataka nijikite kwenye hizi *tax audits* ambazo huzaa *interest* na huzaa *penalties,* kiasi kwamba mfanyabiashara hatimaye anashindwa kulipa kodi kwa zile kodi ambazo atakuwa hajazilipia. Sasa nilikuwa nashauri *tax audits* Mheshimiwa Waziri ananisikiliza,

angalau zifanyike kwa mwaka mara moja badala ya kusubiri miaka mitatu. Ukisubiri miaka mitatu *interest* na *penalties* zinakuwa kubwa, mtu hawezi kulipa, anafunga biashara na akifunga biashara ni hasara kwa Serikali. Kwenye hili natarajia kuleta *schedule of amendments* kuweka sharti la kisheria kwamba *TRA* ifanye *audit cycle* angalau mara moja kwa mwaka na wakikosa angalau iwe ni miaka miwili ili kupunguza mzigo wa kutengeneza *interest* na *penalties.*

Mheshimiwa Spika, lingine misamaha isiyo na tija. Hakika hili ni jambo ambalo limezungumzwa kwa muda mrefu sana. Ipo misahama mingine haitusaidii kama Serikali, haitusaidii kama wananchi. Kwa mfano, tulitoa msamaha kwaajili ya simu janja kuondoa *VAT,* bei haikupungua, bei imebakia palepale, misamaha kama hii inanufaisha sana wafanyabiashara. Tulitoa misamaha samahani kwa taulo za kike, lakini bei haikushuka, wanaofaidi ni wafanyabiashara. Unaweza ukatoa msamaha kwenye jambo ambalo pengine halina manufaa kwa mwananchi kama kupunguza au kuondoa kodi kwenye kutengeneza mitungi ya gesi, anayefaidi ni mwenye kiwanda tupunguzie kodi ya gesi ambayo mwananchi anaitumia. Sasa misamaha ambayo haina tija tuondokane nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, tuboreshe sekta isiyo rasmi. Sekta isiyo rasmi ni kundi kubwa hata hilo la Wamachinga tunalozungumza ni sekta isiyo rasmi. Uwepo mfumo ambao utafanya sekta isiyo rasmi kutambulika iwe rasmi na waingizwe katika mifumo ya kikodi, nao waweze kuchangia katika pato la Taifa lao pamoja na kodi za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa katika jambo kama hili napenda sana kuona kwamba tunaliendea kwa ukamilifu wake kuhakikisha kwamba Serikali Kuu pamoja na Serikali za Mitaa zinafanya kazi kwa pamoja. Kivipi? Tuna tatizo sasa hivi la watu wa kodi kufikia kila biashara. Nililisema hili na bahati nzuri *TRA* wakapeleka vijana 250.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Shally Josepha Raymond na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka ajiandae.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya bajeti ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na kuweza kusimama hapa nami nikiwa mmoja katika wachangiaji siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, naomba nijikite zaidi kwenye hotuba hii ya bajeti hasa kwenye masuala machache ambayo nitaweza kuzungumza kutokana na muda. Katika ukurasa wa 51 kwenye vishikwambi vyetu, kwenye *paragraph* ya 61, Mheshimiwa Waziri amezungumzia kuhusiana na suala zima la mimba za utotoni. Mimi ni mmoja kati ya wananchi wanaotoka kwenye mikoa yenye athari kubwa sana za mimba za utotoni. Asilimia 43 katika Mkoa wa Tabora mpaka

sasa kwa mujibu wa takwimu ndivyo inavyosoma, ikiongozwa na Mkoa wa Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza mkoa wetu ni mkoa ambao uko pembezoni, lakini wakati Mheshimiwa Waziri akiwasilisha hotuba yake, amesema kwamba ili kukabiliana na mimba za utotoni, Serikali itaendelea kujenga mabweni kwenye maeneo hatari kwa watoto wa kike. Hii haiwezi kuwa tiba ya kupunguza mimba za utotoni hasa kwenye mikoa yetu. Ninapokwambia asilimia 43 ni asilimia kubwa sana na tunaathirika sana sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi natokea Manispaa ya Tabora na ndiyo Halmashauri yangu. Pale tuna kata za mjini na za vijijini. Umbali peke yake wa shule anayotoka mtoto kutoka nyumbani kwao mpaka kufika shule, hiyo peke yake inachangia kwa kiwango kikubwa watoto wetu hapa katikati kupata changamoto na vishawishi vikubwa sana mpaka kupelekea watoto wetu kupata ujauzito wakiwa na umri mdogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tabora, mtoto ana miaka 12, 13, 14 unakuta ni mjamzito, inaumiza sana. Kama unavyofahamu, sasa hivi watoto wetu akifika Darasa la Nne, amekua, akifika Darasa la Tano mtoto ameshakuwa mwanamwali, na akishakuwa mwanamwali, ni lazima upatikanaji wa mimba kwa mtoto huyu ni rahisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunaposema tuongeze mabweni badala ya kufikiria kuchukua hatua mbele zaidi ya kutoa elimu. Tunaomba sana elimu ya kutosha itolewe ili kuweza kunusuru vizazi vyetu. Hali ni mbaya sana. Hawa watoto mpaka kufikia kupelekwa huko kwenye bweni, tayari mtoto ameshaharibika huku, kwa sababu ya mazingira peke yake ya elimu wanayopata watoto wetu. Kwanza ni mbali na maeneo wanayoishi.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano mmoja, tuna kata moja iko vijijini inaitwa Kata ya Ifucha. Kata ile upande mmoja inapakana na Bwawa la Kazima, upande mwingine inapakana na Kata nyingine ya Ndembelwa. Shule ambayo watoto hawa wanaotoka upande huu na upande huu iko hapa katikati. Mwendo ni mrefu kweli kweli mpaka mtoto aende akafikie ile shule. Hapa katikati anakupambana na changamoto nyingi sana za vijana wenye ushawishi, na matokeo yake hali ya watoto wetu kupata mimba wakiwa bado na umri mdogo ni changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali katika bajeti hii, badala ya kufikiria kujenga mabweni, fikirieni kutusaidia kuwapa elimu sisi wazazi pamoja na watoto wetu ili kuondokana na changamoto hii ya mimba za utotoni. Hii ni mikoa ambayo wananchi wetu uchumi wao ni mdogo sana. Yaani hawana uwezo mkubwa kiasi kwamba mtu akishaambiwa Shilingi 1,000/=, Shilingi 500/=, akinunuliwa chipsi, mtoto anaingia kwenye majaribu hayo na mwisho wa siku tunaendelea kuwa na kizazi ambacho hakina elimu na matokeo yake mtoto kuweza kuzaa mtoto mwenzie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali iliangalie hili, na ni jukumu kubwa kwa Serikali, lakini hata sisi wazazi ambao tunasaidia kuhakikisha kwamba jamii yetu inajua athari za mimba za utotoni.

Mheshimiwa Spika, niangalie katika ukurasa wa 150 kwenye vishikwambi vyetu, Mheshimiwa Waziri amezungumzia kuhusu kufuta kifungu cha Mamlaka ya Mawasiliano *(TCRA)*. *TCRA* ina majukumu yake, lakini na *TBS* ina majukumu yake tena mengi na mazito. Kazi ya *TBS* tunafahamu ni kuangalia ubora wa bidhaa zilizopo nchini na zinazoingizwa kutoka nchi za nje. Vile vile *TCRA* ni kwenye masuala ya mawasiliano. Huu ubora ambao Mheshimiwa Waziri ameuzungumza anaouhitaji, ambao tunasema uondolewe kutoka *TCRA* upelekwe *TBS* ni ubora wa aina

gani? Ni ubora wa mawasiliano ambayo tunahitaji kuyapata ama ni ubora wa aina gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri hajaweka wazi, amesema tu kwamba anafuta hiki kifungu, lakini akumbuke kwamba vipo vifungu pia ambavyo tuliviweka sisi wenyewe, lakini ni makubaliano ya Kimataifa kwenye hivi vifungu. Je, hivi vifungu ameviangalia vinaitaka nini *TCRA*? Vinataka *TCRA* ifanye nini ili kuweza kuboresha mawasiliano ya Kitaifa na Kimataifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni sawa, na kuna eneo lingine hapa wakati napitia amesema kwamba hata pamba sasa itakuwa inaangaliwa na *TBS*. *TBS* wana Mabwana Shamba? *TBS* wana Mabibi Shamba? Mabibi Shamba na Mabwana Shamba ndio wanaoangalia ubora wa pamba. *TBS* anakwenda kukutana na nyuzi ambazo tayari zimeshatengenezwa. Wao wanatakiwa waangalie ubora wa ile mali ambayo tayari inakwenda kwa mlaji na siyo kuangalia mkulima amelima nini? Zile ni kazi za watu wengine. Hii itakuja kuleta changamoto baina ya taasisi na taasisi kuweza na kukuta kunakuwa na migongano na mwisho wa siku inakwenda kuathiri wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri ajaribu kuangalia hiki kifungu ambacho anataka kukifuta na kukitoa *TCRA* kukipeleka huko kwenye *TBS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze kidogo kuhusiana na suala la utalii. Kwanza naomba na mimi nimpongeze Rais wetu Mama Samia kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kuhusiana na hili suala la *Royal Tour* ambalo Wabunge tumekuwa tukilipigia kelele muda mrefu kwamba tunahitaji kutangaza utalii wetu. Tunahitaji utalii wetu ujulikane. Leo mama ameshafanya kazi yake,

ameshamaliza. Sasa kazi ni kwetu sisi kuhakikisha kwamba yale ambayo yanatakiwa kufanyika yanafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niko kwenye Kamati ya Maliasili na Utalii. Bado kuna changamoto kubwa sana, hususan kwa hawa wawekezaji kwenye masuala ya utalii. Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha kwamba inakutana na hawa wawekezaji tulionao ndani kabla hatujaamua kwenda kutafuta wawekezaji wengine ili waje kuwekeza hapa? Kwa sababu hawa waliko ndani wenyewe wana changamoto nyingi sana ambazo bado hazijapatiwa ufumbuzi. Changamoto hizi zinasababisha hata mapato kwenye masuala ya utalii kupungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hatujiulizi kwa nini wageni wanapokuja wakiondoka hawarudi tena? Shida ni nini? Wapi kuna changamoto? Nini kifanyike? Je, hawa wawekezaji ambao wako kwenye hii *sector* ya utalii tumewaandalia mazingira rafiki ya kuhakikisha kwamba wanafanya kazi zao kwenye mazingira mazuri? Tatu, hii *royal tour* inaenda kutotoa? Hata sasa hivi tunasema tu kwamba *Royal Tour* tayari, *Royal Tour* bado. Hawa ni wageni ambao wamekuja kwenye mwaka huu ambao walikuwa wameweka *booking*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *Royal Tour* ni kuanzia mwakani, tumejiandaa namna gani kuhakikisha tunapokea hawa wageni? Je, baada ya kuwapokea, tumejiandaa namna gani kuhakikisha hawa wageni wanarudi? Je, Serikali kupitia Wizara ya Utalii inafanya kazi yake ipasavyo kuhakikisha kwamba tunaleta wageni wapya lakini hata wale waliokuja na wenyewe wanaendelea kurudi katika nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishauri sana Serikali, badala ya kuangalia tunahitaji wawekezaji wengine, tuanze kuangalia wawekezaji wetu wa ndani ili tuweze kuwasaidia kwenye changamoto zao na baada ya hapo, hata hao

wengine wa nje watakuja kwa sababu kuna mazingira rafiki ya uwekezaji kwenye sekta ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami naomba nizungumze kwenye hii asilimia 10. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, hii asilimia tano anayofikiria kuichukua aiache tu, kwa sababu hata hiyo asilimia 10 yenyewe, tunachosema sisi Waheshimiwa Wabunge, haitoshi. Haitoshi kwa sababu Halmashauri zetu tumetofautiana kimapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi natokea Halmashauri ya Tabora Mjini, lakini huwezi kuamini sisi tunashindwa mapato na Halmashauri ya Kaliuwa. Nasi pale Tabora Mjini ndio tuna Wamachinga wengi kuliko Halmashauri ya Kaliuwa. Kwa hiyo, ukimchukulia asilimia tano huyu mtu wa Tabora Mjini, ina maana asilimia tano inayobaki haiwezi kusaidia hata wale wamama na vijana na watu wenye ulemavu ambao tunategemea kwamba hizi fedha zinawasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitamani sana Mheshimiwa Waziri aje na pendekezo la kuongeza badala ya asilimia 10 zifike asilimia 15 mpaka 20 ili tuweze kuwasaidia hawa akina mama wetu, vijana pamoja na watu wenye ulemavu. Chonde, chonde Mheshimiwa Waziri, acha hiyo hela, asilimia tano hiyo iache tuendelee na asilimia zetu 10. Lete sheria, tafuteni utaratibu mzuri wa kuhakikisha tunawasaidia Wamachinga waweze kupata maeneo yao. Tunao Wamachinga wengi, lakini mwisho wa siku tutafute utaratibu mwingine lakini siyo kuchepua hela ambazo tayari tulishakubaliana nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kuhusiana na suala zima la hizi nywele bandia. Nataka nipate ufahamu, Serikali imefanya tathmini ya kugundua kwamba tuna viwanda vingapi Tanzania ambavyo vinatengeneza nywele bandia? Je, katika hivyo viwanda, ni viwanda vingapi vinavyotengeneza *quality,* yaani nywele ile nzuri ambayo

hata mtu ukivaa unaonekana umependeza? Ni viwanda vingapi ambavyo vinafanya hiyo kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu unaweza ukasema kwamba unataka kulinda viwanda vya ndani lakini ndiyo ukaenda kuviua kabisa kuliko ambavyo ilivyo hivi sasa. Leo mimi nafanya biashara ya nywele, nina uamuzi, niuze nywele za kutoka nchini kwangu ama niuze nywele za kutoka nje ya nchi? Ila tufahamu, hii biashara ya nywele inafanywa na akina mama wenzetu. Wako akinadada ambao wanaishi maisha yao kwa kutegemea hii biashara ya nywele, lakini wanalipa kodi ya Serikali, hawajawahi kukwepa kodi hata siku moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni mdau mmojawapo na-*declare* kwamba na mimi navaa na ndiyo maana hiki nilichokivaa mimi kinaweza kikawa tofauti na kitu alichokivaa mtu mwingine. Kwa sababu unaweza ukavaa wigi ukajikuta ukitoka hapa mtu anashangaa hivi yule dada ni Mbunge kweli! Unavaa wigi unapendeza mpaka kila mtu anakuuliza. Sasa ndiyo *quality* zinakwenda namna hiyo. Je, sisi Watanzania kwenye viwanda vyetu tuko tayari kutengeneza wigi ambazo hata nikija dukani nasema hii nitavaa nitapendeza? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hebu tuwaache hawa akinadada ambao wanafanya hizi biashara wamekuwa maharufu sana. Wakina Luluz, Loluwa, na kadhalika wanaleta nywele nzuri ambazo kila mmoja anatamani aweze kuvaa na aweze kupendeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nakuomba sana nimuombe Mheshimiwa Waziri, hii ni sekta muhimu kwetu sisi, kwa hiyo, naomba sana atusaidie angalau kidogo kuacha ile kodi jinsi ilivyo, wanawake wenzetu waendelee kufanya biashara na waweze kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, atafuatiwa na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka na Mheshimiwa Jesca Kishoa ajiandae.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kipekee namshukuru Mungu aliyetuweka hapa leo, tuna afya njema na tunazungumzia jambo muhimu sana katika nchi yetu, bajeti ya Serikali ya Tanzania mwaka 2022/2023 iliyowasilishwa hapa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Rais wetu mpendwa, Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea bajeti ambayo ni ya viwango. Watanzania wanajua, dunia nzima inajua kwamba sasa hivi mwanamke anayeongoza Tanzania anafanya vitu vyake kwa hali ya juu na kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana mwasilishaji wa hoja hii ambaye ni Waziri wetu wa Fedha na Mipango, Dkt. Mwigulu Nchemba na timu yake yote; makamu wake, Katibu Mkuu na watendaji wote. Jambo hili limefanyika vizuri na nitamke rasmi, naunga mkono hoja japo pia nina michango ambayo nataka aboreshe na aipokee na wengine waliyoyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze tu kwanza kwa kusema jambo hilo la kusoma *Form One* mpaka *Form Six* bila ada ni jambo jema, na wote wameyasikia, wavulana kwa wasichana. Wakati tunaenda jeshini miaka hiyo, mwaka mmoja ukiwa umetoka *Form Six,* maafande wale wanakwambia hao ni wasomi mpaka wakakuta *no class,* yaani unagonga *no class* ndiyo *Form Six.*

Mheshimiwa Spika, sasa nawaomba watoto wetu walio Tanzania nzima wasome mpaka wakute *no class,* hakuna mbadala. Jambo hili linaenda kupunguza mimba za utotoni, kwa sababu kama wewe ni mwanafunzi na mtu akija akigusa mwanafunzi kifungo ni chake. Hiyo ndiyo adhabu. Sasa sijui mabinti zetu nini kitawazuia wasisome mpaka wamalize? Vile vile hao vijana wasichezecheze na watoto wa wenzao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kushukuru kwa jambo hilo, nije na lile ambalo limeleta taharuki kidogo, ni hili jambo la asilimia 10. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, jambo hili ameliongelea vizuri sana mwenzangu aliyenitangulia kabla, alikuwa ni Mheshimiwa Husna. Kwamba hii asilimia 10 ilipowekwa ilikuwa na madhuni maalum. Ukienda kule *library* ukasoma *Hansard* miaka hiyo ya 1994 hili jambo halikuwa rahisi wala jepesi. Ilikuwa ni asilimia 10 kwa wanawake na wanawake hao ni wale wanawake ambao hawakopesheki, hawana dhamana yaani hawana *security,* hawezi kwenda kwenye benki kukopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati huo waliotutangulia wakaona kwamba basi tuwawezeshe akinamama na ikafanyika hivyo. Pia ukizingatia ukiiwezesha kaya, umewezesha kata, umewezesha tarafa, umewezesha wilaya, umewezesha mkoa na Tanzania nzima. Sasa iweje leo Serikali inataka kuwajengea wajasiriamali miundombinu, wanaona waje pale kwenye ile asilimia 10? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi juzi, miaka michache iliyopita, mwaka 2008 wali-*beep* wakaitoa ile asilimia 10 ikaenda kwenye 4,4,2. Wanawake walivyo wasikivu wakanyamaza. Kelele zilipigwa za kichinichini na mnajua wenyewe, kwa sababu wote hapa ni Wabunge na hata yeye ni Mbunge, anajua jambo lililokuwa linaendelea. Ile hela nyingine ilikuwa sasa watu wasaidie, Wabunge wasaidie kutoka mfukoni. Sasa

mnakuja tena kugusa pale pale. Yaani unaweka chumvi kwenye kidonda. Unawagusa tena wale wanawake, unataka tena kuondoa utamu, iweje? Kwani mwanamke akipata nani kapata? Inakupunguzia mzigo wewe baba, inamwezesha mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali yangu sikivu, Serikali ya Chama cha Mapinduzi, isikie jambo hili, waachieni wanawake hiyo asilimia yao ilivyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na maombi hayo, sasa naomba nizungumzie sekta binafsi. Sekta binafsi ni eneo ambalo sasa linatakiwa lifanye kazi kwa kukimbia kabisa. Mheshimiwa Rais wetu amesema, Serikali ipo tayari kuweka miundombinu mizuri ya wafanyabiashara au ya sekta binafsi kufanya biashara zao vizuri. Hili ni kweli, amedhamiria. Sasa hii sekta binafsi nayo inatakiwa pia isaidike.

Mheshimiwa Spika, unakuta kwamba kama watakuja wafanyabiashara wa sekta binafsi kutoka nje tu wakafanya na haupati hiyo faida yao, huku ndani hatutaweza kui-*feel* vizuri, lakini kama wafanyabiashara wa kwetu wa sekta binafsi watafanya vizuri, basi kila mtu atai-*feel* yale maendeleo au wata-*feel* biashara yao waliyofanya hapa kuwa wamepata chochote. Itasikika vijijini na itasikika mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba wafanyabiashara hawa wawezeshwe. Wawezeshwe katika njia nyingi, mpaka sasa Serikali imeshafanya kiasi kikubwa sana. Imewawezesha kwenye miundombinu; barabara, reli, na viwanja vya ndege. Hiyo yote Serikali imeshafanya, lakini sasa tunakwenda kuwawezesha zaidi katika kule kwenye zile ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakuta kwamba mfanyabiashara anapokuja kwa kuajiri mishahara

inatofautiana na pia kodi zinatofautiana, sasa inatakiwa watu wetu tuwaelimishe wanapoenda kufanya kazi kwenye sekta binafsi wawe na nidhamu ya sekta binafsi, kuna mambo yamezoeleka *business as usual* hapana siyo kwenye sekta binafsi! Amefunga safari au mtu amefungua shughuli yake iwe ni hoteli iwe ni nini, anatarajia wewe unaenda kufanya kazi kwake uwe na nidhamu ya kutosha ili aweze kuzalisha kama anavyotarajia.

Mheshimiwa Spika, miaka 94 wakati *TBL* imetaifishwa ilibidi yale mashamba ya kuzalisha shayiri na ngano kule *West* Kilimanjaro itolewe kwa wakulima au sekta binafsi, kweli walikuwepo Watanzania waliojiotolea, wakati huo walikuwako Watanzania wanne waliungana, lakini ukaja kutokea mgogoro yale mashamba wakanyang'anywa sasa walipokuja baadaye, kuja watu wa kutoka nje kuwekeza hawalimi tena ile shayiri na ngano katika kile kiwango kikubwa, matokeo yake ni nini, ni kwamba matokeo yake ni kwamba sasa mashamba yale yamebaki hivyo hivyo na ukienda kule unakuta wana-*import* ngano kutoka nje.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa *BASUTA* imeenda wapi? West Kilimanjaro imeenda wapi? Kwa nini tuna maeneo makubwa hayo na hatuwezi kuzalisha kama tunavyotaka, kwa hiyo nilikuwa naomba sana Serikali iweke jicho la ziada kwa hao watu wa sekta binafsi ili waweze kupata ushindani, ushindani kwa huku huku ndani wenyewe lakini pia ushindani na wale wanaokuja ku-*invest* katika nchi yetu na ikiwezekana hawa wa ndani wawazidi hata wale.

Mheshimiwa Spika, sekta binafsi ninayoweza kuzungumzia ni sekta ya hawa Makandarasi. Tumeona kwamba Makandarasi wa nchi kwetu wanapata kikwazo sana pale kwa ule mtaji wa Bilioni 10, wao hawaruhusiwi kwenda zaidi, sasa matokeo yake wanaopata hizo kazi za *REA*, wanaopata kazi za kwenye maeneo makubwa mengine ni hawa *contractors* kutoka nje, lakini nilikuwa naomba iletwe hapa ile Sheria ya *PPRA* ibadilishe kile kiwango cha *Ten Billion* kiweze kwenda juu waruhusiwe hawa ma-*controctors* waungane hata kama ni barabara kubwa wao waweze kupewa kwa jumla halafu wagawane hiyo barabara kwa sababu kama ni viwango vinavyopimwa kwa wale wa nje ndio hivyohivyo vinavyopimwa kwa watu wa ndani.

Mheshimiwa Spika, haina maana mtu amsomeshe kijana wake afanye *engineering* miaka minne halafu afanye tena *field,* aje aajiriwe aambiwe hapana uwezi kupata kazi mpaka waje hao ma-*contractor* wa nje! Sasa mkumbuke tu kwamba wakishapata wale zinakwenda kuliwa nje na sio hapa. Kwa hiyo, hilo namuomba sana Waziri aweze kuliangalia.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo ni kwenye huo uwezeshaji niliozungumza nyingi ni *Commercial Banks* zinakopesha sisi tuna benki yetu Tanzania *Investment Bank,* ni benki ambayo ilikuwa ni ya kuwawezesha wananchi wakope ndani, lakini ni benki ambayo katika nchi nyingine *any Investment Bank* ni benki kubwa na hapa ndani miaka iliyopita walisema kuwa Serikali ilisema ingewasaidia mtaji, lakini tuna miaka kadhaa hawajaweza kupata mtaji, pia hatujaweza kujua nini kinaendelea *TIB* mpaka sasa hatuoni kama wanatoa mikopo ya kutosha, hata Serikali yenyewe ingeweza

ikakopa huko hela za kujenga hiyo reli – *SGR,* hela za kujenga Bwawa la Mwalimu Nyerere, matokeo yake unakuta tunakwenda kukopa mahali ambako Tunadaiwa faida kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuunga mkono hoja niwaombe wenzangu nao waunge mkono hoja ili Waziri huyu aachiwe mapema akatekeleze hayo majukumu na wote tuweze kupata hii keki ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru nilishaunga hoja mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Kabla ya mchangiaji anayefuata niwatangaze wageni walioingia hapa Bungeni kwa ajili ya mafunzo. Tunao Wanafunzi 100 na Walimu 10 kutoka Shule ya Awali na Msingi ya Ellen White ya Jijini Dodoma, karibu sana Bungeni na tunawatakia kila la kheri katika masomo yenu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilishamtaja Mheshimiwa Christopher Ole Sendeka atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Kishoa Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos ajiandae.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuliongoza Taifa hili na hatua aliyokwisha lifikisha Taifa hili kwa mwaka mmoja ni hatua kubwa sana ambayo kila mtu ni lazima aiunge mkono.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee pia nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha Daktari Mwigulu, kuanzia hotuba yake ya Mpango na hotuba yake pia ya Bajeti, Mheshimiwa Waziri ninakutakia kila lililo jema kwa sababu mipango bora ya sasa ndiyo itakayoamua kesho iliyo njema ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye hoja ambayo ningetaka nigusie na maeneo ambayo nimeyachagua kuyazungumza. Nianze kwa kuyanukuu maneno ya Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika Kitabu chake cha Uhuru na Maendeleo, ukurasa wa Tisa naomba kunukuu kwa ruhusa yako. ''…..kama tunataka maisha yetu yawe na amani na raha na kama tunataka kufanikiwa katika shabaha zetu na kuinua maisha yetu, basi lazima tuwe na uhuru pamoja na utii. Maana uhuru bila utii ni wazimu na utii bila uhuru ni utumwa''. Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba tena nifanye nukuu ya pili ili niendelee na ninaifanya katika imani za mwanachama wa CCM, nataja imani ya kwanza na imani ya pili, inasema… ''binadamu wote ni sawa na ya pili ninasema kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake''. Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, jamii ninayotokana nayo, jamii ya Wafugaji au jamii ya Wamasai katika kipindi hiki wanapita katika taharuki na huzuni kubwa kutokana na maamuzi ya Serikali yanayoendelea katika eneo la Ngorongoro, eneo la Loliondo na sasa tamko la Waziri wa Maliasili na Utalii juu ya nia yake ya kutangaza kupandisha hadhi baadhi ya mapori tengefu kuwa mapori ya akiba.

Mheshimiwa Spika, naomba ninukuuu maneno ya Waziri wa Maliasili na Utalii katika hotuba yake aliyoitoa Tarehe Tatu yanasema hivi …. ‘‘eneo la Idara ya Wanyamapori; Mheshimiwa Spika, Wizara inatarajia kupandisha hadhi mapori tengefu ya Lake Natron, Kilombero, Loliondo, Lolkisale, Longido, Muhuwesi, Umba River, Mto wa Mbu, Simanjiro, Ruvu Masai, Ruvu Same na Kalimawe, misitu ya Litumbandyosi na Gesimazoa kuwa mapori ya akiba. mwisho wa kunukuuu.

Mheshimiwa Spika, suala la mapori tengefu kupandishwa hadhi, kwa maana maeneo ambayo Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii ameyatamka katika Wilaya ya Simanjiro maana yake Simanjiro kwa ujumla wake sasa inatarajiwa kupandishwa hadhi kwenda kuwa pori la akiba, maana Simanjiro kwa asilimia 100 ni pori la akiba kwa mujibu wa Sheria ya Mwaka 1951 ya *Fauna Conservation Ordinance* Sura ya 302. Mapori yale yalipotangazwa Simanjiro yote na niseme *the whole of Masai land* wakati wa Masai *District Council* karibu yote ukiacha maeneo ya *National Parks* ni *game controlled areas.*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Fauna *Conservation* ilikuja kubadilishwa na Sheria ya Uhifadhi ya mwaka 1974, na Sheria ya 1974 ya uhifadhi ilifutwa na Sheria Na. 5 ya Mwaka 2009. Sheria zote Mbili nilizozitaja za mwanzo *Fauna Conservation Ordinance* na Sheria ya Uhifadhi ya mwaka 1974 hayakufanya maeneo ya *Game Controlled Areas* au maeneo ya mapori tengefu kuwa maeneo yanayokataza malisho makazi na vijiji kuanzishwa ndani ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, sheria mpya ya Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009 iliyafanya mapori tengefu kuwa na hadhi ambayo shughuli za binadamu haziruhusiwi isipokuwa kwa kibali cha Mkurugenzi wa Wanyamapori. Kwa maana hiyo Waziri alitakiwa kwa mujibu wa sheria hiyo na hasa Kifungu cha 16(1) ilimtaka Waziri kutamka na kutangaza katika gazeti la Serikali eneo lolote la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa pori tengefu, lakini sheria hiyohiyo Na. 16 Kifungu Kidogo cha (4) ilimpa Waziri huyo muda wa kuchukua zoezi hili la kuyapitia mapori hayo tengefu yote ambayo yako 49.

Mheshimiwa Spika, Kifungu hicho cha 16 cha Sheria ya *Warrant Conservation Act,* ikamkataza Waziri mwenye dhamana ya Maliasili na Utalii kuingiza eneo lolote la ardhi ya Kijiji katika eneo hilo la pori tengefu. Kwa maana hiyo ni kwamba hakuna ardhi ya kijiji ambayo kwa mujibu wa sheria itageuzwa kuingizwa katika ardhi ya pori tengefu, na kwa maana hiyo shughuli zinazoendelea katika Tarafa ya Loliondo na Sale ya kuchukuwa ardhi vijiji vya Kata Saba, Nane za Tarafa ya Loliondo na Sale na kuunda pori tengefu la Loliondo katika sura ya sheria niliyoitaja, ni zoezi batili na linastahili kukemewa na mtu yoyote anayeyatakia mema Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, ninasema hayo kwa kutaja vifungu hivyo vya sheria vinavyokataza kuchukua ardhi ya Kijiji na kuifanya kuingia katika pori tengefu, lakini wakati Loliondo yakiendelea na ya Ngorongoro yakiendelea Waziri mwenye dhamana kana kwamba haoni jeraha hilo kwa jamii ya wafugaji, anatangaza sasa kuifanya Simanjiro kwa ujumla wake kuwa pori la akiba ndiyo kusudio lake, kwa maana ya mapori tengefu aliyoyataja. Kwa lugha nyingine anatangaza Wilaya

nzima ya Longido kwa kuchukuwa *Natron game controlled area* na Longido *game controlled area,* sasa Longido yote kwa asilimia 100 kwa nia ya Mheshimiwa Waziri Pindi Chana sasa itatarajiwa kuwa pori la akiba na sijui wananchi wale wanaenda wapi. Kana kwamba hiyo haitoshi eneo la Ngorongoro lililokuwa limebaki katika Tarafa ya Sale na Loliondo nalo linamegwa katika sura hii.

Mheshimiwa Spika, ukiondoa eneo la Km 8,300 za Tarafa ya Ngorongoro eneo linalobaki kwa wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro ni Km. za mraba sizizozidi 2007 kwa watu wapatao zaidi ya 180,000. Jambo hili kwa vigezo vyovyote vile haiwezi kukubalika, ushauri wangu kwa Serikali yangu Chama cha Mapinduzi, ni kukaa na wananchi katika eneo la Loliondo, na kuwashirikisha kama ambavyo barua ya Mheshimiwa Waziri Mkuu Mstaafu Mizengo Kayanza Peter Pinda ilivyoelekeza alivyokuwa amemuandikia Mkuu wa Mkoa wakati huo wa Mkoa wa Arusha kwamba wananchi washirikishwe kwa sababu sheria haziruhusu kulichukuwa eneo hili na kulifanya kuwa Pori Tengefu.

Mheshimiwa Spika, kugeuza ardhi za Wilaya hizo zote za Masai maana wamasai wana Wilaya hizo nne ndiyo ambalo ndiyo wako *majority* leo kuyageuza yote kuwa mapori ya akiba yanatwisha mzigo wa kujiuliza dhamira yake ni nini?

**NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole-Sendeka kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mary Masanja.

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa ambae ametoka kuzungumza sasa kwamba hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii iligusia maeneo ambayo hayatahusisha maeneo ya vijiji vya wananchi, kwa hiyo maeneo yanayoenda kupandishwa hadhi, kutoka mapori tengefu kwenda mapori ya akiba ni maeneo *potential* tu kwa ajili ya uhifadhi na hayana wananchi ndani yake. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole-Sendeka unapokea taarifa hiyo?

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikuhakikishie wala silpokea maana wala haina hadhi ya taarifa, kwa sababu akisoma *section 16 sub-section (5)*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole-Sendeka

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, naam!

**SPIKA:** Kanuni unazifahamu vizuri, unapokea taarifa au unaikataa unaendelea na mchango wako.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, ninakataa silpokei, kwa sababu ukweli unabaki hivi kwamba alichokitangaza Waziri ni kupandisha mapori ya akiba yaliyoanzishwa na *Fauna Conservation Ordinance* kuwa *game reserve,* wakati yeye mwenyewe anajua

kabisa kwamba pori, *game reserve* inaanzishwa na Rais kwa mujibu wa Kifungu cha 14, anamuuzia Rais Mbuzi kwenye gunia kwa sababu yeye mwenyewe hana mapori tengefu hajayaanzisha, kwa mujibu wa Sheria hiyo Na. 16 (1). hujaanzisha kitu halafu unamwambia Rais aanzishe pori la akiba na unafanya hivyo katika Wilaya Nne kamili. Kwa kweli nia hiyo siyo ni njema na Wizara hiyo mnapaswa mjitafakari, muangalie na mpitie maamuzi yenu, lazima yajenge haiba nzuri kwa nchi yetu, yajenge haiba nzuri kwa raia waliotuchagua yajenge haiba nzuri ya nchi yetu katika uso wa dunia.

Mheshimiwa Spika, nataka nirudie kusema….

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole-Sendeka nakulindia muda wako Makatibu mtazame hapo.

Mheshimiwa Naibu Waziri, hii taarifa uliyoitoa kwamba maeneo yale yanayopandishwa hadhi hayana wananchi, Mbunge anasema hayo maeneo yana wananchi, sasa hebu fafanua vizuri hapo, kwa sababu upotoshaji upo kona gani kwenye hoja hii. Hayo maeneo yanayo wananchi au hayana wananchi ili kama hayana wananchi mchango wa Mheshimiwa Ole-Sendeka nitakuwa na mazungumzo nao huo mchango wake kama maeneo hayana wananchi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba nirudie tena ili muongeaji asikie vizuri. Haya maeneo ni maeneo ambayo yalikuwa ni mapori tengefu *Game Controlled Areas*. Maeneo haya yanapokuwa na hadhi nzuri na haya maeneo kwa asilimia kubwa yanawawekezaji tayari, hivi ninavyoongea kuna wawekezaji ndani yake, kuna wawindaji wa kitalii

nakadhalika. Tunapoona yana sifa ya kuhifadhiwa ili wananchi wasiendelee kuwasongelea tumeyapandisha hadhi. *Game controlled area* inapanda kuwa *game reserve*, *game reserve* inapoongezeka kuwa sifa tunapeleka kwenye *National Park*. Sasa tumeona haya maeneo yana hadhi ya kupanda kutoka kwenye *Game Controlled Areas* kwenda kwenye *game reserve* na hayana wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie hili aelewe vizuri, amesema kwamba asilimia 100 ni maeneo ya wananchi, na hii kauli niwaombe Waheshimiwa Wabunge wanapotumia maeneo eti ardhi yetu, Tanzania ardhi ya Umma, siyo ya mtu mmoja. Tunawagawa wananchi tunaposema kwamba haya ni maeneo ya kwangu, haya ni maeneo ya nani!

Mheshimiwa Spika, tunapoona haya maeneo hayana watu tumeyahifadhi vizuri na yamekuwa na sifa nzuri, tunayapandisha hadhi. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni asilimia 100 haya maeneo hawamo wananchi ndani yake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole-Sendeka nimekusikiliza kwa makini sana, ukizungumzia hizo sheria, ukivitaja na vifungu. Maelezo niliyomtaka atoe ya ziada Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, ambayo wananchi ndiyo maneno kama haya yanayozungumzwa, kwamba wananchi watahamishwa hayo maeneo yote wanayoishi huko ndiyo yanayoleta taharuki! Kwa mchango wako Mheshimiwa Ole-Sendeka unaashiria kwamba wananchi wote wa Simanjiro asilimia 100 watatakiwa kutoka huko kwa agizo la Mheshimiwa Waziri. Hebu fafanua hapo ili mimi nijue upotoshaji upo sehemu gani.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, mapori tengefu hayo ambayo Waziri anayazungumza kwanza ili uyajue ni mapori tengefu ambayo yalishafutwa na Sheria Na. 5 ya mwaka 2009 na yakamwelekeza Waziri hivi….

**SPIKA:** Kwa kuwa sheria unayo hapo nisomee Mheshimiwa.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikusomee.

**SPIKA:** Nisomee.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, *for the purposes,* nakusomea *section 16 subsection (5). …. ''for purposes of subsection (4), the Minister shall ensure that no land falling under the village land is included in the game controlled* areas. Lakini….

**SPIKA:** Nisomee *subsection four*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, ngoja nirudi sasa *exactly*, ngoja nikuanzishie na hiyo *subsection (4),* safi sana nakushukuru sana. Ninaanza na one ili tuenda *four*.

**SPIKA:** Soma *four*, tutaenda kwa mtiririko huo mpaka tutafika sehemu nzuri wala usiwe na wasiwasi soma *subsection four*.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, *subsection four, The Minister shall, within twelve months after coming into operation of this Act and after consultation with the relevant authorities, review the list of game-controlled areas for the purposes of ascertaining potentiality justifying continuation of control of any of such area.*

Mheshimiwa Spika, sasa *subsection (1)*...

**SPIKA:** Sawa ngoja umeshanisomea hiyo 16 ngapi ngapi na nimekusikiliza, sasa hebu nisomee kwenye hiyo hiyo sheria kifungu kilichofuta, kwa sababu umesema hiyo sheria imefuta hayo maeneo, hebu nisomee hicho kifungu kilichofuta, nakupa muda nisomee kifungu kilichofuta.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, kifungu cha 16 nilichokusomea kwamba Waziri atayapitia mapori hayo tengefu na ku…

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole-Sendeka kupitia ni sawasawa na kufuta?

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, ndio nilikuwa nataka nikusomee, twende moja turudi nne, twende tano ili wewe Mwanasheria utusaidie.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole-Sendeka sheria huwa inasomwa namna ulivyoanza, wakakuambia *subject to subsection (4)*. Kwa hiyo, kabla hujamaliza kile unakwenda kwenye kifungu kidogo cha (4) ambayo umeshanisomea. Sasa katika kifungu kidogo cha (1) mpaka (4) kuna mahali wanasema wamefuta, kwa

sababu ile kifungu kidogo cha (1) uliyonisomea na (4) uliyonisomea, hakuna mahali niliposikia yamefutwa. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, sitaki kubishana na wewe katika *angle* ya sheria.

**SPIKA:** Kwenye hoja hii mimi ndiyo niliyekupa ruhusa kwa sababu nazungumza nawe..

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Ili nielewe upotoshaji upo wapi?

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, kweli ni hivi kabla sheria hii ili utusaidie wote, maeneo ya *Game Controlled Area* ilikuwa ni ardhi ambayo ni ardhi za vijiji kwa wakati huo. Kwa hiyo...

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole-Sendeka sheria unayo wewe mwenyewe, nimekwambia usome wewe mwenyewe na mimi nakusikiliza, sasa nakupa nafasi hebu soma hicho kifungu kidogo cha (1) mpaka (4) labda nitasikia mahali uliposema pamefutwa hebu soma.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE–SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kwenye *section 16 (1); subject to section 4(2) of the Land Act, the Minister may, after consultation of the relevant local authorities, and by order in the Gazette, declare any area of land in Tanzania to be a Game Controlled Area.*

Baada ya mamlaka hayo ya kutamka na kutangaza…

**SPIKA:** Nisomee umalize ili tuwe tunasikilizana, soma moja mpaka nne kama ulivyosema na mimi nakusikiliza kwa makini sana. Soma sheria yako uliyonayo, usiongezee maneno kwa sababu nitahisi pengine umeanza kutafsiri. Wewe nisomee ili mimi na wewe twende ngazi kwa ngazi.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE – SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nilishakusomea kifungu kinachoanzisha *Game Controlled Area* na ambacho ni kifungu cha 16(1), nimeshakusomea kifungu hicho cha …

**SPIKA:** Umesema nikupe nafasi unisomee kifungu cha 16(1) mpaka (4) ndio nitaelewa, si ndio umesema hivyo?

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE–SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, sawa kwa hiyo nirudie.

**SPIKA:** Nisomee pengine nitasikia neno la kufuta ili nimshike sasa Naibu Waziri kwamba yeye ndio anayezusha.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE–SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nirejee kwenye wapi ambapo nimenukuu kwamba sheria moja inapoanzishwa inafuta nyingine, naomba nimnukuu barua iliyoandikwa na Waziri Mkuu Mizengo Kayanza Peter Pinda.

**SPIKA:** Naomba unisomee Sheria kifungu cha 16(1) mpaka (4).

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE–SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, sawa niende kwenye (4), niende kifungu 16(4).

**SPIKA:** Kifungu kidogo cha (2) umeshasoma tayari?

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE–SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, *no* hapa...

**SPIKA:** Nisome (1) mpaka (4), mimi ninakurahisishia ili nikuelewe, nakulinda na Naibu Waziri naye namlinda.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE–SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nilinukuu kwenye sheria na nikawa nakusomea kwa hiyo (2) haikuwa na uhusiano na hoja yangu, kwa hiyo ambazo nimezitaja ndizo zilikuwa na uhusiano na hoja yangu.

**SPIKA:** Kama hivyo ndivyo, maelekezo yako marefu niliyoyasikiliza, kifungu cha 16(1) na 16(4) ulivyonisomea, hakuna mahali panaeleza kwamba hayo mapori tengefu yaliwahi kufutwa. Hakuna na kwa maelezo aliyoyatoa ya ziada Mheshimiwa Naibu Waziri hakuna mahali ambapo maelekezo ya Waziri mwenye sekta yanasema watu wa Simanjiro na pori tengefu wanaondoka, hakuna. *(Makofi)*

Sasa haya maneneo ya kwamba maeneo yote ambayo wanakaa Wamasai katika Wilaya nne zote wanaondoka, yametoka wapi?

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE–SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, hapo ndiyo mahali ningeomba wote wanisikilize. Kabla ya sheria hii tunayozungumza namba tano, maeneo yaliyokuwa yanaitwa mapori tengefu ni maeneo ambayo shughuli za binadamu zilikuwa zinaruhusiwa na

zilikuwa zinahifadhiwa kwa mujibu wa sheria hizo mbili nilizozitaja ya mwaka 1974 na ile ya mwaka 1951. Ilipokuja sheria hii ndiyo ikapandisha pori tengefu kupewa hadhi sasa ya kuwa ya miongoni mwa *reserved lands* ambazo shughuli za binadamu haziruhusiwi. Ili hilo liwezekane ilikuwa lazima mapori hayo yapitiwe kama ilivyosema *section (4)* halafu mwishoni yatangazwe na Waziri mwenye dhamana baada ya kufanya *consultation* na *local authorities.*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo...

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole-Sendeka unanipa wakati mgumu sana, kwa nini unajua? Sheria uliyosoma hapo imetumia neno *may,* mimi nikakusikiliza kwa sababu wewe unajua sheria, mimi pia ni Mwanasheria. Umesoma mwenyewe hapo, hakuna mahali palipofuta, hilo ni la kwanza, maana ulianza kwa kusema kwamba sheria ilifuta hujasema ni wapi sheria ilifuata, moja.

La pili, umesema maeneo yote wanayokaa Wamasai maeneo ambayo ni mapori tengefu, Wamasai wanaondoka kwa sababu maeneo hayo yamepandishwa hadhi. Mheshimiwa Naibu Waziri pale ametoa ufafanuzi kwamba si kweli maeneo yanayopandishwa hadhi wananchi huko hawapo. Kwa hiyo hapo wewe ukiambiwa kwamba unazikosea kanuni zetu, ukiambiwa wewe Mheshimiwa Ole-Sendeka unazikosea kanuni zetu, kwa nini? Kwa sababu umesema jambo ambalo halipo, kwa sababu la sivyo wote ninyi, jamani mimi ndiyo shughuli yangu hapa ya kusimamia kanuni.

Mheshimiwa Ole-Sendeka tukiendelea kwa mtindo huo, nitataka uniletee ushahidi na Mheshimiwa Waziri ataleta na yeye wa kwake, halafu mimi nitafanya maamuzi kama unashikilia huo msimamo wako. Nilitaka nikurahisishie ili kama huna uhakika na hicho unachokisema tuliachie hapo, kama unao uhakika nitataka wewe uniletee ushahidi na Waziri aniletee ushahidi na si ushahidi ule ambao umeusema hapa Mheshimiwa, kwa nini? Kwa sababu hapa nimekuongoza vizuri, hiyo sheria inachosema, nitakapokutaka ulete ushahidi siyo ushahidi wa hivyo vifungu vya sheria kwa sababu hivyo vinakukaba wewe mwenyewe.

Mheshimiwa Ole-Sendeka nakupa hiyo nafasi.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE–SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu hapa nazungumza habari ya tafsiri ya sheria na mimi siyo bingwa kwenye eneo hilo, naomba niondoe hoja hiyo katika sura hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa Katibu alikuwa amekutunzia muda wako kama nilivyoahidi, kwa hiyo sasa endelea na mchango wako. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE–SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, katika barua ya Waziri Mkuu naomba nifanye nukuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda alisema hivi, nanukuu: "Mwaka 1974, Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori ilianzishwa na kufutwa Sheria ya awali ya *Fauna Conservation,* Sura ya 302. Chini ya sheria hizo mbili masuala ya malisho na makazi hayakukatazwa katika maeneo ya pori tengefu ikiwa ni pamoja na Pori Tengefu la Loliondo. Sheria hiyo ya Hifadhi ya Wanyamapori iliendelea kutumika hadi mwaka 2009

ambapo sheria mpya ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya *The Wildlife Conservation* ya mwaka 2009 ilianzishwa na kufuta ile ya awali ya mwaka 1974." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, hiyo ni barua ya Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda alipomuandikia Mkuu wa Mkoa baada ya kuchambua hali ya mgogoro wa Loliondo na haya ndiyo maneno ambayo nimeyanukuu.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho, baada ya Waziri Mkuu kupokea maoni ya wananchi wa Loliondo alikuja na uamuzi huu. Kwanza amebainisha kwamba maoni ya wananchi kwa ujumla yanataka eneo hilo kumilikiwa na wananchi ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakitumia kuhifadhi kwa taratibu zao za kimila na desturi za jadi, lakini mwisho kabisa Waziri Mkuu alitambua hali iliyokuwepo ya wananchi kutokushirikishwa awali katika uamuzi huo.

Mheshimiwa Spika, ninalotaka kuishauri Serikali kwa sasa ni kwamba ikitaka kwenda kuanzisha mapori tengefu kwa sababu ni matakwa ya sheria kushirikisha wananchi, hakuna mwananchi wa Simanjiro aliyeshirikishwa kuanzishwa kwa pori tengefu, kinachotakiwa sasa ni waje watushirikishe ili wapate pori tengefu ambalo watamshawishi Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa kifungu cha 14 alipandishe hadhi kuwa pori la akiba. Hiyo ndiyo hoja yetu ya msingi ambayo tunazungumza na hicho ndiyo kilio cha wafugaji katika maeneo hayo niliyoyataja ambayo yameathiriwa na mapori tengefu hayo niliyoyataja.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee na hoja nyingine moja ya uagizaji wa mafuta kwa njia ya *bulk*

*procurement*. Ni jambo la busara sana kama tunataka kupunguza gharama za mafuta na kuondoa mzigo kwa wananchi, tuyaachie makampuni yote yenye nia ya kuleta mafuta nchini, kazi yetu iwe kuangalia usafi na ubora wa mafuta pale yanapoingizwa badala ya kuwa na makampuni sita au nane. Hii itasaidia kuhakikisha kwamba tunapunguza ugumu wa maisha na jambo hili halina sababu kuendelea kufichwa, tuendee tuweke uwazi kwa kuwakaribisha watu wote wenye uwezo wa kuleta mafuta.

Mheshimiwa Spika, nimwombe pia Waziri mwenye dhamana ya Nishati ya kupitia suala la vinasaba katika mafuta ambapo Wizara ilikuwa imeipatia kampuni moja uwezo wa kutosha shilingi saba kwa kila lita ya mafuta na iliingizwa kwenye *pricing template* ya mafuta na kampuni hiyo siyo kampuni nyingine ni kampuni ambayo imefanya kazi kwa zaidi ya miaka 10 ya *GFI* ikishirikiana *SICPA SA* ambayo ilikuwa ime-*tender* bei mara mbili zaidi ya washindani wenzake ambao walikuwa wameomba katika zabuni hiyo. Nakusudia baadaye kuleta hoja katika Bunge lijalo ili mambo haya yaweze kuwa wazi na kuweza kunusuru katika nchi yetu katika mzigo huu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, maana naona umeshika *microphone*.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamtaja Jesca Kishoa, atafuatiwa na Mheshimiwa Tauhida Gallos Cassian na Mheshimiwa Lusinde ajiandae.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza kabisa nianze kwa kusema kwamba suala la bajeti ni moja ya jukumu muhimu sana la Kibunge ambapo linapima uwezo wa Bunge katika kushiriki kupanga na kupitisha matumizi ya Serikali na baadaye kuhoji matumizi ya bajeti tengwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu huo ni muhimu tukajikumbusha kwamba nchi yetu imepata makusanyo makubwa kutoka kwenye sekta mbalimbali. Moja ya sekta muhimu sana ambayo nchi imekuwa ikikusanya mapato hayo makubwa ni Sekta ya Utalii. Tuna taarifa kwamba kabla ya *COVID - 19* sekta hii ilikuwa inakusanya takribani asilimia 17.9 na baada ya *COVID-19* inafanya vizuri kuelekea kufikia kiwango kilekile ambacho kilikuwepo awali.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya mchanganuo huo na mchango huo wa sekta hii kwa pato la Taifa, ni muhimu sasa Serikali na wananchi tunapaswa kujua tuna wajibu wa kulinda vya kutosha sekta hii kwa wivu mkubwa. Ni wakati muafaka nafikiri wa Serikali kuweka wazi na kuwaeleza wananchi wa Tanzania kujua vita kubwa inayoendelea kiuchumi hasa hasa kwenye sekta hii upande wa *East Africa*. Tusidanganyane hapa, kumekuwa kuna maneno mengi sana na kuna watu wamekuwa wakizungumza mambo mengi wakijinasibu kwamba wao ni wazalendo, mimi nasema hivi hakuna mahali popote katika dunia hii anakuwepo mzalendo wa Taifa lake anakuwa na *guts* za kwenda kwenye *public* na ku- *damage* nchi yake kwenye ajenda ambayo inahusiana na masuala ya kimataifa. Ni wakati wa kuwaeleza wananchi wa Tanzania ukweli, wajue ukweli ili

tuweze kushikamana sana kwenye vita hii ya kiuchumi inayoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaenda kwenye mjadala unaoendelea sasa, mjadala wa *National Cake* Ngorongoro; yanasemwa mambo mengi sana na mambo haya yanayosemwa na yana *pollute mind* za Watanzania, ni vema tukaweka mambo sawasawa hapa mezani kwangu na ukihitaji nitakupatia hapo nina ripoti ya *TAWIRI*, *TAWIRI* ni Tanzania *Wildlife Research Institute* ya mwaka 2020 ambayo inaonyesha kwamba idadi ya watu Hifadhi ya Ngorongoro kwa miaka 30 mfululizo kuanzia mwaka 1970 na kuendelea mpaka 2018 imeongezeka mara tano zaidi hii ni ripoti ya utafiti. Ukiangalia *the citizen* gazeti lilinukuu takwimu ya sensa maalum ya Ngorongoro mwaka 2017 ilikuwa ni sensa maalum kabisa kwa ajili ya *National Park* ya Ngorongoro inaonyesha idadi ya wananchi kwenye Hifadhi ya Ngorongoro ilifika 98,183 kutoka wananchi 8,000 mwaka 1959. Ukiangalia upande wa mifugo ilitoka mifugo 16,100 mpaka mifugo 805,000 kwa muda huo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa hesabu ndogo tu ambayo haihitaji *records science,* ukiangalia eneo la Ngorongoro ni kilometa za mraba 8,292 kwa mwaka 1959 uwiano wa mtu mmoja na eneo ilikuwa hivi; mtu mmoja anakaa kilometa za mraba moja lakini kufikia mwaka 2019 uwiano ukabadilika mtu mmoja anakaa kilometa za mraba 0.084 sawasawa na hivi watu 11 wanakaa kilometa za mraba moja. Hapo bado sijataja nafasi ya wanyama katika eneo hilo. Naomba niseme hivi, hesabu hazijawahi kudanganya, nimejaribu kuyasema haya yote kwanza ili kuthibitisha hoja ya msingi ya idadi ya watu kuwa kubwa kwenye hifadhi na ndiyo maana Serikali

ikaona umuhimu wa kupunguza idadi ya wananchi na wanyama katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanasiasa na wanaharakati waache kupotosha wananchi kwa kutumia kiraka cha haki za binadamu. Kwenye vita hii naomba nitangaze, naungana na Mkuu wa Nchi Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kulinda urithi wa Tanzania, naungana na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kulinda Taifa na urithi wa Taifa letu, naungana na wananchi wote wa Tanzania wanaosimama na kulinda Taifa letu na urithi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mkuu wa Nchi, Mheshimiwa Rais kwenye hili asirudi nyuma, vizazi na vizazi vitamkumbuka katika hili, hili suala limekuwa likijaribiwa kwa muda mrefu bila mafanikio. Tunahitaji rasilimali hii *I mean* tunahitaji keki hii ya Taifa ambayo Mwenyezi Mungu ametupa, inufaishe vizazi na vizazi. Pia tuambiane ukweli hivi ni wapi katika Taifa hili kimewahi kufanyika kilichofanyika kule Msimiro? Ni wapi acha Tanzania, *East Africa* ni wapi kimewahi kufanyika kilichofanyika Msimiro, leo wananchi wanahamishwa Msamiro *I think…(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Handeni.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, Handeni huko. Leo wananchi wanahamishwa unapelekwa eneo unajengewa nyumba, unakuta hospitali, unakuta shule, unapewa hati kama una wanawake watatu unapewa hati za nyumba tatu, naomba leo nitangaze rasmi mimi naitwa Ole-Kishoa ili nipelekwe kule Msamiro na mimi nikapewe nyumba ya bure kabisa. Na wanao pinga hili wanatakiwa ku-*declare interest,* tuna taarifa kuna

wabunge wengine humu ndani wanatetea haya kwa maslahi ya mashemeji zao huko, tunajua. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuna wanaosema kwamba wananchi wa Loliondo na Ngorongoro hasa hasa wananchi wa Ngorongoro kuhamishwa eneo lile ni makosa kwa sababu maeneo yale wameshayazoea. Nataka niseme jambo moja tunatengeneza *double standard* ya hali ya juu sana katika Taifa letu, kwa sababu kama hili likisikilizwa maeneo mengine watu watakapokuja kuhamishwa kwa kupisha miradi ya maendeleo watajenga *experience* ya Ngorongoro, watakataa watasema mbona Ngorongoro hawakuhama kwa sababu walikuwa wamezoea maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nina mambo manne ya kushauri; la kwanza, ni muhimu sasa Serikali ikaweka wazi ime-*target* kiwango kiasi gani cha wananchi wanaotakiwa kubaki pale katika Hifadhi ya Ngorongoro. Pili; Wizara iongezewe bajeti kwa ajili ya kuhakikisha kwamba zoezi hili linafanyika ufanisi mkubwa sana. Tatu; mbinu rafiki za kuhamisha wananchi hawa ziendelee kufanyika kwa sababu tunahitaji wananchi hawa wahamishwe kama ambavyo inafanyika sasa, wamehamishwa kwa hiari kabisa, hakuna ambaye amelazimishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho; tunahitaji kwenye yale maeneo ambayo wamepeleka vituo vya afya wapeleke Madaktari wa kutosha. Eneo ambalo wamepeleka shule wapeleke Walimu wa kutosha ili wananchi wa Ngorongoro ambao wamehamia maeneo hayo waweze kupata haki zao stahiki.

Mheshimiwa Spika, nakusihi sana kupitia Bunge lako hili Tukufu liendelee kuwasihi wananchi wa Tanzania, ni vema tukalitazama suala hili kwa sura ya kizalendo katika nchi yetu, ni vema ifike mahali tujue kwamba hakuna mtu mwenye nia ovu katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wapo watu wanaoaminishwa kwamba eneo hili kuna sijui mwarabu anataka kulichukua, yaani kuna propaganda za ovyo, watu wanatafuta kiki. Wanasiasa wanatafuta kiki. Tusiruhusu mambo haya. Najisikia vibaya sana kuona kwamba leo niko kwenye nchi ambayo kuna mwananchi *from know where* yuko nchi nyingine anamtukana Rais wa Tanzania. Hili suala haliwezi kukubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa kumalizia nigusie jambo moja linalohusiana na Jimbo la Mkalama, Singida. Nimekuwa nikisikiliza sana watu wengi sana humu ndani wakiwa wanachangia, wanazungumzia kwenye suala la miundombinu, wanazungumzia ukubwa wa barabara zao kutokuwa na lami, mtu anazungumzia kilomita mbili, mwingine anazungumzia kilomita tatu na mwingine anazungumzia kilomita tano.

Mheshimiwa Spika, kuna Wilaya moja Mkalama ipo Singida kule pacha na Wilaya ya Mheshimiwa Waziri alikotoka, Wilaya ya Iramba. Hii Wilaya ya Mkalama kuna kilomita zaidi ya 42 kutoka barabara kuu mpaka kufika Halmashauri. Barabara ni ya vumbi, barabara ni *rough road,* ni mbaya, madaraja hayafai, hayapitiki mvua ikinyesha. Wananchi wa kule wanajishughulisha sana na suala la kilimo cha vitunguu. Ikifika wakati wa mavuno wanapata taabu sana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, namwomba kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, kama kuna jambo ataliacha kuwa na alama kwenye Wilaya ya Mkalama ambalo ni pacha na Jimbo lako la Iramba, fanya jambo kwa ajili ya Wilaya hii Mheshimiwa Waziri. Inasikitisha sana kuona kwamba Iramba... *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Kengele imeshagonga, nani amesimama? Mheshimiwa Francis nikukupa taarifa maana yake na yeye nimpe nafasi tena. Muda wa mchango wake umekwisha na amegongewa kengele. Ahsante sana.

Waheshimiwa nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, atafuatiwa na Mheshimiwa Livingstone Lusinde, kama muda utaruhusu tutamalizia na Mheshimiwa Robert Maboto.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia bajeti yetu. Kwa namna ya kipekee nampongeza Waziri na Naibu Waziri na Mawaziri wote kwa kutuletea bajeti ambayo ni bora na nzuri, yenye majibu na matumaini kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaanza na *Royal Tour*. Tumshukuru kwa namna ya kipekee Mheshimiwa Rais wetu wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kutangaza utalii wa Tanzania. Hizi kelele zote tunazoziona zinazohusisha Longido, Ngorongoro ni matokeo na jibu la *Royal Tour*. Tunamshukuru kwa namna ya kipekee Mheshimiwa Rais wetu ameifungua Tanzania. Kila kona na

kila milango ya Tanzania iko wazi. Tuna matumaini makubwa kuona kwamba Tanzania inaenda kufunguka.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru *Royal Tour* kwa matokeo makubwa yanayoenda kutokea. Utalii wetu unaenda kugusa vijana na wanawake wa Tanzania. Hii itaenda kuongeza vipato vyao na kuendelea kuongeza shughuli walizokuwa nazo. Tulitegemea kuona Watanzania, hususan Wabunge wanaowakilisha Watanzania, ambapo sisi tuliokuwemo humu ni wachache ambapo wengine hawakupata fursa ya kuwepo hapa. Pale kwenye masuala ya Kitaifa kuona kwamba tunaunga mkono Serikali yetu na kuunga mkono jitihada za Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa ambayo sijawahi kuifanya, nampongeza Ndugu yangu Mheshimiwa Kishoa kwa uzalendo wake aliyouonesha hapa. Kwenye suala la Kitaifa lazima Watanzania tuwe wamoja. Kwenye suala la maslahi ya wananchi, lazima Watanzania tuwe wamoja. Tukiungana kwa namna hii, hii ndiyo siasa inayotakiwa kuwa nayo ndani ya Tanzania. Hii ndiyo siasa tuliyoitegemea kwa miaka mingi kuiona ndani ya Tanzania. Suala la maslahi ya nchi, lazima tuungane na tuwe wamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitegemea kuona Wabunge wote tukiunga mkono jitihada za Mheshimiwa Rais. *Royal Tour* inaenda kukuza uchumi wetu, inaenda kupandisha kipato cha Watanzania. Sikutegemea kuona vikwazo. Vikwazo venyewe inabidi sasa tuwaambie Watanzania, ni vikwazo ambavyo watu wa nje wanatutumia baadhi yetu wanasiasa, wafanyabiashara na mbaya zaidi wanawatumia wananchi waliokuwemo ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tumesimama hapa tuseme kwamba tuko pamoja na Mheshimiwa Rais wetu. Kwenye hili hatuna mjadala na mtu. Kwenye hili hatutamung'unya maneno.

Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa, lengo na dhamira ni moja tu, kukuza kipato cha Watanzania. Lengo ni moja tu, kukuza uchumi wa Tanzania. Kwenye hili, haturudi nyuma na hatutamwangalia mtu usoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matamanio yetu na matarajio yetu, mambo mazuri anayoeleza Waziri Mkuu kwenye mikakati ya kupunguza watu kwenye maeneo haya, Watanzania wote wakiwa wamesikia, tulitegemea kuona wameunga mkono. Hili kwetu limekuwa ni fumbo, lakini tunasema wa kulifumbua ni sisi Wabunge. Jibu letu ni moja, tuko pamoja na Mheshimiwa Rais wetu. Tanzania kwanza, wananchi wa Tanzania kwanza, mengine yatafuata baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti yetu ina mambo mengi, Serikali yetu ina mambo na mambo wanayotupangia ni mazuri. Kuna suala la wanafunzi wa *Form Five* na *Form Six* sasa kusoma bure. Kama ni Mtanzania mzalendo lazima afikirie kwamba ndani ya nchi hii ya Tanzania kuna wanafunzi walikuwa wanafaulu lakini wanashindwa kwenda kusoma kwa sababu ya vipato vya chini walivyokuwa navyo ndani ya familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Rais amesema watoto hawa wasome bure, sisi ni nani wa kutokumpongeza Rais kufanya jambo zuri kama hili? Tuchukue fursa hii tumpongeze Mheshimiwa Rais kwa bajeti ya mfano iliyomjali mnyonge, iliyomgusa mtu wa chini. Hakuna mtu wa juu aliyeshindwa kusomesha mtoto wake. Waliokuwepo juu wengi wao watoto wao wanasoma ma-*private* toka Darasa la Kwanza mpaka wanamaliza wanalipia fedha. Mnyonge aliyekuwepo chini, kijijini mtoto wake anafaulu.

Mheshimiwa Spika, juzi tuliona mfano, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma alimtoa mtoto kashindwa kusoma kaenda kufanya kazi, lakini akamwambia acha, njoo usome. Wako wangapi kama wale? Wanahitaji msaada;

Mheshimiwa Rais amesikia, ameona, naye ni mama mlezi, tunamshukuru. Hatuna maneno makubwa ya kumpa zaidi ya ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuje kwenye suala la Shirika la Bima, Shirika letu la Taifa. Hili Shirika likionekana kwa undani ni kama limesuasua, sidhani kama lina fedha ya kutosha ya kuweza kufanya kazi, kuingia kwenye ushindani uliyokuwepo. Lazima Shirika hili liongezewe fedha liweze kuingia kwenye ushindani. Haiwezekani tunakuwa na Shirika ambalo unaliona; tatizo siyo watu waliyokuwepo pale, tatizo fedha za kuwawezesha watu kufanya kazi vizuri. Lazima Shirika liwe na fedha ya kutosha liweze kufanya kazi zake vizuri. Namwomba Mheshimiwa Waziri, nalo hili liingie kwenye suala la fedha ili liweze kupata ushindani mzuri kuweza kufanya majukumu yake vizuri

Mheshimiwa Spika, vilevile naishauri Serikali, Shirika la Zanzibar la Bima linafanya kazi mpaka Tanzania Bara, basi nami niseme angalieni sheria, mikakati, utaratibu, nalo pia liwe na uwezo wa kufanya kazi Zanzibar. Tanzania ni moja na Watanzania ni wamoja.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye asilimia 10 za wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum. Kwenye hili, naishauri Serikali yangu, hapa tupaache kama palivyo. Tunaposema tuchukue asilimia tano tuipeleke kwa Wamachinga, hili suala halijakaa vizuri. Ili likae vizuri, hawa watu tunaowazungumza, Wmachinga wanapatikana kwenye kundi la wanawake. Mheshimiwa Waziri wa Fedha utusikilize kwenye hili.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Spika, hawa wanapatikana kwenye kundi la wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum. Huu mfuko haujawazuia wao

kutokufanya kazi, hawajazuiliwa na wao kuingia kwenye mikopo kwa mfumo uliyokuwepo. Hebu Mheshimiwa Waziri pata muda ufuatilie huu mfuko, unafanya kazi vizuri? Kuna Halmashauri imelimbikiza fedha chungu mzima zipo, wanawake hawapatiwi mkopo, vijana hawapatiwi mikopo, sasa tunaposema tunanyofoa asilimia tano, zinabaki asilimia tano, wakati hata hizo zilizokuwepo watendaji wetu wanatuangusha, hawazifanyii kazi ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza tuangalie mifumo vizuri, tuangalie utekelezaji wake kama uko vizuri ndipo tuone tunakuja na maamuzi gani? Kwa sasa ni mapema mno na tumefanya haraka. Turudi tuache mfuko ulipo. Mheshimiwa Rais amesema zitakwenda Shilingi milioni kumi kumi, atapeleka. Vilevile kwenye bajeti yako ukurasa wa 69 imeonesha kuna Shilingi bilioni 45 ambapo zitakwenda Shilingi bilioni moja moja kila Mkoa. Nadhani bado kuna fursa na namna ya kuangalia, ile asilimia 10 iachwe kama ilivyo, iwasaidie wanawake na vijana wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii tena kuishukuru Serikali yangu kwa kutenga fedha katika bajeti kwa ajili ya vifaa tiba. Waaguzaji ni wanawake. Baba leo akiumwa muugazaji ni mwanamke, mtoto akiumwa muugazaji ni mwanamke. Tunapoona vifaa tiba vimepatikana, tunasema ahsante na tunaishukuru Serikali yetu, inatuangalia kwa jicho la kipekee, inatuangalia kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakwenda kumalizia. Kuna migogoro, wananchi wetu wanatuletea malalamiko. Mheshimiwa Waziri aangalie, kuna migogoro ya mabenki, hususan kwa wawekezaji wazalendo. Waangalieni, kweli!

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa muda wa kuchangia hoja ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, naomba kwenye Bunge hili tumtangaze Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu kuwa Spika wa viwango vinavyozingatia kanuni, sheria na utaratibu wa kuliendesha Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anaiongoza nchi yetu kwa ufanisi mkubwa. Nataka niseme bila kuficha, nimekuwa Mbunge hapa mwaka wa 12, nimesikia bajeti nyingi hapa, lakini bajeti ya mwaka huu Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba ameitendea haki kwa kuisoma, kuihusianisha kabisa na Mkuu wa Nchi, kwamba yeye ametumwa tu kuja kufanya, lakini mwenye kazi ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naweza kusema bila kuficha, ni bajeti pekee ambayo imemtaja Mheshimiwa Rais kwa wingi sana kuliko bajeti zote zilizosomwa na Mawaziri hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya mambo tuyazungumze katika ukubwa na upana. Hapa tunazungumzia Mfuko Mkuu wa Serikali, tunazungumzia namna gani tutaishauri Serikali kwanza kukusanya mapato yaingie kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali halafu baadaye namna ambavyo tutanufaika nayo kwenye Majimbo na Watanzania namna gani watafaidi baada ya kuwa yamekusanywa.

Mheshimiwa Spika, sasa tunapozungumzia vyanzo vya mapato, tuwe wakweli, tunahitaji kuishauri Serikali kukusanya kodi kwa uhakika, lakini vilevile kuwa na nidhamu ya kutunza fedha zinapoingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali ili kesho na keshokutwa zije zirudi tena kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Spika, niseme, viongozi wengi sana wa Afrika kumbe wakati mwingine huwa wanabadilishwa na watu. Nasema hivi kwa sababu Mheshimiwa Samia tunayemsifu leo kuwa mpole na mtulivu, sina hakika tukiendelea na tabia hii kama itafika 2030 akiwa hivyo. Tunaweza tukajikuta sisi wenyewe tumembadilisha. Rais anaweza kuwa mpole, mtulivu anayefuata sheria lakini vitendo vya baadhi yetu vikambadili akawa mkali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania tumeshuhudia watu wakihama baadhi ya maeneo. Tumeshuhudia ndugu zangu Wasukuma, wafugaji wakihamishwa kutoka bonde la maji pale kuelekea Mtwara, wote tulikuwepo na ni watu wazima; watu walikufa katika safari ile na mifugo ilikufa. Mtu alimnunulia mwanaye raba mpya za kutembelea, lakini baada ya kufika Tunduru zilikuwa zimechanika, zimechakaa na miguu imetoboka, anatembea kijana kutoka Mbeya kwenda Tunduru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo Rais anahamisha watu kwa mabasi, ng'ombe wanapanda malori, bado tusiseme jamani tuna Rais mwenye huruma na anayependa watu? Haiwezekani. Rais hili jambo amefanya ni la kibinaadam la kiutu sana. Hakuna katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania watu walioweza kuhama kwa raha kama watu wanaohamishwa kutoka Ngorongoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi tukubaliane, hapa kwenye jengo la Bunge ikilipuka volcano, kuna Mbunge anabaki hapa? Ikitokea hatari hapa wote tunatoka; huwezi sheria ilisema hapa ndiyo jengo la Bunge, hakuna! Siku moja king'ora kililia

tu hapa, Waziri Mkuu alikuwa ndio wa kwanza kutoka hapa anakimbia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tukubaliane kwamba tunataka mapato yaongezeke kwenye mfuko wa nchi. Haya mapato mengine yanatoka kwenye utalii, mengine yanatoka kwenye kilimo. Kwa hiyo, ni lazima tukubali tunapotaka kuboresha utalii, tunaboresha mapato yaongeze kwenye mfuko wa Taifa. Kumbe Rais anaongoza Taifa hili kutoka wapi hizo fedha? Tunapotaka maendeleo, huku tunasema Rais asikope, huku tunasema watalii wasije, sasa huyu Rais ataongoza Taifa kutoka wapi? Fedha atazitoa wapi?

Mheshimiwa Spika, fedha nyingine ni za utalii, lazima watalii waje kwenye nchi yetu. Tumeona pale Wabunge wengi sana wametembelea China. Umeona kwenye *great wall* pale, Mchina hataki mtu asogee pale! Bahati mbaya sana nchi hatuwezi kuiongeza ukubwa. Nchi yetu ndiyo hii hii tumepewa, upande huu tunapakana na Msumbiji, huku Kenya, huwezi kuiongeza ukubwa. Kwa hiyo, lazima rasilimali tuliyonayo, hiyo hiyo itutoshe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upendeleo mwingine uliotoka hata nyumbani kwako pale unapoishi, mimi nimefika, wewe unakaa sehemu ina heka moja ile! Ila watu waliohamishwa Ngorongoro wamepewa heka tatu, wakati wewe unakaa pale padogo kabisa! Watu wamepewa heka tatu. Ardhi ya heka tatu siyo ndogo mabwana. Kwa hiyo, tumsaidie Mheshimiwa Rais kwenye baadhi ya mambo, tumsaidie kuwashauri wale ambao hawaelewi, jamani eeh, maeneo haya ni hatarishi. Hapa tunataka kuimarisha utalii, watu waondoke kwa hiyari, sisi tusiwe vikwazo. Tunaoelewa tusiwe vikwazo, tuwaelimishe watu wetu namna gani ya kuweza kukubali ili Serikali iongeze mapato. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuna mambo yamezungumzwa hapa na Wabunge wameyazungumza kwa ufasaha sana kuhusu kuipongeza Serikali. Mimi naipongeza sana Serikali.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lusinde, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mtaturu.

**T A A R I F A**

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba migodi yote ambayo unaiona inachimbwa madini nchi hii ni maeneo ambayo walikuwa wanaishi watu. Leo walipopewa leseni zikatolewa na Serikali, watu wale walihamishwa kwa mujibu wa Sheria Na. 5 na Na. 6 ya mwaka 1999. Kwa hiyo, hata kinachofanyika Ngorongoro ni kufuatana na Sheria hiyo ya Ardhi ambayo inasema kwa mujibu wa Sheria. Kwa hiyo, naomba nimwongezee taarifa hiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Lusinde, unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, naipokea kwa mikono miwili.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

Mheshimiwa Spika…

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam, huwa mtu hawezi kupokea kabla hujaka hapo, lazima achangie kwanza halafu ndio umpe taarifa. Maana sasa utakuwa unampa taarifa yule aliyekaa kule, utakuwa haumpi mwenye muda wake.

Ahsante sana, Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Halafu mimi leo nilikuwa nimejiandaa kuhutubia nchi, kwa hiyo, akina Mheshimiwa Tabasam hebu watulie kidogo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa hapa suala la Wamachinga. Naishauri Serikali, tufanye utafiti. Hivi tunashindwa kufanya utafiti Wamachinga wetu wa Tanzania wanataka nini? Hebu tujipe muda wa kwenda kufanya utafiti, kuongea nao, Wamachinga wanachotaka pengine siyo kile ambacho sisi tunafanya. Wamachinga wanataka kukaa maeneo yenye mlundikano mwingi wa watu ili waweze kuuza biashara zao. Machinga hawahitaji jengo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wamachinga unaweza kuwajengea jengo nzuri na bado lisiwasaidie. Wanataka kukaa maeneo yenye watu wengi ili waweze kufanya biashara. Wamachinga hawahitaji vitu vingi ambavyo sisi tunafikiria.

Mheshimiwa Spika, lingine limezungumzwa hapa juu ya asilimia 10. Nilikuwa nataka Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakaposimama anisaidie kidogo. Hivi alipokuwa anasema kipindi kile cha Mpango kwamba lengo la Serikali ni kuzalisha mabilionea wengi, ndiyo kwa hii asilimia tano au kuna mpango mwingine unakuja? Maana unapataje mabilionea wengi kwa utaratibu huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, tuone ni namna gani tutahamasisha kilimo. Ndugu zangu Wizara ya Kilimo imefanya kazi kubwa sana, watu wanalima sana, lakini Benki yetu ya Kilimo ni ngumu kukopa. Wakulima hawawezi kukopa. Hebu siku moja waite watu wa Benki ya Kilimo waje waeleze, utashangaa hawana mkulima hata mmoja wamemkopesha. Tulipeka wakulima wa zabibu 15 kutoka Mvumi wakawapokea, wakawapa maelezo mengi, lakini mwisho wa siku hawakupata hata senti tano. Kukopa kwenye Benki ya Kilimo ni ngumu, haiwezekani. Fedha wanazo,

wanataja mabilioni lakini hakuna wanayemkopesha hata mtu mmoja. Hii Benki ni ya namna gani? Yaani bora mtu akakope *CRDB* atakopa alime lakini Benki ya Kilimo tuitake kila mwaka ituletee orodha ya majina ya wakulima waliokopa. Benki ina masharti magumu, haiwezi kumkopesha mtu wala kumsaidia mtu, lakini inaitwa Benki ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna Taasisi zina majina mazuri lakini hazimsaidii mtu, mtu wa chini imekuwa ngumu kukopa. Kwa hiyo, naomba sana Benki ya Kilimo tujipange vizuri, ushirika uimarishwe ili wakulima wawe na masoko. Tuwe na bei elekezi kwenye kila zao. Zabibu tuweke bei elekezi, korosho tuweke bei elekezi, tukija kwenye ufuta tuweke bei elekezi, tukija kwenye alizeti tuweke bei elekezi ili wakulima wetu wasipunjwe na kudhulimiwa.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Antony Mtaka, ameelekeza vizuri namna nzuri ya kubana matumizi kwa wazazi wanaopeleka watoto wao kwenye Kidato cha Tano na cha Sita ili msamaha wa ada uliotolewa na Rais uweze kuwafaa watoto wetu. Vinginevyo mwakani tutaiomba Serikali irudishe ada, lakini iondoe michango, maana tunaona kwenye michango sasa ndiyo kuna tatizo kubwa kuliko kwenye ada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa sehemu ya kwanza ya kipindi chetu kwa leo. Niwatangaze Wabunge wachache watakaonza kuchangia mchana. Pia nimepokea ushauri kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba wale wanaotajwa kwa ajili ya mchana basi wawe wanaanza wao kwa sababu wananchi wao wanakuwa wanawasubiria kuwasikia, kwa sababu wakitajwa hapa halafu wakaja kuwekwa mwishoni wananchi wanakuwa

hawaelewi, sasa Mbunge wetu vipi tena? Au hajatokeza Bungeni?

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge nawaomba wale wanaotajwa mwanzoni pia tuwahi kufika kwa sababu utakapoitwa ni muhimu uwepo kama mlivyotoa ushauri ninyi wenyewe.

Tunao hapa Waheshimiwa Wabunge wengi, lakini nitawataja wachache kama nilivyosema. Yupo Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mheshimiwa Samweli Hhayuma, Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao na wengine tutaendelea kuwataja kadri utakavyokuwa unakwenda.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni Leo.

*(Saa 7.02 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.  Katibu!

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Hoja za Serikali.

**20 JUNI, 2022**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Tutaanza na Mheshimiwa Ali Mlaghila Jumbe atafuatiwa na Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu ajiandae.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, timu bora sana duniani zinazocheza mpira zina mifumo ya uchezaji mpira na mfumo mmojawapo ni 4-4-2 lakini ipo na mifumo mingine ambayo wanaibadilisha inakuwa 4-3-3 na sisi katika kujenga vijana wetu, wakina mama pamoja na walemavu tulichagua mfumo bora kabisa ambao unashinda mfumo wa 4-4-2. Mimi leo nataka nishangae wakati tunataka kushinda tunaletewa mfumo wa *5-2-2-1* mfumo huu ni wa *ku-defend* haujawahi kushinda hata siku moja. Maana yake ni kwamba, nasema hivi turudi kwenye mfumo wetu ambao umekuwa ukitushindia ambao umekifanya Chama cha Mapinduzi kiweze kushinda, ambao tuliwaahidi wananchi wetu kwamba tutafanya hivi ili waweze kushinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kusema hivi asilimia 10 ninataka nilishawishi Bunge ibaki kama ilivyo, lakini tunasema asilimia tano iende eti ikajenge miundombinu, miundombinu ipi? Miundombinu ambayo tunataka

kuijenga haijatolewa ufafanuzi, lakini hata tukijenga miundombinu hivi ni lini mmachinga yaani huyu mmachinga ambaye tunamuangalia akafanya biashara ya kukaa badala ya kwenda kutembea kuuza bidhaa zake? Mimi nasema hapana, hili tuliangalie vizuri.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kazi nzuri inayofanywa na Waziri wetu, kwa kuhakikisha sasa hivi tunapata fedha za kulipa elimu bure kuanzia shule ya awali mpaka Kidato cha Sita. Hivi tunapofanya haya tumewafikiria watoto wa kike ambao tunataka kesho wawe wakina Mama Samia, kesho wawe wakina Tulia, kesho wawe wakina Mama Abdallah tumewafikiria ni watoto wangapi hawaendi shule kwa kukosa taulo zao za kike? Mimi nilitaka nilishawishi Bunge hili kwamba tuoneshe mfano, kwa mara ya kwanza tusimchoshe mama yetu Samia Suluhu Hassan hebu twende tuongeze katika hii asilimia 10 hata iwe asilimia 12 au asilimia 11. Asilimia moja itolewe ruzuku kila shule watoto wa kike wapate mataulo ya kike.

Mheshimiwa Spika, yaliyopo huko vijijini ni mengi unajua sisi hapa Wabunge wako tunaongea mambo yaliyoko *site* hatuongei mambo yaliyoko Mjini, huko *site* watoto wa kike hawaendi shule wengine wanafikia hatua ya kuweka mawe kwa sababu wamekosa fedha. Kwa hiyo, ninaomba hili lifanyiwe kazi na Wizara yetu ninajua ni sikivu inataka Bunge hili litoke na vitu vipya kama inavyofanya sasa. Nashukuru sana kwa usikivu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapoongelea mambo ya *site* ni mengi sana katika vitu ambavyo ni muhimu kwa nchi yetu pia ni viongozi wetu. Usalama wa viongozi wetu ni kitu

muhimu sana, lakini tunapozungumza usalama wa viongozi wetu kuna sehemu ambapo wananchi wetu tunawakwaza. Kiongozi wetu anaposafiri au anapita sehemu utakuta atapita Saa Tano, lakini magari yanaanza kufungiwa kuanzia saa 12 asubuhi! Hili halikubaliki katika teknolojia ya sasa, hivi ni nani amewahi kufanya utafiti wa madhara yanayotokea? Kwa mfano, mtu alikuwa anakwenda Mahakamani halafu akafungiwa mnajua ni watu wangapi ambao wameshindwa kufika Mahakamani? Mimi ninaomba tutumie njia rahisi sana, kuna mambo mengi viongozi wetu wanaweza wakaenda kwa helikopta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa majuzi Mheshimiwa Nape alikwenda kwa helikopta *well done*! lakini viongozi wetu sisi tunao uwezo wa kufanya TEHAMA nzuri kabisa na sasa hivi kwenye mitandao tunao uwezo wa kufikia, kwa nini hazitolewi taarifa kwamba leo barabara fulani na barabara fulani hazitapitika, ili kama mtu unawahi basi mtu uanze saa 10 uwahi sehemu unayokwenda ili ikiwezekana hata wale ambao wanataka kusafiri wajiandae.

Mheshimiwa Spika, katika uchumi tunaokwenda nao, uchumi huu tunaoujenga muda ni kitu muhimu sana tusiuchezee muda. Hapa majuzi mimi nimeshuhudia tumesimamishwa *round about* hapo tunakuja Bungeni, tumekaa dakika 40 halafu hakuna kiongozi aliyepita magari yakaruhusiwa kweli hii ni haki? Hii siyo nchi ya kujenga uchumi ambao ni wa blabla! tujenge uchumi uliokamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mazuri sana yaliyopo kwenye bajeti hii, pamoja na hotuba nzuri sana,

lakini kuna suala la pendekezo la kufuta baadhi ya vifungu vinavyoiwezesha *TCRA* kusimamia baadhi ya huduma na miundombinu. Hivi kwa nini *tuna-rush* sana kwenda huko kitu gani kinachotukimbiza mpaka tukahangaike na kubadilisha kanuni sasa? Hata ambao tunasimamia Wizara hiyo hata hatujui hivi vifungu *vina-conflict* gani, vina faida gani na wala hatujui ni sababu gani ambazo zinatupelekea twende tuvibadilishe. Kazi kubwa ya *TBS* ni *ku-formulate,* mimi nilidhani sasa hivi tunatakiwa tuiwezeshe *TBS* ilete viwango vya ujenzi wa nyumba zetu. Sasa hivi tunatumia viwango vya watu wa Ulaya, kwa mfano *standard temperature* ni 20 je, Tanzania *standard temperature* ni 20? Hivi utafiti umefanyika? ndiyo kazi ya *TBS! TBS* kuna sehemu tumewahi kufeli, tuliwapa wakague magari Japan hivi hilo limefika wapi? Matokeo yake Serikali imepata hasara sasa. Mimi ningeomba tusikimbilie huko Mheshimiwa Waziri, tuende tufanye mijadala ya kina na kuangalia kwa kina zaidi kuna mambo mengi. Haya mambo tunayokwenda kuyafuta ni *globally harmonized,* ni mambo ya Kimataifa. Wizara yetu ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeingia mikataba ya Kimataifa kwa ajili ya kusimamia haya. Mimi ningeomba hili tuachane nalo tulifanyie utafiti wa kina ili lilete tija kwa nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la kubana matumizi limeongelewa sana hapa, mimi nitakuwa kinyume sana na kubana matumizi mpaka kufikia eti vikao na semina vifanyike kwa sinema Hapana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu uchumi wake unategemea fedha za Serikali na jinsi tunavyokula maisha ndivyo mzunguko wa fedha unavyozunguka kuwafikia

kila mtu. Tukisema tubane hilo Wakurugenzi wakae huko eti aje huku hatutafika popote. Haya mahoteli tunayojenga sasa hivi ambayo ndiyo uchumi lakini uchumi wa Dodoma utakufa, wanaoleta fedha ni hao ambao tunataka tuwabanie tuwaangalie kwa sinema. Lakini *exposure* tu *DED* akitoka huko anakutana na mwenzie, akifika hapa anabadilishana mawazo, anakuwa na mawazo mapya lakini pia *ana-refresh*. Mimi nataka kusema mlowee kwa kubana matumizi ya kuangalia semina kwenye ving'amuzi hapana, tusifike huko, tunaharibu nchi! acha watu wale maisha wapate fedha Mama amefungua zipu. Jambo kubwa hapa tumsaidie Waziri atafute vyanzo vizuri vya mapato na kuna wakati waliwahi kusema uchumi tunao lakini tumeukalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru ulituruhusu Kamati yetu tukaiangalie barabara bora kabisa inayotoka Njombe kwenda Ludewa mpaka Manda kilomita zaidi ya 200 inayojengwa kwa zege. Barabara ile tukifikia hatua ya kwamba tunataka tuache kubana matumizi watu wale maisha nataka niseme ile barabara acha tuimalizie sasa. Ile barabara ikifika Manda itaunganisha na Itungi *Port* ambapo meli zikibeba makaa yatafika pale Itungi *Port* mpaka Manda. Manda yatabebwa kwa magari kwa barabara bora nzuri sana kabisa, lakini kule ndiko Mchuchuma na Liganga iliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini leo hii tuache kuvuna yale makaa sasa, ndiyo uchumi ambao tunasema hebu tuende tujielekeze huko, tutafute vyanzo vizuri vya uchumi tuache haya mambo ya kubana bana matumizi madogo madogo haya ambayo hayana maana kwa

kweli. Fedha yetu tunayohitaji ni kubwa matumizi tunayobana ni kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la kilimo tumefanya kazi nzuri sana na Waziri amefanya kazi nzuri sana, lakini tunakwenda kutoa zaidi ya Bilioni 900 Je, tumewaangalia Maafisa kilimo waliopo huko wanafanya kazi gani? Hivi ninavyosema inawezekana tunakwenda kutoa ruzuku kwenye mbolea lakini hata idadi *(database)* ya wakulima hapa hatuna! Ni sababu gani? hatujawaangalia Maafisa Kilimo waliopo mimi nataka kusema tuweke maafisa kilimo walio bora ili waweze hata kusimamia haya tunayoyasema yaweze kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe mfano mwingine, kuna suala la kilimo cha umwagiliaji hapa tumezungumza lakini kuna mradi mkubwa ambao siuoni popote. Wizara ya Mambo ya Nje siuoni, Wizara ya Fedha siuoni, Wizara ya Kilimo siuoni, Wizara ya Maji siuoni ni ule wa Songwe *River Basin* ambao unakwenda kufanya kazi kubwa. Nataka niseme Mheshimiwa Waziri hebu liangalie hili ni *Dola* Milioni 577 zinahitajika, ili watu wa Kyela walime mpunga kwa kumwagilia ili kule kuwepo na mambo ya umwagiliaji mazuri.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii, naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga ajiandae.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kwa kuja na bajeti nzuri, nimshukuru Mheshimiwa Rais wetu mama yetu Samia kwa kuweza kuruhusu kuanzisha dirisha maalum kupitia *TASAF* itakayosaidia watoto wanaotokea familia maskini. Watoto wengi wanaotoka katika familia maskini wamekuwa wakifaulu vizuri sana na kupangiwa mbali na kushindwa kumudu gharama. Kwa hiyo, kupitia mpango huu kutawasaidia hawa vijana wetu waweze kutimiza ndoto zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee na mchango wangu katika hoja yetu hii katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika eneo la mazingira ya biashara ndogo ndogo na sekta binafsi, ameelekeza kwamba wataitoa asilimia tano iende ikatengeneze miundombinu pamoja na masoko kwa ajili ya wamachinga. Naomba Serikali iahirishe kwanza hili jambo kwa sababu mazingira katika maeneo yetu yanatofautiana. Hivyo ikafanye tathmini pamoja na kuangalia fursa zilizopo katika maeneo yetu ili waone kama tunauhitaji wa kujengewa yale masoko na miundombinu ya Wamachinga vinginevyo miundombinu hii itakwenda kukaa bila kuleta tija yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema kwamba toka tupitishe sheria yetu mwaka 2018 Wakurugenzi wamekuwa wakichangia kwa kasi asilimia 10 katika makundi yaliyotajwa katika sheria hii na kuleta tija, katika kuinua wananchi wetu vijana wetu na wakina mama kiuchumi, tutakapowaondolea asilimia tano tutaendelea kuwadidimiza. Pamoja na Serikali ilitoa maelekezo

kwamba mifuko yote ya uwezeshaji kiuchumi iweze kuunganishwa Pamoja, iweze kuhudumia vijana, lakini mpaka leo katika Wilaya ya Meatu hatujawahi kupata mfuko wowote kwenye hiyo mifuko ya uwezeshaji kiuchumi. Kwa hiyo, tutakapopunguza hii asilimia tano tutaendelea kuwapunguzia uwezo wa kujijenga kiuchumi vijana wetu na wakina mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mazingira ya Meatu hayaruhusu kuwa na miundombinu ya kimachinga kwa sababu ya vikundi vinavyojishughulisha na shughuli tofauti ambazo hazihitaji miundombinu hii. Shughuli hizi ni kilimo cha vitunguu, kilimo cha ufugaji ng'ombe, ambao soko lao ni kupeleka minadani tayari soko lipo, kwa ajili ya ile mifugo na mingine inasafirishwa kwenda Dar es Salaam tena inaleta matokeo kwa haraka. Kama asilimia tano itatumika kujenga miundombinu wa wamachinga pale, sioni mwananchi anayetoka Mwasengera kilomita 120 kuja pale makao Makuu ya Wilaya atanufaikaje na hiyo miundombinu. Kwa hiyo, miundombinu hii itakaa *idle* bila kuleta tija yoyote kwa vijana wetu, labda nimuombe tu Mheshimiwa Waziri aongeze ifikie hata asilimia tano ziwe 15 ili ziweze kunufaisha na kuziba zile pengo la mifuko ya kiuwezeshaji kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika maoni ya Kamati ya Bajeti iliongelea kwamba kilimo ni moja ya sekta ambazo ni nguzo kuu ya maendeleo ya viwanda kwa sababu ndio malighafi zinazopatikana. Mimi naunga mkono maoni ya Kamati kwa sababu zifuatazo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali iwekeze zaidi katika mazao ambayo inayaona ni malighafi kwa ajili ya viwanda vyetu. Kwa mfano, Kamati ilitembelea Kiwanda

cha Nguo cha *NIDA* kiwanda kile kilionekana kinaupungufu mkubwa wa malighafi ambayo ni pamba, pia Serikali inataka kufufua viwanda vingi vya *ginnery* kikiwemo kiwanda cha *solar*, hata viwanda vilivyopo havina malighafi ya kutosha kwa sababu msimu wao unakwenda miezi mitatu tu ile pamba inakuwa imekwisha. Zao hili pamoja na mazuri yaliyofanywa na Serikali mimi nimshukuru Rais kwa miaka miwili mfululizo, bei ya pamba imepanda juu maradufu kuliko miaka ya nyuma ilivyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kusamehe madeni ya pembejeo kwa ajili ya wakulima wa pamba. Nimshukuru kwa sababu, zao hili limekuwa na changamoto nyingi sana kuanzia pembejeo ya kuua wadudu pamoja na mbegu. Pamoja na ukame ulioikumba nchi yetu ikiwemo Wilaya ya Meatu wakulima walipanda mbegu ya pamba lakini hazikuweza kuota kutokana na ukosefu wa mvua, walipotaka kurudishia mbegu zingine walikosa kwa sababu hakukuwa na mbegu zilizokaribu kwa ajili ya kupanda mbegu nyingine. Hii ni kutokana na kiwanda cha kuzalisha mbegu kiko Mkoa wa Katavi, lakini pamoja na kuwa Serikali imeweka ruzuku kwa ajili ya pembejeo bado kuna gharama kubwa ya kusafirisha mbegu hizo kuzitoa Katavi mpaka kuzileta Simiyu. Ninaiomba Serikali ifanye inavyoweza ili wananchi wasiwe na changamoto ya ukosefu wa pembejeo ya mbegu kwa ajili ya viwanda tunavyovifufua pamoja na viwanda vya nyuzi na viwanda vya ushonaji nguo *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa nyingine iko kwenye dawa za kuua vidudu. Mheshimiwa Rais akiwa Makamu wa Rais alipokuja Mkoa wa Simiyu alitoa

maelekezo wataalam wetu wajikite kutengeneza dawa ambayo itauwa vidudu, lakini mpaka leo Mheshimiwa Samia akiwa Rais bado wakulima wa pamba wanaletewa dawa za kuua wadudu ambazo haziui wadudu, zinafifisha tu. Ukimwagia wadudu ndio wanashamiri, ukimwagia ndio matunda yanaanguka chini, lakini sasa ni afadhali ambao hawakumwagilia angalau wameweza kuvuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali yetu inapoongea kwamba, uzalishaji wa pamba unaenda kuongezeka mara dufu msimu huu, sikubaliani nao, kuweza kulichukua lile kijumlajumla, waangalie maeneo ambayo zao litaongezeka mara dufu, lakini waangalie maeneo ambayo yana changamoto ili waweze ku-*deal* na changamoto zilizojitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kushukuru pia pamoja na upungufu uliopo katika *AMCOS* zetu na kwamba, utaratibu wa ununuzi maeneo mengine unataka kubadilishwa, lakini *AMCOS* imefanya kazi kubwa. Mkulima miaka yote amekuwa akipunjwa kilo yake ya pamba, lakini toka *AMCOS* zianze wakulima hawalii kuhusu kupunjwa mizani kwenye zao la pamba. Hata kama watabadili utaratibu, lakini waendelee kulinda mkulima asiendelee kupunjwa katika mizani ya pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, atafuatiwa na Mheshimiwa Abubakar Damian

Assenga. Mheshimiwa Mhandisi Samuel Hayuma ajiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo ili kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka 2022/2023. Kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita ya Chama cha Mapinduzi chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha Dkt. Mwigulu, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii kwa namna ambavyo wamekuja na bajeti inayolenga kutatua kero za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wapo waliojadili kutaka kuifanya hii bajeti isionekane kama ni ya kulenga kero za wananchi, lakini nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Serikali, hawajafikia viwango vya bajeti hii. Hawajaonesha vyanzo mbadala, wanaizungumzia bajeti hii kwamba ni bajeti ambayo wanaishangaa, lakini wamefeli mapema kwa sababu hawana mbadala wowote. Nakumbuka nyakati zake Mheshimiwa Waziri alivyokuwa Mchumi Daraja la Kwanza aliwahi kuchanachana bajeti za aina hiyo. Nimpongeze na nasema kwa maoni yangu hii ni bajeti ya aina yake kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, sijawahi kushuhudia Bajeti Kuu ya Serikali ikionesha ongezeko la zaidi ya bilioni 660 kwa sekta moja ya kilimo, sijawahi kushuhudia kwa vipindi viwili. Sijawahi kushuhudia Bajeti Kuu ya Serikali ikiongeza bilioni mia moja kwenye ukomo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, sijawahi kuishuhudia. Sijawahi kushuhudia Bajeti ya Serikali ambayo imeonesha jitihada

zote; kwanza, kubana matumizi na pili, kuwaondolea wananchi hali ngumu za kiuchumi ila ni bajeti hii. Sijawahi kushuhudia bajeti ambayo inategemea sekta mbalimbali za uzalishaji ili kuongeza mapato, ndio naiona bajeti hii. Tulikuwa tunasema hapa wigo wa walipakodi ni wachache, niipongeze Serikali kwa kuja na mkakati wa kutoa *TIN* kwa kuanzia umri wa miaka 18 na kuendelea.

Mheshimiwa Spika, hapa kama Balozi wa Kodi nataka niwatoe hofu Watanzania, hata sasa si wote wanaolipa kodi. Wale wenye vipato vya kuanzia *zero* mpaka milioni nne hawalipi kodi yoyote. Kwa hiyo, ni wazi ambao watakuwa na *TIN* wasiokuwa na vipato, msingi wa kodi utabaki palepale ni kipato. Kwa hiyo, niwatoe hofu Watanzania tunaelekea kuzuri kwamba, Serikali ikifanikisha kutoa *TIN* kwa Watanzania takribani milioni 19, tunaweza kuongeza wigo wa walipakodi kutoka milioni tatu na kitu hadi kufikia pengine milioni 10, tutakuwa tumeleta ukombozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya sekta ambayo inategemewa kuchangia pato la Taifa, hasa pesa za kigeni ni sekta ya utalii, zaidi ya asilimia 25 ya pesa za kigeni. Naomba nichukue fursa hii nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa ubunifu wake wa kuja na *Royal Tour* na kipekee kwetu Mkoa wa Pwani, Mheshimiwa Rais alifika wakati wa kurekodi *Royal Tour,* lakini matokeo ya *Royal Tour* yamezungumzwa ndani ya Bunge na mwenye macho haambiwi tazama tunayaona, ongezeko la wageni wanaoingia ndani ya nchi, ongezeko la safari za Mashirika ya Ndege ya Kimataifa; mfano *Qatar* wameongeza mpaka safari 15, Emirates mpaka safari saba na mambo kadha wa kadha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niseme filamu ilionesha vivutio mbalimbali kikiwemo kivutio cha mbuga yetu ya urithi wa Taifa Ngorongoro. Hapa asubuhi zimeelezwa hoja mbalimbali, naunga mkono, ikiwemo Mheshimiwa Kishoa amesema vizuri, lakini nataka niseme yapo maeneo kwa mfano, eneo la Likongo, Lindi ambako kunatarajiwa kufanyika Mradi wa *LNG,* wananchi wale wametoa ardhi yao kwa bilioni tano tu fidia, hawakupewa nyumba, hawakusafirishwa, lakini wametanguliza uzalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo pale kwetu Bagamoyo tumetoa eneo la ujenzi wa viwanda na bandari ya kisasa. Tumelipwa tu fidia hatukupewa eneo la maisha, hatukupewa eneo la nyumba, wala maeneo mbalimbali. Hawa wenzetu wa jamii ya kimasai wamepewa upendeleo wa kipekee, lakini hii inaonesha namna gani Mheshimiwa Rais Mama Samia anajua uchungu wa mwana na uchungu wa Taifa lake na ndio maana kwa jamii ya Kimasai amefanya mambo ambayo hayajafanyika nchi yoyote ya Afrika; kulipa fidia, kuwasafirisha, kuandaa mazingira wezeshi, kuwapa nyumba, kuwapa maeneo mbadala.

Mheshimiwa Spika, mimi ambaye natoka Wilaya ya Bagamoyo nina ushahidi wa kukaa na wafugaji Wamasai maeneo mbalimbali, Mkoa wa Tanga, Mkoa wa Pwani, tuna Wamasai ambao wanamiliki ardhi. Niwaombe wakazi wa eneo la Ngorongoro kwa kuwa, Serikali imewaomba kuhama kwa hiyari na kwa kuwa eneo linalokusudiwa hapa na wanaweka *beacon* ni eneo la kilometa zisizozidi 1,500, niwaombe Watanzania wenzangu tuunge mkono jambo hili la utalii linaweza

kuiweka nchi yetu kwenye nchi ya kwanza kwa Afrika kwa vivutio vya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa niishauri Serikali vivutio viko vingi. Kama nilivyosema Mheshimiwa Rais alikuja Mkoa wa Pwani, kwetu Pwani tunacho kivutio Saadani, mbuga pekee ambayo Wazungu wanasema *where the beach meets bush* ni Saadani; tunacho Kisiwa cha Mafia ambako samaki mkubwa, Papa Potwe, anapatikana duniani; na tunayo mbuga Hifadhi ya Mwalimu Nyerere. Ninachoishauri Serikali ni kuharakisha ujenzi wa miundombinu ya kufikia vivutio hivi, ujenzi kwa mfano, kufikia Mbuga ya Hifadhi ya Taifa ya Saadani, tunaomba Barabara ya Mandela – Miono – Mkange ijengwe kwa kiwango cha lami ili ikutane na Barabara inayotoka Tanga – Pangani – Mkange. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kukifikia Kisiwa cha Mafia tunaomba uwanja wa ndege uwekewe taa, kwani Mafia ni ya tano kwa ubora wa fukwe duniani. Kwa hiyo, unaona umuhimu wa Kisiwa cha Mafia; kuifikia Mbuga ya Hifadhi ya Taifa ya Rufiji, tunaomba Serikali iharakishe ujenzi wa kiwango cha lami cha Barabara ya Kibiti – Mloka na Barabara ya Ikwiriri - Mloka – Mtemele. Hata hivyo, kwa sasa nishukuru kwa hatua ya Serikali ya kutenga pesa kujenga Barabara ya Ubena Zomozi – Ngerengere. Naamini itaelekea Mvuha - Kisaki na hatimaye itaingia kwenye bwawa letu ambalo tunatarajia kuwa ni bwawa la kutalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, niungane na wenzangu, hasa Wabunge wanawake kuomba Serikali ibaki na mtazamo huu kwamba, hizi pesa za halmashauri zibaki zichangie kundi la wanawake asilimia nne, kundi la vijana

asilimia nne na kundi la watu wenye ulemavu asilimia mbili. Halmashauri zetu zimetofautiana, mpango huu waliokuja nao Serikali ni mzuri, lakini uanzie na majiji makubwa yale 16. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatambua dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kulijali kundi hili la Wamachinga pia tunaipongeza Serikali kwa jitihada zake, imetenga bilioni 45 kwa ajili ya masoko haya. Kwa hiyo, tuombe hizi halmashauri nyingine tuendelee na huu utaratibu baadaye kidogo kidogo itafanyika tathmini.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo pia, niikumbushe Serikali suala zima la biashara ya vitenge. Nchi yetu kupitia soko la Kariakoo ilikuwa inafanya biashara ya vitenge kwa kiwango kikubwa na wanawake ndio waliokuwa wafanyabiashara hawa, lakini hatua za Serikali kwa mwaka wa fedha 2021 ya kuongeza kiwango cha malipo ya *container* kutoka dola *0.24* mpaka dola 1.0, lakini hatimaye wakapunguza mpaka dola *0.8* na kulifanya *container* kuwa na gharama zaidi ya milioni 300, imewafanya akinamama kushindwa kufanya biashara hiyo na hatimaye leo Kongo au Kariakoo imehamia Uganda, Kariakoo imehamia Tunduma na Kariakoo imehamia Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo wafanyabiashara hawa wanaenda kununua vitenge nchi za jirani na wanarudisha hapa. Tumepoteza kiwango cha zaidi ya bilioni 204. Niiombe Serikali kupitia Mamlaka ya *TRA* irudishe kiwango cha kawaida ili vitenge hivi viingie hapa nchini, lakini hata hivi ambavyo vinazalishwa hapa ndani ya nchi pia, najua nia ya Serikali ya kuvilinda viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, naiunga mkono bajeti ya Wizara hii. Naomba tuendelee kuwahamasisha Watanzania walipe kodi. Ndugu zangu bila ya kodi mambo yote mazuri haya ikiwemo elimu bure kwa kidato cha tano na cha sita, kutenga bilioni nane kwa familia maskini, Serikali yetu inaweza kupata ugumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na nawapongeza sana Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abubakar Damian Assenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Samuel Hhayuma na Mheshimiwa Robert Chacha Maboto ajiandae.

**MHE. ABUBAKARI D. ASSENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2022/2023. Nami kama walivyosema Wabunge wenzangu hapa, napenda kuendelea kuwapongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha bajeti hii vizuri kabisa na kuwasilisha kazi inayoendelea ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. Nawashukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, kaka yetu Emmanuel Tutuba ambaye kwa kweli ni Katibu Mkuu msikivu sana na usikivu wake sisi tumeuona katika ufuatiliaji wa Barabara yetu ya Ifakara – Kidatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema kwenye bajeti hii kuna mazuri mengi sana, nikisema tutumie muda hapa wa kuyasema hayo mazuri tutamaliza dakika zetu, lakini tunaenda kutaja mazuri huku tukichangia.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, mimi kama Mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* kuna mambo ambayo tunataka tuyapongeze na tuiombe Wizara ihakikishe kwamba, bajeti hii inafanikiwa na mambo haya yanafanyika, ili Serikali zetu za mitaa ziweze kufanya vizuri zaidi. Jambo la kwanza, nimemsikia Mheshimiwa Waziri kwenye bajeti yake na nimesoma, anasema kuhusu uboreshaji wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani hasa katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, sisi katika Kamati ya *LAAC* maeneo mengi tumepita tumekuta kwamba, kitengo hiki ni kama kimekufa. Ni kwamba, ni kitengo tegemezi kwa Mkurugenzi ambaye wanamkagua na kumshauri. Sasa kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ni wazi kwamba, kinaenda kuboreshwa Kitengo hiki cha Ukaguzi wa Ndani na kitakuwa *indicator* kubwa kwa *CAG* anavyoenda kukagua katika halmashauri zetu. Hilo ni jambo la msingi sana na tunamwomba Mheshimiwa Waziri kwa kweli kiboreshwe kama alivyosema, watafute fedha katika bajeti hii wahakikishe wanamwezesha *CAG,* kama walivyosema wamempa asilimia mia ya bajeti yake, basi na Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kwa Taifa na katika halmashauri kiende vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukomo wa bei. Sisi katika hesabu za Serikali za Mitaa huko, tenda na mambo mbalimbali, tumeona kwa kweli kama kuna sehemu hela zinapigwa basi ni katika tenda mbalimbali hizi za halmashauri zetu. Tumemsikia Mheshimiwa Waziri kasema kwamba, utaratibu wa ununuzi utakuwa na ukomo wa bei usiotofautiana sana na soko; basi tunashukuru na tunapongeza hatua hii itaokoa sana fedha za Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, mengine wamesema katika TEHAMA, mimi bado nasema TEHAMA ni muhimu sana katika dunia ya sasa ya sisi vijana. Hatuwezi kwa kweli, kuendelea kuogopa TEHAMA, tufanye mikutano, Mabaraza ya Madiwani, imeshindikana Waheshimiwa Wabunge kushiriki vikao vyote vya Mabaraza ya Madiwani. Pamoja na maelekezo mbalimbali ya Serikali kwamba, lazima tushiriki kama Wabunge katika vikao hivyo, lakini imeshindikana kwa sababu lazima vitaingiliana na ratiba za halmashauri, vitaingilina na ratiba za Bunge. Kwa hiyo, kwa kutumia hiyo TEHAMA itatusaidia sisi kushiriki, kwa hiyo, mimi naunga mkono jambo hilo lifanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia katika Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa tuliona matatizo makubwa ya kurejeshwa fedha katika miradi. Ikishafika 30 Juni, Wakurugenzi wa Halmashauri wanakuwa wanahangaika, wanahaha kuhakikisha kwamba, wanawahi hata saa nyingine kulipa bila utaratibu kwa sababu, fedha zitarudi kwenye mfumo. Tumemsikia Mheshimiwa Waziri anasema hilo halitakuwepo kwa sababu, hilo ni kuwaadhibu wananchi ambao hawana hatia.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine zuri ni Usajili wa Wakuu wa Taasisi kwa ushindani, kuwapa malengo ya taasisi na malengo yanayopimika, ni jambo zuri, kufuta ada ni jambo zuri, kuongeza bajeti ya kilimo kutoka bilioni 294 mpaka 954, ni jambo zuri. Hapa kwa kweli, nitapasemea huku mbele kwa sababu, naona hili ni jambo kubwa sana ambalo ningekuwa na uwezo ningemwambia Mheshimiwa Waziri wa Fedha, basi tarehe Mosi, Julai au tarehe 2 Julai, ampatie Waziri wa

Kilimo hizi fedha zote ili akatekeleze bajeti ya kilimo kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mazuri ni mengi sana, lakini napenda kusema wazi kwamba, mimi kama kijana siwezi kuunga mkono suala la kuondoa *5%* katika *10%* ya mikopo ya vijana katika halmashauri. Kama walivyosema Wabunge wengine hapa haiwezekani, kwanza haieleweki. Mimi nina Ilani ya Uchaguzi nimesema hapa nimeisoma hii Ilani inaahidi kuhusu hiyo *10%* na sisi tunatekeleza hii ilani sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi, Godfrey Chongolo, amezunguka hata juzi anasema kuhusu hiyo *10%.* Sasa wale waliofanya ubadhirifu kukopa fedha hizi bila utaratibu wasisababishe fedha hizi zikaondolewa kwa vijana, Serikali iwawajibishe tena hata kule Kilombero, Morogoro tunao. Wawajibike waende Mahakamani wachukuliwe hatua wawajibike. Machinga ni watu wazuri sana, lakini tutafute vyanzo vingine mbadala vya kuendeleza masoko ya Machinga.

Mheshimiwa Spika, halmashauri ambayo ina mapato ya bilioni moja ukitoa *10%* milioni 100, ukitoa *5%* ni milioni 50, itajenga soko gani na 50 zinazobaki zitasaidia vijana wangapi? Kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Waziri arekebishe katika *paper* yake hapo tuachane na jambo hili tuendelee kutekeleza ilani kuhakikisha kwamba, tuna *10%* ile ya *4:4:2* kama ilivyo kawaida.

Mheshimiwa Spika, ziko falsafa zinatufundisha, pamoja na utekelezaji wa bajeti ya Mheshimiwa Waziri, kufikiri nje ya *box* zaidi na kutazama bajeti zetu nyuma. Sidhani kama kuna bajeti ilishawahi kuja hapa Bungeni

haikuwa na shamrashamra? Bajeti zote zina shamrashamra, bajeti zote zinapendeza, bajeti zote tunasema ni sawa, tunazisema vizuri, lakini tunafanya tathmini ya miaka mitano nyuma mathalani. Tunaweza tukasema korona hii ya juzi, vita ya Ukraine, lakini miaka mitano nyuma utekelezaji wetu wa bajeti ni asilimia ngapi? Ni vitu gani vinatukwamisha katika kuhakikisha hatufikishi asilimia 80 ya utekelezaji wa bajeti? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa si lazima Mheshimiwa Waziri, sijui kama hii *41 trillion* ambayo tunaitafuta sasa hivi tutaipata na tutatekeleza kwa *100%* ama asilimia 80 ama asilimia 90 sina uhakika, lakini kufikiri nje ya *box* ama falsafa ya kusema jikadirie kihalali, kama anavyosema Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson; lazima tujikadirie kwa kujiuliza miaka 10 nyuma je, tunajitazama kweli sisi kama Watanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu, hatuwezi kutaja bajeti zinazoongezeka tu tuonekane nchi yetu inaendelea, lakini utekelezaji haufiki *80%,* lazima tujikadirie kihalali na ni lazima tufikirie nje ya *box*. Tazama 2016/2017 ilikuwa trilioni 25; mwaka unaofuata 2017/2018 ikawa trilioni 26; mwaka 2018/2019 ikawa trilioni 28; mwaka 2019/2020 ikawa trilioni 29; mwaka 2020/2021 ikawa 32; mwaka 2021/2022 ikawa 39; mwaka 2022/2023 tuna trilioni 41. Inaongezeka ndio, ni vizuri, lakini hata katika *economics* ya *form five* na *six* katika *economics* ya *diploma,* yuko baba yangu Mkenda atasema, walitufundisha aina tatu za bajeti na ziko nchi zinatumia aina nyingine za bajeti. Sasa kama nchi yetu tangu ipate uhuru inatumia aina moja ya bajeti, *deficit budget* kwamba, matumizi tunapanga mengi kuliko mapato,

tuachane nayo na kwa ushahidi kwamba, hatufikishi asilimia 80. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wametufundisha kuna *balanced budget* kwamba, zipo nchi zinapanga matumizi sawa na mapato yao na kwa sababu, zina mipango ya maendeleo ikitokea fedha za *IMF, World Bank* na misaada mingine wanachukua, wana-*click* katika ile *check list* kitu gani tulipanga kufuata tukifanye tuingize pale na Watanzania ni waelewa, hiyo ni *balanced budget* kwamba, tunapanga matumizi sawa na mapato yetu.

Mheshimiwa Spika, tumefundishwa kuna *surplus budget*. kwamba, unaweza ukapata mapato mengi ukapanga matumizi kidogo, lakini ya mwisho hii *deficit* ambayo tunaing'ang'ania ya matumizi mengi kuliko mapato, ufanisi wake miaka mitano nyuma unaonekana haufiki *80%.* Kwa hiyo, nasema kufikiri nje ya *box,* kujikadiria sijui hii *41 trillion* iko wapi kwa sababu, tunakopa tena *five trillion* hapa tunaongezea kwenye hii bajeti. Hatuna uhakika kwa sababu, majanga yamekuwa majanga, *Covid-19* itakuja *Covid-42* itakuja ngapi, sisi tunaamini hizo nchi zitatupa hizo fedha tuongezee kwenye bajeti utekelezaji ukija hapa asilimia 60, asilimia 70 au asilimia 80. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania ni waelewa. Mathalan tunapata shilingi trilioni mbili kwa mwezi kutoka *TRA*. Kwa mwaka ni shilingi trilioni 24, mapato yasiyo na kodi shilingi trilioni sita, una shilingi trilioni 30. Mheshimiwa Waziri panga mipango yako katika shilingi trilioni 30 tuletee hapa tutoe vipaumbele vya kutekeleza asilimia 100. Peleka kwenye hizo Wizara kama tano za mfano, tutekeleze asilimia 100, tusonge mbele, watu wataelewa. Halafu *on the way* tukipata fedha

za *World Bank*, UVIKO na kadhalika, tunakaa kama Bunge tunaeleweshwa, tunaendelea na mpango wetu wa Serikali wa miaka mitano. Hilo Watanzania watalielewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mathalan tunahitaji shilingi bilioni 954 hii ya kilimo, hata Mheshimiwa Waziri Bashe apewe kesho. Ila kwa mfumo wa Wizara zote kupewa pewa fedha hivi, hakuna Wizara itatekeleza kwa *hundred percent.* Vipaumbele vya Taifa letu ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nasisitiza, katika kilimo hapa ni pazuri sana na vipaumbele vya Taifa vichache vya kutekeleza kwa asilimia 100 kwa kutegemea mapato yetu tuliyokuwa nayo ni ya uhakika, kuliko kwenda mwakani kwa sababu tuna *fourty one*, lazima tujikadirie kihalali. Tuna *fourty one* leo, mwakani tunataka tuwe na *fourty five billion, how* tunaipata na uchumi wa dunia unarudi chini?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri siyo lazima kufikiria zaidi ndani ya *box* tangu uhuru mpaka sasa hivi, ndani ya *box* tu, kwamba sisi *surplus* bajeti mwaka 2021 ilikuwa *fourty one*, tukiongeza *fourty five* ndiyo tutaonekana tunaendelea, *no!* Tuna uhakika gani na mapato ya nchi yetu ya uhakika ya *TRA* na mapato yasiyokuwa na kodi tukijumlisha tupange mipango hiyo, Watanzania watatuelewa.

Mheshimiwa Spika, uzuri wake, Mheshimiwa Rais Samia sasa hivi amesema vizuri sana, amekuwa muwazi na anakuwa kama ana mashaka na mambo ya mikopo. Wakati wa mikopo hii ya *one trillion* ya *COVID* amezungumza wazi, tumieni vizuri mikopo hii, Watanzania watalipa. Juzi tulikuwa tuna miradi 28 ya maji, amezungumza hivyo hivyo, amesisitiza kwamba tutunze sana fedha hizi za mikopo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nashauri sana kwa kumalizia kuwa Mheshimiwa Waziri mwakani kama hii

haitafika *eighty percent,* basi tufikirie bajeti ya kupanga kutokana na matumizi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, tujikadirie tuje nje ya *box*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Samwel Hayuma atafuatiwa na Mheshimiwa Robert Chacha Maboto na Mheshimiwa Tabasam Hamisi Mwagao ajiandae.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nami nianze kuchangia hoja hii kwa kuanza kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwigulu Nchemba na timu nzima ya Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri wanayoifanya, lakini nigusie tu kwamba tunayo barabara yetu inayotoka Hydom kuja Katesh. Ile barabara inategemewa sana na wana Hanang na Watanzania. Pia ile barabara ukifika Katesh inaunganisha na Nangwa - Gisambala - Nkondoa ni barabara muhimu sana kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Hanang ukiacha kuwa wanalima sana mazao mbalimbali ikiwepo ngano na ndiyo kitovu cha uzalishaji wa ngano kwa Taifa hili, lakini pia tuna kiwanda cha *cement* ambacho kiko kwenye utaratibu wa kuanza, na pia tuna kiwanda cha chumvi ambacho kiko kwenye utaratibu wa kuanza. Kwa hiyo, barabara hizi zikitengenezwa zitatusaidia sana kusafirisha bidhaa hizo muhimu kwa Taifa letu na itakuwa ni *hub* ya kuilisha Dodoma ambako ndiyo Makao Makuu ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, vilevile tuna barabara ambayo inatoka Kibarashi inakuja mpaka Kijungu – Kibaya – Kijoro; barabara hii inakuja mpaka Dalay – Mbicha. Kwenye mpango wa Taifa ambao tumeupitisha hapa Bungeni na bahati nzuri ninao hapa, barabara hii inapita Kondoa, baada ya Kondoa inaenda Singida. Ila kwenye mpango ambao Mheshimiwa Waziri ameuleta sasa, barabara hii amei-*divert,*

badala ya kupita Kondoa, yeye anataka ipite Chambalo, ipite Chemba baada ya hapo iende kwa Mtoro halafu Singida.

Mheshimiwa Spika, barabara hii inategemewa na watu wengi, barabara hii tumeinadi kwenye ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Wana-Hanang nimewaambia, wana Kondoa vijijini wameambiwa wana-Kondoa Mjini wameambiwa, maeneo mbalimbali watu wameambiwa kwamba hii barabara inakuja kutengenezwa.

Mheshimiwa Spika, barabara hii iko kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, iko kwenye ukurasa wa 73. Sasa kama iko kwenye Ilani, pia iko kwenye mpango wetu wa miaka mitano 2021/2022 - 2025/2026. Nini kilichotokea hapa katikati hii barabara ikabadilika? Mheshimiwa Waziri mimi niseme wazi, hii barabara inategemewa na watu wengi, na watu wameweka matumaini huko. Hayo mabadiliko mnayoyafanya sasa, watu hatuyatambui, ni mapya, hatuyaelewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwa niaba ya wana-Hanang, wana-Manyara wana-Kondoa tunaomba utupe ufafanuzi, nini kilichotokea? Kwa sababu haipo kwenye mpango, haipo kwenye Ilani, kama itabaki hivi ilivyo ndugu yangu Mheshimiwa Waziri wewe ni mtani wangu, kwa hapa hatuko pamoja. Hapa hatuko pamoja, naomba hili niliweke wazi kabisa. Hili lirekebishwe. Naamini ni makosa madogo ya kiuchapaji, siyo ya kimpango. Makosa haya ya kiuchapaji yarekebishwe ili yale matumaini ambayo Watanzania wameyaweka hapo yaendelee kubaki kama yalivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusemea hili suala la barabara, na mara zote napenda kuongea masuala ya barabara, nimefananisha barabara na mishipa ya damu ya mwili wa binadamu, kwa sababu barabara ndizo

zinazoboresha uchumi wa maisha ya wananchi. Lazima hapo tupaangalie vizuri.

Mheshimiwa Spika, nichangie kidogo kwenye eneo la ukuaji wa uchumi wa Taifa. Nimejaribu kupitia kwenye hotuba ya Waziri. Ukiangalia, ametupa taarifa, mwaka 2019 chumi za nchi za kusini mwa Afrika zilikua kwa asilimia 3.1, lakini wakati wa Corona mwaka 2000 uchumi ukashuka sana ukuaji wake mpaka -1.7. Baada ya Corona kuondoka mwaka 2021, ukuaji huo ukaboreka ukaenda kwenye 4.5.

Mheshimiwa Spika, kwenye nchi zetu za Afrika Mashariki, ukijaribu kuangalia ukuaji kabla ya *Corona* mwaka 2019 nchi nyingi sisi tulikuwa 7.0, lakini nyingine zilikuwa 4.8, 9.5, 3.1, 1.8, 0.9. Baada ya *Corona* kututandika na mambo yakaenda ndivyo sivyo, sisi Tanzania kwa kuwa tulichukua hatua mahususi za kutokufunga shughuli za uzalishaji, za kuhakikisha kila fursa tunayoipata tunaitumia ili kuhakikisha kwamba uchumi wetu haudorori. Tulikua kwa asilimia 4.8, lakini nchi nyingine zote za ukanda wa Afrika Mashariki iliyojitahidi sana ilikuwa kwa 0.6, lakini kuna nyingine zilifanya vibaya kabisa, zilikua kwa -6.6.

Mheshimiwa Spika, baada ya *Corona* mwaka 2021 nchi nyingi zili-*bounce back*. Iliyoshindwa sana ilikuja kwenye 0.1 kwenye ukuaji wa uchumi, lakini hiyo kabla ilikuwa na -6.6. Maana yake ni kwamba baada ya *Corona* yenyewe ule ukuaji wa uchumi wake umeongezeka kwa asilimia 6.7. Sisi tume-*bounce back* kwa 4.9, ongezeko la asilimia 0.1.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema, ukiangalia sisi baada ya *Corona* ile *gain* haijawa kubwa. Wataalam wetu wa uchumi, Mheshimiwa Waziri ukiwaongoza, hapo tunapaswa kufanya kazi ya ziada. Tuangalie ni sehemu gani tunapaswa kuboresha ili tu *bounce back* kama wenzetu. Kuna nchi ambayo ilikuwa -3.4, lakini baada ya Corona iko 10.9. Maana yake ongezeko lake ni asilimia 14.3. Sisi

tunapaswa kujitathmini hapa, sehemu gani tumekosea na nini tukifanye?

Mheshimiwa Spika, nimejaribu kuangalia kwenye suala la ukuaji wa uchumi mwaka 2021, sekta ambayo imeongoza ni sekta ya ujenzi asilimia 13.1. Ni imani yangu kwamba eneo hilo lilifanya vizuri kwa sababu fedha ziliongezwa kwenye eneo la *TARURA*, shughuli nyingi za uchumi zilifanyika kwenye ujenzi wa miundombinu. Ukiangalia shughuli ambayo Watanzania wengi wanategemea, kilimo imekua kwa asilimia 9.6, lakini ufugaji asilimia 7.1. Ukiangalia ndiyo Watanzania wengi walikoajiriwa.

Mheshimiwa Spika, kwa wastani wa kitaifa, wakulima na wafugaji ni asilimia 65 *plus.* Kwa sisi wa vijijini ni zaidi ya asilimia 95. Eneo hili tumeongeza bajeti, ni jambo jema, lazima tuangalie namna ya kuhakikisha kwamba inaleta tija ambayo tunaitarajia.

Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia maeneo ambayo yamefanya vibaya sana, kuna suala la sayansi, utaalam na ya ufundi. Mheshimiwa Waziri wa Elimu alitueleza kwa kina wakati ana-*present* bajeti yake na akasema yeye ataweka *incentive* kwa wale ambao watafanya tafiti zitakazoleta tija na hatimaye atatoa fedha. Naomba kwenye eneo hili, Waziri wa Elimu awezeshwe ili tafiti ziweze kufanyika na hatimaye ugunduzi uweze kufanyika, nchi yetu kwenye eneo hilo tuanze kujitegemea tujitengenezee vitu vyetu na eneo hilo liweze kukua kwa sababu ukuaji wake kwa sasa ni asilimia 0.9. Ila ukiangalia shughuli kubwa ambayo inaajiri Watanzania ni hilo eneo la kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwenye bajeti hii tumependekeza uingizaji wa ngano kutoka nje ya nchi tunapunguza kodi. Kwenye ngano tunapunguza kutoka asilimia 35 kuja asilimia 10. Tufanye maamuzi magumu kama tulivyofanya maamuzi magumu wakati wa *Corona,* wenzetu wakifunga mipaka sisi

tunafanya shughuli, uchumi unaimarika. Tuachane na kupunguza kodi kwenye eneo la shughuli zinazohusiana na kilimo kwa sababu watu wetu wana uwezo wa kulima.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wengi wako vijiweni, wakiamka asubuhi utawaona wanacheza karata, wako kwenye michezo ya bonanza; ile kamari ambayo kila siku mtu anakuwa na shilingi, lakini kila siku inaondoka na bonanza. Twende tukawahamasishe watu waende shambani wakalime, fursa ndiyo hiyo. Badala ya kusema tunapunguza kodi ili tupate mazao zaidi kutoka nje ya nchi, tuna ardhi ya kutosha ya kilimo, hatuna sababu yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata kwenye upande wa kilimo cha miwa, miwa mingi inaharibika lakini kwa nini tupunguze kodi kwenye sukari? Tuangalie eneo hilo. Hayo ni maeneo ya msingi sana kwa Watanzania wetu tukawahamasishe wakalime zaidi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nitaunga mkono hoja baada ya kuwa nimepata ufafanuzi wa barabara niliyoisema, ile ambayo haijakaa sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, atafuatiwa na Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao na Mheshimiwa Almas Athuman Maige, ajiandae.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwanza kwa kupata nafasi hii ili nami niweze kuchangia kwenye Wizara ya Fedha na Mipango. Awali ya yote namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo

anaendelea kuifanya kwa ajili ya Taifa letu. Suala la bajeti yetu ya nchi 2022/2023, imeenda mpaka shilingi trilioni 41. Fedha hizi, shilingi trilioni 41, kuna fedha ambazo zinakwenda kwenye Wizara ya Kilimo na Chakula.

Mheshiiwa Spika, juzi wakati Wizara ya Kilimo inawasilisha bajeti yake hapa nilitoa mchango wangu na nikashauri kwamba ikiwezekana Wizara ya Kilimo na Chakula ijiweke tayari au ijipange ili kutuwekea akiba ya chakula nchini takribani miaka miwili.

Mheshimiwa Spika, bajeti yetu hii ili iwe imara, na iwe yenye uhakika, lazima wananchi wetu wawe na uwezo wa kupata chakula; na nchi kama nchi iwe na uwezo wa kujiwekea akiba ya chakula kwa muda walau hata miaka miwili ijayo. Leo kukitokea tatizo la njaa kwenye nchi yetu, kwa bajeti hii tunayoipanga leo hapa au tunayoipitisha hapa leo, kukitokea njaa kwa wananchi wetu, mipango yote itakayokuwa imepangwa kutekelezwa kati ya 2022/2023 haitafanyika kwa sababu wananchi watakuwa na njaa na nchi itaingia kwa ajili ya kuwanusuru wananchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Wizara ya Kilimo na Chakula wamepewa bajeti kubwa kwa mwaka huu, lakini bado jambo la akiba ya chakula nchini ni la muhimu sana. Tusipolizingatia hili, kuna siku Bunge litakaa, litatoa maamuzi na kupitisha bajeti, lakini katikati ya safari wakati tunaendelea kukitokea njaa kwa wananchi wetu, bajeti ile itavurugika kwa vyovyote. Leo tukipata shida ya chakula hapa, lazima mipango mingine yote ile ambayo ilikuwa inapangwa kwa ajili ya utekelezaji wa maendeleo ya wananchi kwenye nchi yetu itavurugika. Taifa litageuka kufanya na kutafuta suluhu kwa ajili ya kuwapatia wananchi wake chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Wizara ya Kilimo na Chakula jambo hili ilichukue na ilifanyie kazi. Wenzetu wa nchi za nje wamejiwekea akiba kwenye mambo yao; mafuta na

vitu vingine, sisi Tanzania ardhi tunayo, mvua tunapata ya kutosha, na watu wapo. Tunakosaje kujiwekea akiba ya chakula cha nchi cha miaka miwili? Tukijiwekea akiba ya chakula cha miaka miwili, aidha miaka mitatu, yale yote ambayo tutakuwa tunakaa kwenye Bunge humu tukayapitisha, tuna hakika yatatekelezwa kwa sababu hatutapata mtikisiko katikati ya safari. Haiwezi kutokea.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni Mamlaka ya Mapato Tanzania. Mimi ni mfanyabiashara, lakini wafanyabiashara walio wengi hapa nchini kwetu sio wafanyabiashara ambao wamesomea mambo ya biashara. Sisi tunafanya biashara kutegemeana na kile ambacho umekiona kiko mbele yako, aidha kwa namna ambavyo umepata mtaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishauri Wizara ya Fedha kwamba Mamlaka ya Mapato Tanzania na kwa sababu wafanyabiashara wetu walio wengi hawakusomea mambo ya biashara, ni vizuri mamlaka ikaweka zile kodi za wafanyabiashara wazi ili kuongeza tija kwa walipakodi. Ila wafanyabiashara wale kwa sababu hawana elimu ya biashara, halafu yule anayekuja kuwafanyia hesabu ya kulipa kodi amesomea, kwa hiyo, anabaki kumsikiliza kila atakachomuamulia yeye. Wizara ikitengeneza mpango wa kutengeneza kodi ya uwazi, kwanza itawavutia wafanyabiashara wengi na kujua viwango halisi vya kodi zao wanavyotakiwa kulipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huwa najiuliza, kwa mfano, kwenye bajeti hii ya Shilingi trilioni 41, labda fedha ambazo zinatoka kwa wafanyabiashara labda ni Shilingi trilioni 12 au 13, halafu wafanyabiashara na walipakodi wale wote ambao wanalipa, kama ni wafanyabiashara mle kwenye idadi yao, inajulikana wako wangapi? Kila mtu analipa kiasi gani? Kama kweli tunataka kuondoa hii sintofahamu iliyopo kati ya wafanyabiashara na Mamlaka ya Mapato, pangewekwa

utaratibu kila mmoja akawa anajua kodi yake atakayoilipa kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine linatolewa jedwali tu ambalo linamwonyesha Maboto mwaka huu fedha zitakazotakiwa kuchangia kwenye kodi ya Mamlaka ya Mapato ni kiasi fulani kwa mwaka, na ikishatolewa hiyo hakutakuwepo na mazungumzo tena na mtu mwingine. Watu wa Mamlaka ya Mapato watabaki kuja kukaa kufuatilia namna ya ulipaji wa zile fedha ambazo zimetolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili linapoachiwa tu kwao wenyewe wakaenda kuzungumza na watu ambao wao kwenye biashara wameingia tu kufanya biashara, jambo hili wakati mwingine linaleta sintofahamu kwa wafanyabiashara, halafu linawafanya pia nao wasione kwamba kile wanachofanyiwa ni haki kwenye kodi zile wanazokuwa wanakadiriwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, nataka kuzungumzia suala la madini. Jambo hili naona bado lina matatizo makubwa, kwa sababu wananchi wetu kwenye maeneo yao wanayoishi, wanakuwa ndio wa kwanza kuvumbua sehemu hii kama ina madini. Wao wenyewe wananchi wa kawaida tu, wakishavumbua lile eneo ambalo lina madini, hawa wataalam wetu wakijua kwamba wananchi wamegundua eneo ambalo lina madini, wanachokifanya ni kwenda kutafuta watu ambao wanakata leseni kwenye eneo lile, bila kuwahusisha wananchi wenyewe, wahusika. Jambo ambalo bado linaleta mgogoro mkubwa.

Mheshimiwa Spika, ukija kuangalia, kiongozi wa wasimamizi wa wachimbaji wadogo wa madini nchini, yeye mwenyewe ni mfanyabiashara wa madini, halafu yeye ndio anawasimamia wachimbaji wadogo, halafu yeye mwenyewe huyo ndio akawatafute wenye mashamba akazungumze nao. jambo hili halikai vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kama Kiongozi wa Wachimbaji Wadogo wa Madini Nchini, anatakiwa atokane na watu ambao hana *interest* yoyote na uchimbaji wa madini ndiyo ataweza kuleta haki kati ya wenye mashamba, wenye leseni na wachimbaji wadogo. Anapewa mtu kusimamia wachimbaji wadogo aidha wenye mashamba na sehemu ya kuchimba madini ambaye yeye mwenyewe ana-*interest* na uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Spika, jambo hilo linaleta migogoro mikubwa sana kwa wananchi wetu linawafanya wao waone, wao kama raia wa kawaida wamevumbua eneo lile la uchimbaji wa madini, huyu yeye kwa sababu anakuwa yupo ngazi ya juu anakwenda anatafuta leseni anakuja kuwaambia kwamba eneo hili tulishapata leseni miaka mitano iliyopita. Wakati madini yamevumbuliwa labda zaidi ya mwaka mmoja au miaka miwili iliyopita. Sasa jambo lile linaleta mgogoro mkubwa sana kati ya wananchi na Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, wale Wasimamizi wao na Viongozi wa Wachimbaji Wadogo nchini, wanasababisha migogoro iendelee kuwa mikubwa jambo hili lisipowekwa vizuri kuna siku ninaamini litaleta mgogoro mkubwa kwa sababu wale wananchi wanaona kama wananyimwa haki zao, madini ya kwao, eneo la kwao, ardhi ya kwao, Babu yake na Bibi yake wamezikwa hapo halafu leo … *(Makofi)*

**SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa kengele la pili imeshagonga.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hamis Tabasam Mwagao, atafuatiwa na Mheshimiwa Almas Athuman Maige, Mheshimiwa Francis Isack Mtinga ajiandae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia katika Bajeti Kuu. Kwanza, naipongeza Wizara kwa kuandaa bajeti ya wananchi na kwa mara ya kwanza katika nchi hii tunapata bajeti ya kijamaa, lakini nasikitika kwamba Waziri wakati anakuja kuiwasilisha ile bajeti hakuja kijamaa lakini nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nataka nianze na Bandari, bandari ni mlango ambao tumepewa na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya sisi kutokupata shida, uwekezaji wa bandari kwa mwaka jana tu Mheshimiwa Rais Samia wakati anaingia madarakani kulikuwa kuna mradi pale ulikuwa unahitaji shilingi bilioni 210, baadaye mwezi Desemba ikatolewa shilingi bilioni 290, tukapata shilingi bilioni 500 katika kutengeneza kupanua bandari.

Mheshimiwa Spika, bandari ndio mlango pekee ambao unatakiwa kutusaidia kupata fedha nyingi, kwa mfano kwa mwaka huu tunapata Trilioni Moja na katika hiyo Trilioni Moja ambayo tunakuja kuipata katika bandari kwa magati 12 tu, sasa tukiangalia nchi ambazo zinatuzunguka, tukiwaangalia Kenya, wenzetu Kenya wanajenga bandari ya pili Lamu ambayo itakuwa ina magati karibu 40, wana bandari yao ya Mombasa ina magati 25, leo tuna mtu mwingine ambaye ni mshindani wetu Beira ana magati 17 anapanua magati Sita kupata 23. Pia tunae mshindani wetu mwingine wa nne ambaye sisi tunamuona siyo mdogo ni mkubwa ana magati 52 Durban.

Mheshimiwa Spika, sasa ukichukua wenzetu wanapakua meli za kutosha, kwa mwezi Mombasa anapata meli kama 240 kwa siku anapata meli sita hadi nane. Dar es Salaam tunapata wastani wa meli mbili au tatu kwa siku, sawa na wastani wetu sisi ni meli 60 hadi 70 kwa kipato cha Trilioni Moja. Wenzetu Bandari ya Beira wanapata meli nne hadi

tano, wenzetu Bandari ya Durban wanapata meli kuanzia10 hadi 15 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, sasa tunakwama wapi Mheshimiwa Waziri? Ni kwamba tunao uwezekaji wetu Kwala kutoka Dar es Salaam kwenda Kwala ni kilometa 90, lakini Kwala kama tutasafirisha reli yetu hii tuliyonayo ambayo siyo ya mwendo kasi, hii reli yetu tu ya Mjerumani tuliyoirithi, kutokea Dar es Salaam tukaweka vichwa vipya vikachukua yale makontena kutuletea Kwala kwenye eneo ambalo limekwenda kuwekezwa na Bandari ni hekta kama tano ambalo linaweza likakaa na makasha kontena zaidi ya 3,600, bandari inakuwa wazi tunapata nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri hapa leo mimi naomba nikushauri nachukua ndani ya Katiba Ibara ya 72 inasema Kazi ya Mbunge ni kuishauri na kuisimamia Serikali, leo pokea ushauri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umeniteua kuwa Balozi wa mafuta nitakuja kwenye mafuta leo nipo kwenye bandari halafu nitakuja kwenye mafuta. Sasa kule Kwala nakushukuru mmetenga eneo la kuwapa wenzetu Warundi mmetenga eneo la kuwapa Wazambia, Wakongo, mmetenga eneo la kuwapa Wanyarwanda na Waganda, sasa…

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasamu, hiyo mmetenga unaniunganisha mimi na nani?

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nasema Serikali.

**SPIKA:** Maana wewe unazungumza na mimi na kama unasema Serikali sema Serikali imetenga.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam kwa sababu ukisema mmetenga na Spika wako unamuweka huko, maana wewe unaongea na mimi hapa.*(Kicheko/Makofi)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru endelea kunilinda.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga eneo kwa ajili ya kuwapa wenzetu sehemu ya kushushia mizigo na hiyo itakuwa fursa kupakuwa mizigo mingi, sasa kwa hatua hiyo mwendelezo wa lile eneo la Kwala toka mwaka 2017 eneo linatengenezwa haliishi, na kutokea Vigwaza kwenda kule Kwala ni kilometa 15, kutokea Ruvu kuja Kwala pale ni kilometa moja na nusu. Reli tayari imeshatengenezwa pale, kwanini kunakuwa kuna mlundikano wa makontena Dar es Salaam tunashindwa kushusha mizigo kwa wakati? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, meli ukipita nenda kule *Sea Cliff*, ukiwa eneo la Msasani Dar es Salaam unaona meli zimefunga gati kule, zile ni *demurrage charges* tunapata hasara Watanzania. Kwa mfano, meli ikisimama kule kwa ajili ya kushusha mafuta *demurrage charge* peke yake tunapaka kwa mwezi Bilioni Mbili, Bilioni 24 tunapoteza kwa ajili ya *demurrage charge*. Bilioni 24 ukizipigia hesabu kama Kituo cha Afya kimoja kinajengwa kwa Milioni 500 angalieni Billioni 24 tunapoteza vituo vingapi vya afya. Leo bado Waziri unakwenda kuchukua asilimia tano kwamba uitoe kule wakati kuna fedha tunakaba hapo bandari tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa hatua hiyo ni kwamba tukiimarisha bandari yetu, tukawekeza katika bandari kwenye mifumo na teknolojia pale bandarini, tutashuka hadi reli 300 kama leo meli 70 tunapata Trilioni Moja, kwanini tusishushe meli 300 tukapata Trilioni Nne. Naomba Waziri wa Fedha uzingatie jambo hili tukiwekeza katika bandari tunaweza kufaulu, na hizi kodi ndogo ndogo zinatoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niongelee kuhusu suala la ushindani. Suala la ushindani kama wenzetu wana magati mengi kiasi hiki hatutaweza kuja kupata hizi fedha, tuangalie nafasi yetu ya kusafirisha haya makasha, tufanya haraka kwa ajili ya uwekezaji wa Kwala, tukiifungua Kwala bandari itakuwa wazi, tutaweza kushusha mizigo yetu vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo bandari ina miaka 75 imeanzishwa mwaka 1947 lakini leo bandari zinazoanzishwa mpya zinatuzidi sisi wenye miaka 75. Pale bandarini kuna mifumo 36 yaani uki-*log* ili utoe kontena mifumo 36 unaingia kwanini usiwe na mifumo mitatu, huko na kwenyewe tunakwenda kuvujisha pesa. Tunakuomba ukija kwenye majumuisho yako utueleze lini Mheshimiwa Waziri utarejekebisha hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mafuta. Kuna bwawa la kushushia mafuta kule Kigamboni - Mji Mwema, wanaita *SPM*. Bomba lile lipo tunaweza tukashusha mafuta pale *metric* tani 120,000 lakini tukilisogeza mbali kidogo tu kwa kilometa mbili meli itakayoweza kushusha pale ni meli ambayo inaweza ikabeba metric tani hadi tani laki tano za mafuta. Tunaweza tukachanganya mafuta ya petroli na dizeli tuweke la pili litakalopakia petroli kwa sababu ndani kule Kurasini meli zinazoingia kule ni *metric* tani 39 zina oda moja ya mafuta inatolewa Tanzania vimeli vidogovidogo vya *metric* tani 40. *tender* moja inatoa meli nane, lazima wananchi wanakuja kuumia.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri uliniteua mimi kuwa Balozi wako wa mafuta, hebu tukae tuongee sasa na mimi nitakuletea na watu wengine tuje tukae tuzungumze tunaumizwa wapi kuhusiana na suala la mafuta, ukiniita tukaja na hao wanaokataa kwamba hatuumii katika mafuta, tuje kwenye mjadala wa Kitaifa kimya kimya tu utaona tunaokoa hizi fedha nyingi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TPDC* ukiona watu wanapinga *TPDC* isiwezeshwe ujue hao ni maadui wa Taifa hili. Yapo makampuni duniani makubwa ngoja, nivae miwani naona hata macho sioni vizuri sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika kuna makampuni kwa mfano kama Abu Dhabi kuna kampuni inaitwa *ENOC - Emirates National Oil Company* ni kampuni *giant* kampuni kubwa kuna *ENOC* kuna Malaysia wale wanajiita *PETRONAS* kuna Saud Arabia *ARAMCO* kuna *SONATRACH* ya Algeria, kuna kampuni ya Nigeria inaitwa *NNPC* kuna Oman *OTI,* kuna Urusi wanajiita *Rosneft*, lakini wapo wale mpaka Brazil. Brazil wana kampuni kubwa za mafuta ambazo zinafanya kazi zote. Mheshimiwa Waziri, Kampuni hizo zinatafiti mafuta, kampuni hizo zinasafirisha zinauza, sasa sisi tunafeli wapi kuiongezea mtaji?

Mheshimiwa Spika, leo *TPDC* inaidai *TANESCO* Bilioni 552 hiyo ilikuwa hadi mwezi wa Machi, hadi leo kama deni lile bado linaendelea kwa Bilioni 50 kila mwezi leo limefika Bilioni 700, hivi tunavyozungumza na wewe kama wataiwezesha *TDPC* tunatoka,. *(Makofi)*

**SPIKA:** Muda umeisha Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, naomba dakika moja nizungumzie Hazina tu tuwasaidie kuwafungua *TPDC* naomba.

**SPIKA:** Sekunde thelathini.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, ahsante *TPDC* Mheshimiwa Waziri ni kwamba…

**SPIKA:** Ongea na mimi Mheshimiwa unavyomwongelesha Waziri ndiyo maana muda wako unaenda haraka zaidi.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Spika, kuna *TIPER, TIPER* kule tumewekeza tuna asilimia 51 ya kwetu kwa *ORYX* lakini kuna hawa watu wa *BP* ambao wameuza *PUMA* tuna asilimia 50 ile ni mali ya Serikali, *PUMA* wale watu wa PUMA tunakuomba tu hawa watu wa Wizara ya Fedha, Msajili wa Hazina achukue zile hisa akamkabidhi *TPDC*.

**SPIKA:** Haya ahsante.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa mchango wangu.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO**: Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Aya ahsante sana. Mheshimiwa Almas Athuman Maige atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mheshimiwa Aida Joseph Khenani ajiandae.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kutamka rasmi kwamba naunga mkono hoja hii ya bajeti ya kufurahisha.

Nakushukruu sana kuniruhusu na mimi nichangie hoja hii ya Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka 2022/2023. Nianze kwanza na pongezi na shukrani. Mimi nampongeza sana Mama Samia Suluhu Hassan kwa alama nyingi alizotuwekea katika Jimbo langu la Tabora Kaskazini. Niruhusu nizitaje

baadhi ya alama ambazo kila mtu anaziona na ndiyo maana ninasema Mama Samia tunamuona kila siku Jimbo la Tabora Kaskazini. Mama Samia hongera sana. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna miradi ya maji Ziwa Victoria Vijiji 58 vitapata maji kutoka Ziwa Victoria kutoka kule Mwanza hadi Tabora Vijijini tuna maji, pia umeme tulikuwa hatuna sasa tunavyo vijiji 41 umeme unawaka tunamshukuru Mama Samia. Kuhusu afya tulipewa fedha za kujenga zahanati Nne tumejenga tatu na moja inaendelea kujengwa, pia vituo vya afya vitano tayari vitatu, bado viwili vinaendelea kujengwa kikiwemo kile cha Marehemu Benjamini Mkapa pale Usagali. Tunampongeza sana Mama Samia Suluhu Hassan, pia tumejenga hospitali kubwa ya Wilaya hongera sana Mama tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhsuu elimu, sawa tuna elimu ya bure kuanzia darasa la kwanza hadi *Form Six*, tuna kuunga mkono na tunampongeza sana Mama Samia Suluhu Hassan, lakini pia tumejenga madarasa 17 ya shule za Sekondari na shule mbili shikizi, tunampongeza sana Mama Samia Suluhu Hassan. Pia tunayo shule mpya inayojengwa tumepewa Milioni Mia Nne itakayoitwa Almas Maige kule Gilimba tunampongeza sana Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan. Pia kipo kituo cha *VETA* ambacho kimegharimu karibu Bilioni Mbili kinakaribia kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye bajeti, kabla ya bajeti kuna barabara sita zinajengwa kwa fedha ya bajeti iliyopita, kuhusu bajeti ya sasa tunao pia utawala bora ambao tumejengewa jengo la Halmashauri ya Wilaya jipya kabisa Shilingi 1,750,000,000.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bajeti ya sasa Serikali inatakiwa ipongezwe sana na wananchi, tumeona kwamba bajeti ni ya wananchi kwa sababu imeongeza fedha za sekta ya kilimo kutoka Milioni 254 mpaka Milioni 954 hii haijapata

kutokea, na sisi tumeona kwa sababu asilimia 75 karibu ya Watanzania wote ni wakulima bajeti hii imewagusa wakulima moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa nina ushauri wangu ninaomba Serikali ifanye jukumu kubwa sana la kufanya kilimo cha umwagiliaji na siyo kilimo cha mitaro, ni kilimo cha kumwagilia kwa mashine na ichimbe mabwawa au ipate maji kwa kukinga kwenye mabwawa ya mito wakati wa mvua au mito ya msimu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji wa mbolea nashauri kwakweli turudi kama tulivyokuwa kule nyuma, tujenge viwanda vyetu vya mbolea ambavyo itafanya mbolea ipatikane kwa urahisi na kuwafikia wananchi na hasa wananchi wa Uyui.

Mheshimiwa Spika, lipo suala la ruzuku nchi zote duniani inatoa ruzuku kwa wakulima wao, tungependa pembejeo za wakulima wa Tanzania zipatikane kwa ruzuku na kwa mtandao wa nchi nzima kwa hiyo tutaongeza tija ya kilimo nchini kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kukuza bajeti ya kilimo hadi kufikia asilimia 10 mwaka 2030, jambo hili ni la kupongezwa na Serikali itilie mkazo, isiwe porojo ya bajeti hii tulione linakua kila mwaka hadi mwaka 2030 tupate asilimia 10 ya Bajeti ya Kilimo iwe sawa na asilimia 10 ya bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchumi wa Bluu, tuna bahati kubwa ya kuwa na mito na maziwa mengi sana lakini bahati mbaya sana hatupati faida ya uchumi wa bluu na hapa ninapendekeza kuwa moja, tumekuwa tunaongelea bandari ya Bagamoyo ipo haja ya kusema sasa tunaijenga hiyo bandari ili iweze kuwa kitega uchumi chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono mawazo ya Serikali katika bajeti hii ya kujenga Bandari ya Bagamoyo, lakini pia tunaomba uendelee ujenzi wa Bandari ya Uvuvi kule Lindi ili tuweze kupata mazao ya uvuvi kutoka meli mbalimbali ambazo zitatua pale.

Mheshimiwa Spika, lipo pia suala la kufufua *TAFICO, TAFICO* lilikuwa ndiyo shirika kubwa linalotengeneza faida hapa Tanzania tukaliuza, sasa nimeenda kutembelea juzi *TAFICO* unaweza ukalia hakuna chochote, lakini Serikali ina nia ya kufufua *TAFICO* ninaiomba Serikali yangu iweke nia ya kuweka fedha za kutosha ili *TAFICO* ilete faida hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika bajeti iliyopita tulikusudia kununua meli nane lakini mwaka huu bajeti imepungua kutoka meli nane hadi meli mbili, hata hivyo ninaipongeza sana Serikali kuwa na wazo la kununua meli za uvuvi mbili. Ahsante sana naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, suala kubwa la mwisho niliongee kwa kituo ni kuhusu kodi, wigo wa kodi ni mdogo sana, watu Milioni Tatu tu ndiyo wanaolipa kodi nchi hii katika watu Milioni Sitini, wigo huo hautoshi! Yapo maeneo mengi ambayo najua kwamba yakifanyiwa kazi yanaweza kuingiza fedha na wananchi wakalipa kodi. Kwa mfano, Sekta ya ulinzi binafsi hapa nchini ilianza na makampuni mawili sasa ina makampuni 3,500, imeajiri watu chungu mzima askari, kama ingesimamiwa vizuri kama ambavyo Serikali inasimamia *SUMA guard* wanapatiwa kazi lakini pia wanalipa kodi na kwa kufanya hivyo kama sekta ingesimamia Makampuni yote 3,500 tungepata fedha nyingi sana lakini hatuwezi kusimamia sekta ya ulinzi binafsi kama hakuna sheria wala *GN* ya kuanzishwa kwa sekta ya ulinzi binafsi.*(Makofi)*

Kwa hiyo, nashauri Serikali sasa ije na nia bora ya kuleta Muswada wa Sekta ya Ulinzi Binafsi hapa Bungeni ili iweze kuundwa mamlaka ya kusimamia makampuni haya ya ulinzi

ya sekta binafsi ambayo itazaa hela nyingi na itakuwa chanzo rasmi cha mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nikushukuru tena na naunga mkono hoja kwa mara ya pili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Isack Mtinga atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani na Mheshimiwa Omar Ali Omar, ajiandae.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti kubwa ya Serikali yetu. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Timu yake yote kwa bajeti nzuri ambayo ipo chini ya Rais wetu, bajeti inayojibu matakwa ya wanyonge wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitachangania mambo kama matatu au manne, lakini kubwa sana ni kilio kikubwa cha wananchi wangu wa Mkalama. Katika bajeti hii yameongelewa mambo mengi lakini mojawapo ni la barabara. Naishukuru Wizara imekuja na mpango mpya wa ujenzi wa barabara kwa mtindo wa *EPC+F,* mtindo huu ni mzuri kwa sababu mkandarasi anajenga barabara kwa fedha zake, Serikali inaendelea kumlipa taratibu wakati wananchi wakitumia barabara. Kwa mtindo huu zimetajwa barabara kadhaa lakini mojawapo ni Barabara ya kutoka Meatu, Mbulu na ikaelekea Daraja la Sibiti kwenda Lalago mpaka Maswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo la barabara hii kuambaambaa pembeni mwa Mkalama kwenda kufuata Daraja la Sibiti ni kufuata daraja hili ili kuvuka Mto Sibiti, lakini kimsingi kabisa daraja hili lilijengwa kwa nia ya kuunganisha Mkoa wa Simiyu na Mkoa wa Singida na ndiko liliko daraja hili. Kwa hiyo, kuambaambaa kwa barabara hii ni kulifuata daraja. Sasa

inasikitisha sana kwa wananchi wangu wa Mkalama kuiona barabara ikiambaambaa pembeni mwa wilaya kufuata daraja ambalo wamelilia kwa miaka mingi mpaka limekamilika, leo linavusha barabara zingine kuunganisha Mkoa wa Manyara na Mkoa wa Arusha wakati wenyewe wa Singida wakitazama kwa mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi si muumini wa kutaka changu kwa kukandamiza wengine, nimwombe Mheshimiwa Waziri kaka yangu, pacha wangu, tunachangia jimbo, wilaya moja baba yetu mmoja Iramba, Waziri yuko Magharibi mimi nipo Mashariki. Tumeacha jina la Iramba Mashariki kulinda historia kwa mawazo ya Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri Barabara hii ya Lalago inayotoka Meatu kwenda Lalago mpaka Sibiti iwepo, ni nzuri sana, inamega kidogo katika jimbo langu, lakini barabara hii ikifika Sibiti inaacha kipande kidogo cha kilometa kama 120 kutoka Iguguno mpaka Sibiti. Katika hizi kilometa 120 kuna kilometa 20 tayari zinajengwa kama matolezi ya daraja, kwa hiyo, zinabaki kama kilometa 105 ukiunganisha kilometa hizi 105 na zile kilometa 389 zinakuwa kilometa 494. Kwa sababu mpango wenyewe ni *EPC+F* ambao mkandarasi anajenga kwa fedha zake kama ataongezea kipande hiki atakuwa hajaathiri bajeti yake Mheshimiwa Waziri, kwa sababu anajenga Serikali inaendelea kulipa polepole. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri barabara hii isomeke kwamba inatoka Karatu inapita Mbulu inakwenda Sibiti inakutana na matawi mawili; tawi moja linakata kwenda Iguguno kwa kupitia katika jimbo langu na hii inaelekea Meatu. Kwa hiyo, inakuwa kilometa 494. Akiikabidhi hii kwa *EPC+F* maana yake atakuwa hajaathiri bajeti yake. Nimwombe sana kaka yangu hii inasabisha sasa hata wapita njia wameanza kudandia barabara hii kama *political mileage* yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana sana Waziri utakapokuja ku-*windup* uje uongeze kipande hiki hakitaathiri bajeti yako na mimi mdogo wako utaendelea kunifanya niendelee. Hivi sasa huko jimboni ni gumzo tupu kuhusu mimi na wewe ambao ni mapacha. Nikuombe sana Waziri, nipo chini ya miguu yako, ingekuwa kanuni hazijazuia hapa ningeanza kugalagala lakini kanuni imezuia. Kwa hiyo nikuombe sana Waziri utakapokuja ku-*windup* ujumlishe kipande hiki na kuwa… *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis wakati mwingine maombi yanakuwa hayasikiki vizuri kwa sababu unaongea na yeye wewe ongea na mimi, mimi ndiyo ananisikiliza yeye.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, naomba ukikazia hii barabara mimi kijana wako angalau nirudi awamu ya pili hapa nitashukuru sana. Baada ya kilio changu hicho sasa niende kwenye mambo ya kitaifa.

Mheshimiwa Spika, hapa tunalia ili tupate kodi na mimi nataka niende kwenye suala zima la kodi. Sheria ya Kodi ya mwaka 2015 kifungu cha 35 kinawatambua walipakodi wadogo wanaopata mauzo kuanzia milioni nne mpaka milioni mia moja. Katika kiwango hiki cha walipakodi hawa sheria imetenga wigo wa madaraja kama manne tu ya walipakodi, kwa maana ya kwamba wanaopata mauzo chini ya milioni nne wanapata kitambulisho kile cha mlipakodi ambaye hasumbuliwi, lakini kuanzia milioni nne mpaka milioni saba wanalipa shilingi laki moja kwenye ule wigo. Kuanzia mauzo ya milioni saba mpaka kumi na moja wanalipa laki mbili na nusu na kuanzia kumi na moja mpaka kumi na nne wanalipa laki nne nusu, madaraja yanaishia hapo lakini tukumbuke wigo unatambua mpaka milioni mia moja. Kwa hiyo, kuanzia milioni kumi na nne kwenda juu yule afisa inabidi sasa achukue kile kiwango cha mauzo, halafu anakipiga asilimia 3.5 anajumlisha na laki nne na nusu. Hapa ndipo

wafanyabiashara wengi wanapoanza kulalamika kwamba wanaonewa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kinachochukuliwa ni mauzo, sasa mtu anaweza kuwa na mauzo ya milioni hamsini, lakini katika yale mauzo ya milioni hamsini kiasi kikubwa ni mtaji wake, faida pale ni ndogo sana, lakini sasa inapigwa pale asilimia tatu inajumuishwa na laki nne na nusu anaambiwa alipe kodi ambayo anaona anaonewa sana. Kwa hiyo, nataka nimshauri Mheshimiwa Waziri kaka yangu alete hii sheria kwanza nikiwatambua wafanyabiashara katika wigo mpana huo wa milioni nne mpaka mia moja, hata haya madaraja sasa yasiwe manne, yaongezeke kwa maana ya tofauti hata ya laki moja moja kuanzia laki moja, laki mbili, laki tatu mpaka huko juu ili yule Afisa wa Kodi anapokuja akiangalia mauzo, mtu ameuza milioni 50 anajua *category* yake ni hii hapa, wala haina mabishano wala haina malalamiko. Kwa hiyo, niombe sheria hii iletwe tuiangalie upya, tuongeze madaraja ili tuondoe huu wigo wa kukadiriana kwa asilimia 3.5 halafu mtu ni mauzo na wala si faida inawaumiza watu wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la *EFD machine; EFD machine* ni chombo kinachosaidia *TRA* kukusanya kodi lakini mpaka sasa *EFD machine* zinaagizwa na wafanyabiashara binafsi na wanapokuja hapa wanawauzia wafanyabiashara wenzao sasa hao wafanyabiashara kwanza hawana ofisi wilayani ofisi, zao zinaishia mkoani na hata hizi *EFD machine* zinapoharibika inabidi wairudishe kwa wakala yuleyule akatengenezewe kwa malipo. Sasa wale wafanyabiashara waliopo vijijini inabidi ahangaike kusafiri mpaka mkoani aende akatengenezewe au kuituma inakaa wiki mbili sasa katika kipindi hiki kwanza Serikali inakosa mapato kwa sababu katika kipindi hiki wakati hii *EFD* inatengenezwa huko wilayani ina maana Serikali inaendelea kukosa kodi na hata hao wafanyabiashara mawakala wanaweza waka-*collude* na wafanyabiashara kwamba

chelewesha chelewesha hiyo mashine huko hata wiki mbili huku yeye anaendelea kuuza na Serikali inakosa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali inakuja inamrudishia, inakata mtu kodi kwa sababu alinunua *EFD machine*, anakatwa kodi kupunguziwa kodi yake, sasa aliyeuza ni mfanyabiashara, halafu Serikali inakuja inampunguzia kodi mwingine kwa kufidia. Kwa hiyo, ina maana yule mfanyabiashara wakala amelipiwa na Serikali *EFD,* kwa nini *TRA* wasiagize *EFD machines* wao wenyewe? Waanzishe vitengo kwenye mikoa kule na kwenye wilaya kiwepo kitengo maalum cha *EFD* ambacho kitakuwa kinahudumiwa na Serikali ikibidi kutugawia bure kama ni kuuza basi itakatwa kwenye zile *session* nne za kulipa kodi katika mwaka, lakini ikae mikononi mwa Serikali, *TRA* wenyewe wamiliki *EFD machine*. Huu mkataba wa kuwaachia wafanyabiasha wengine wawatoze wafanyabiashara wenzao unaumiza na unaiumiza Serikali pia Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nataka niguse kidogo kwenye Bima ya Taifa *NIC,* hili Shirika la Bima. Shirika hili ni la kwetu limeanzishwa na baba wa Taifa shirika hili lililegalega sana leo zimeanzishwa bima nyingi naomba Serikali sasa iipe mtaji shirika hili ili liweze kujiendesha lishindane na mashirika mengine ya bima na wateja kama Wakala wa Serikali, halmashauri zote zinakata bima ziende zikakate kwenye shirika hili ili kulipa mtaji liweze kushindana, tupate gawio tuongeze kodi Serikalini. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Aida Joseph Khenani atafuatiwa na Mheshimiwa Omar Ali Omar na Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali. Nashukuru kwamba mapendekezo ya bajeti yametambua kabisa kwamba kipaumbele ni sekta za uzalishaji, mimi nitajikita kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba changamoto ya ajira Tanzania ni changamoto inayofahamika na ni changamoto ambayo haiwezi kumalizwa kwa mwaka mmoja. Pamoja na kwamba tumeona kwamba fedha imetengwa kwa kiasi kikubwa kwa sasa imeongezeka kwenye bajeti ya kilimo, lakini kwenye Serikali yetu kutenga ni jambo moja na fedha kupelekwa ni jambo lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia leo kwamba kilimo kikawe mbadala au kikapunguze changamoto ya ajira lazima tuachane na utaratibu wa kilimo cha msimu kwa kutegemea mvua, lazima tuelekeze fedha na mitazamo kwenye utaratibu wa umwangiliaji, namaanisha nini? Leo tunachangamoto ya mafuta, tuna changamoto pia ya mazao tunajua msimu wa safari hii siyo mzuri sana, lakini Mungu ametujalia tuna Maziwa Makuu. Haya Maziwa Makuu tunayategemea kwa ajili ya uvuvi peke yake wakati pale tunaweza kuyatumia kwa kuchukua hayo maji yakatusaidia kwenye kilimo cha umwagiliaji, badala ya kulima alizeti mara moja kwa mwaka, tunaweza kulima zaidi ya mara tatu tukijipanga. Kwa hiyo, badala ya kufikiri tu ndani kumaliza changamoto ya mafuta wakati tuna changamoto ya ukali wa maisha tunaweza kutumia mbadala kwa sababu tumepata mafuta ya kutosha ya kupikia, tukauza yakaja kupunguza ukali wa maisha kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nijikite zaidi kwa sababu tumeamua kujiwekeza kwenye kilimo lazima tuje na mkakati wa ziada wa kumaliza changamoto ya mbolea ambayo inawakumba wakulima walio wengi.

Mheshimiwa Spika, unapozungumzia ruzuku kabla hujapeleka ruzuku lazima ujue mahitaji ya mbolea kwenye Taifa ni kiasi gani. Msimu wa kilimo wa mwaka 2021/2022, makadirio yalikuwa ni tani 698,000, lakini hadi Machi zilipatikana tani 480,000, sawa na asilimia 69 peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba nia asilimia 69, lakini katika hiyo asilimia 69 uzalishaji wa ndani ilikuwa ni asilimia 6.0 peke yake. Waziri anapokuja anataka kulinda viwanda vya ndani vinazalisha kiasi gani na mahitaji ni kiasi gani. Changamoto ya hapa ya kwanza tuna taasisi ya kwetu wenyewe ya Serikali ya kuagiza mbolea *TFC, TFC* ina hali mbaya sana, ina changamoto kubwa mbili; changamoto ya kwanza ni suala la mtaji na changamoto ya pili ni madeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ili twende kwenye malengo na matarajio ambayo tumejiwekea ya kufanya mapinduzi makubwa kwenye kilimo ni lazima tuwezeshe taasisi hii, *TFC* inadaiwa bilioni 15 na taasisi za kifedha tofauti tofauti, *TFC* inadaiwa na taasisi za kifedha lakini makampuni ya waagizaji wa mbolea, lakini pia inadaiwa na watoa huduma. Wakati huo *TFC* inadaiwa lakini bado *TFC* yenyewe inadai na hapo unazungumza suala la *management,* ni suala la usimamizi mbovu wa shirika hili.

Mheshimiwa Spika, madeni yaliyopo ambayo *TFC* wakiamua kuchukua hizo fedha wanaweza kumaliza badala yake Serikali ijikite kuwapa fedha ili wajiendeshe kibiashara. Ruzuku ni bilioni tano ambayo wanadai na Serikali

haijapeleka, lakini vyama vya ushirika vinadaiwa bilioni tatu, wadaiwa binafsi bilioni tisa. Hili jambo halihitaji muujiza, linahitaji uthubutu wa wale waliopewa dhamana. Vyama vya Ushirika vipo vinafanya kazi kila siku, ni suala la usimamizi wa waliopewa dhamana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mazingira hayo ambayo yamejitokeza kwenye hili shirika, Mheshimiwa Waziri kama tunataka kuwasaidia vijana wetu waingie kule lazima tujue kwamba sisi hatuna shida ya ardhi, ardhi ipo hatuna shida ya nguvu kazi, shida iliyopo ni namna gani tumeamua kwa dhamira ya dhati kuwekeza kwenye kilimo. Nataka kushauri mambo kadhaa, huko nyuma tulikuwa na mfumo wa uagizaji wa mbolea kwa pamoja. Mfumo uliopo leo hata tukiweka ruzuku haiwezi kuwa suluhisho la changamoto ya mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu wa kwanza lazima turudi kwenye mfumo ule, kwa sababu walikuwa wanaweza kununua kiwandani badala ya kwenda kwenye soko la dunia. Leo ukizungumzia bei ya tani moja kwenye soko la dunia ni Dola 800 mpaka 1,000 kwa tani, lakini kiwandani ni Dola 300 mpaka dola 400. Lengo ni kuwasaidia wakulima na kama lengo ni hilo lazima turudi kwenye mfumo ambao unakwenda kuwasaidia Watanzania ambao ndiyo tunaamini asilimia 70 ni wakulima ambao watakwenda kuinua na kuleta mapinduzi ya uchumi kwenye nchi yetu. Serikali wasikwepe waende wakalipe madeni, walipe hili shirika fedha, walipe hayo madeni kisha lijiendeshe kibiashara, hapo tutakuwa tunakwenda kutafuta suluhisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya muda naomba niende kwenye suala la ukali wa Maisha. Natambua juhudi za Serikali ambazo zimefanyika kwenye ile fedha iliyotolewa, lakini ile fedha imetolewa tulikuwa tunalenga ikamsaidie nani? Tulilenga ikamsaidie mwananchi wa kawaida kabisa, lakini pamoja na fedha hiyo kuwekwa kwenye mafuta, bei ya nauli

haijashuka, bei ya gharama vifaa vyovyote vile ambavyo vinakwenda kwa wananchi wa chini haijashuka, tulikuwa tunataka kuwasaidia wamiliki wa magari au tulitaka kuwasaidia wananchi wa chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kwenda huko lazima tujikite kuondoa tozo ambazo tunaamini hizo ndizo zinapelekea bei kubwa ya mafuta. Kwenye petroli peke yake kuna tozo ya shilingi 920, dizeli 813, mafuta ya taa 577, pamoja na mazingira yote yale kwa kuwa Serikali imeonyesha nia ya kwenda kupunguza ukali tujikite kwa suluhisho la kudumu, siyo la muda mfupi, lazima tutafute suluhisho la muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda na haya mambo tumeshazungumza sana, naomba niende kwenye suala ambalo Serikali imechukua kuondoa ada kwa kidato cha tano na cha sita kwa maana hiyo kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha sita elimu itakuwa bila ada, Wabunge lazima tujue siyo elimu bila malipo ni elimu bila ada. Tunashukuru kwa hatua ya awali ambayo Serikali imechukua, lakini changamoto ya wazazi ambayo inawakumba huko siyo ada peke yake, changamoto kubwa ni utitiri wa michango iliyopo kwa hao wanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kuwekeza kwenda kulinda ndoto za watoto wetu wa Kitanzania na kama hiyo ndiyo nia ya Serikali pamoja na kwamba tunakwenda kumsaidia huyu mtoto kwa kuondoa ada. Naomba nizungumzie hakuna kitu ambacho hata wafanyabiashara wanawekeza ili wapate faida Serikali imeamua kuwekeza kwenye elimu ili kuwalinda wototo wakiwemo watoto wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema wote tunajua kwamba mahakama ilishatoa hukumu juu ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, ilitoa na ikatoa mwaka mmoja sasa ni miaka

mitatu. Tunamshukuru Mungu leo Rais tumempata ni mwanamke na Spika wa Bunge ni mwanamke, wote tunaamini ndoto ya mtoto wa kike, jambo hili litakwenda kupata suluhisho kipindi hiki, naamini ndiyo *dream* yangu. Hata hivyo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama mahakama imeamua na sote tunajua kwamba mahakama ndiyo chombo cha mwisho na lengo letu ni kumsaidia mtoto wa kike, najua kwamba Serikali ina nia njema ndiyo maana imeondoa ada, sasa hiyo nia njema ionekane kwa dhamira njema ya kumaliza kuondoa hiki kifungu cha 13 na cha17 ili kumlinda mtoto huyu wa kike wa Kitanzania tuwapate akina Samia wengi, tuwapate akina Tulia Ackson wengi na akina Aida wengi ili na wao waweze kuweza kufanya kazi ambayo sisi tumeianzisha, kwa kuwa lengo ni kumlinda mtoto wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya muda naomba nizungumzie suala la asilimia 10. Lengo la asilimia 10 ilikuwa ni kwenda kuwasaidia wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. tunahitaji fedha ziongezeke badala ya kuwakopesha watu milioni tatu. Tulitegemea leo Mheshimiwa Waziri wa Fedha aje na utaratibu wa kwenda kuwapatia watu fedha, kufungua viwanda awape milioni 100 kwamba baada ya mwaka mmoja tuone wanawake waliokopeshwa mwaka jana sasa wanaweza kama walikuwa na mtaji wa milioni 10, wanaweza kuwa na mtaji wa bilioni. Hatuwezi kufikiri kurudi nyuma lazima tufikiri kusonga mbele, badala ya kuindoa hiyo asilimia tano, haisaidii chochote. Tunataka fedha ziongezeke kwa sababu mahitaji ni makubwa. Wanawake wapo tunawaona wanavyofanya kazi na wote hapa tunajua kwamba umesema wamekuwa ni waaminifu kurejesha, kama ni waaminifu tukaongeze fedha tuwasaidie wanawake wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Omar Ali Omar, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi na Mheshimiwa Eric James Shigongo ajiandae.

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa jioni hii ya kuchangia katika bajeti yetu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka mchango wangu niuelekeze zaidi kwenye lugha ya Kiswahili. Nianze kwa maneno aliyoyazungumza Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Baba wa Taifa la Tanzania. Mwalimu alizungumza kwamba Uhuru wa Tanganyika ulichochewa sana kwa kutumia lugha hii ya Kiswahili. Kwa hiyo, uliharakishwa kutokana na kutumia lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, lugha ya Kiswahili ilisaidia sana kupata uhuru wa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 1962 lugha ya Kiswahili iliamriwa kwamba ni lugha ya kutumika katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mwaka 1964 lugha ya Kiswahili ndiyo ilitangazwa rasmi kwamba ni lugha ya Taifa. Kwa hali hiyo basi, lugha ya Kiswahili ni moja katika lugha ambayo tunatakiwa Watanzania tuienzi, tuitukuze na tuhakikishe kwamba tunaitumia ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi za Ulaya ikiwemo China, Korea, Uturuki na kadhalika, zimepata maendeleo makubwa kwa sababu ya kutumia lugha zao. Sasa sisi Watanzania bado hatujajikita kutumia Kiswahili kama ni lugha yetu ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunawapongeza sana tena sana Wizara ya Katiba na Sheria kwamba wameanza angalau kuonesha mwanga kwenye hukumu wanazozitoa kwenye Mahakama. Ila ni jambo la kushangaza, Wizara mama ya Elimu ambayo ina mitaala ya kutosha, ina uwezo wa

kubadilisha kuitumia lugha ya Kiswahili katika shule zetu za sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hili linahuzunisha sana, kwa sababu hata somo la historia jamani! Hata somo la historia ya nchi yetu tunalizungumza kwa lugha ya Kiingereza! Lugha ya Wakoloni ambao wametutawala kwa sababu ya kuitumia lugha yao? Ukitaka mtoto ajisikie katika nchi hii, basi azungumze Kiingereza. Ila ukitaka aonekane kadhalilika, basi azungumze lugha ya Kiswahili. Hii ni kuonesha kwamba lugha yetu ya Kiswahili bado hatujaipa kipaumbele katika kuhakikisha kwamba lugha hii ndiyo lugha halisi tunayotakiwa kuitunza na kuhakikisha kwamba tunaitumia ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna wataalam wengi wamezungumza lugha ya Kiswahili. Kama mtunzi mmoja Ibrahim Hussein, alizungumza katika tamthilia yake ya "Mashetani" kwamba Tanzania tunajiamini kwamba mkoloni katuachia kisu sasa, na kisu kile ndiyo tunachotumia kujikata sisi wenyewe. Siku zote tunaona kwamba lugha ya Kiswahili ndiyo lugha ambayo inaweza kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waingereza hao hao wanasema *don't bite the hand that feeds you.* Usiule mkono unaokulisha, ukiula mkono unaokulisha utakulia nini? Naomba sana lugha ya Kiswahili itumike kwamba ni lugha ya Taifa kweli kweli na tuhakikishe kwamba vizazi vyetu tunawarithisha lugha yetu ya Kiswahili kwa kuitumia ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niende kwenye ukurasa wa 75 ambapo Mheshimiwa Waziri wa Fedha alizungumza juu ya mkakati wa uchumi wa bluu. Ni dhahiri kwamba Tanzania tuna watu ambao wanategemea sekta ya uvuvi wasiopungua milioni tano. Watu hawa wote wanategemea sekta ya uvuvi, lakini uvuvi huu unategemea

vyombo vinavyohusika kwenda bahari kuu. Ni-*quote speech* moja ambayo aliitoa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Spika, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli alisema kwamba kipindi cha miaka mitano, mwaka 2020 Novemba 15, alisema maneno haya yafuatayo: Kwamba, kipindi cha miaka mitano sekta ya uvuvi itakuzwa ikiwemo uvuvi wa bahari kuu kwa kununua meli nane zitakazofanya kazi katika ukanda wa Pwani ulioko Zanzibar na Tanzania Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo haitoshi. Mheshimiwa Waziri katika bajeti iliyopita ya 2021/2022 aliizungumza kwa kinywa kipana kwamba tunanunua meli nane za uvuvi. Naomba atakapokuja Waziri, atueleze, hizi meli nane zilipotea wapi kwenye bajeti hii ikawa haionekani? Hazionekani kabisa, wala hakuzungumza kwamba kutakuwa na meli nane zitakazofanya shughuli za uvuvi. Angalau angesema kwamba tushanunua meli mbili zimebaki sita, lakini hata moja hajaizungumza katika bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee katika kilimo cha mwani. Mikoa inayozalisha mwani kwa Tanzania Bara haipungui minne; Lindi, Mtwara, Mkoa wa Pwani, Mafia; nadhani ni mikoa hiyo. Kwa Tanzania Visiwani, Zanzibar, karibu mikoa mitatu inazalisha mwani ikiwemo Mkoa wangu wa Kaskazini Pemba.

Mheshimiwa Spika, asilimia 90 ya wanawake wanajishughulisha na kilimo cha mwani. Ni masikitiko makubwa sana kwamba wanawake hawa wanadhalilika mpaka sura zao zimebadilika, nywele zimenyonyoka vichwani kwa kushughulikia kilimo cha mwani. Nadhani hata kiwanda kile cha kutengeneza nywele bandia kinaweza kikajengwa Pemba sasa, kwa sababu nywele hazimo tena kwa kilimo cha mwani. Zimepotea kabisa kwa sababu ya kilimo cha mwani. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini? Ni kwa sababu mwani haujapewa kipaumbele na nchi yetu. Kilimo cha mwani kinasaidia sana kukuza uchumi wa wanawake nchini, lakini changamoto kubwa ni jinsi bei zinazopangwa na mashirika yanayonunua mwani. Mashirika haya yote, hakuna ambalo linawaonea huruma wakulima wa mwani. Maana wananunua kati ya Shilingi 600/= mpaka Shilingi 1,800/=, kiwango kidogo kabisa cha fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake wakae kutafakari na kupanga bei ya mwani kama vile inavyopangwa bei ya korosho, kahawa, karafuu kwa kule Zanzibar na maeneo mengine. Hii itaweza kuwakomboa wanawake wabaki salama kwenye mwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hali hiyo, mwani huu tunauuza sisi kama malighafi. Inakera sana. Tanzania ni nchi ya viwanda, ina uwezo wa kujenga viwanda vidogo vidogo, lakini mpaka sasa hivi hakuna kiwanda hata kimoja kinachochakata mwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwani unatusaidia sana kwa kutengeneza mboga mboga, mwani ni chakula, mwani tunatengenezea mafuta, lakini hutoamini rasilimali inayotoka kwenye mwani. Mwani unatengeneza mpaka hii mitambo yetu wanaume tunayoitumia inatokana na kilimo cha mwani. Hii ni kuonesha kwamba mwani kumbe una faida kubwa kwa nchi yetu. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Omar, hoja ya msingi sana hiyo, dakika moja malizia muda wako umeisha. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Penye watu wazima wengi hufahamu lugha nzuri. Mitambo ya wanaume mnaijua, na mkifanya mchezo basi wanaume tunaweza tukapoteza mabibi zetu kwa sababu ya mitambo haifanyi kazi kutokana na kwamba hatuutumii mwani vya kutosha. Kwa hiyo, mwani una faida kubwa na tuendelee kuutumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi/Vicheko)*

**SPIKA:** Nilikuwa naangalia Wabunge wanaopiga makofi humu ndani. Mheshimiwa Omar, kuna umuhimu wa kuleta huo mwani na kufanya maonesho hapa Bungeni, ni muhimu sana. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, atafuatiwa na Mheshimiwa Eric James Shigongo. Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah ajiandae.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nitaanza mchango wangu kwa kuzungumzia suala la usimamizi wa fedha za umma. Kama kuna jambo ambalo inabidi tuliangalie kwa makini na ikiwezekana tulifanyie mabadiliko ni muda ambao CAG na Bunge tunautumia katika kufanya ukaguzi, kujadili na kuchakata hizi taarifa za ukaguzi na hatimaye kutoa maelekezo na maagizo kwa Serikali juu ya matumizi yasiyofaa kwa fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ilivyo sasa, kuanzia mwisho wa mwaka wa fedha tarehe 30 Juni, muda ambao Wakuu wa Taasisi, Maafisa Masuuli wamepewa kuandaa taarifa za mwaka na baadaye kuziwasilisha kwa CAG na CAG

anazikagua na halafu anawasilisha taarifa kwa Mheshimiwa Rais na baadaye Bungeni; baada ya hapo, Kamati za Bunge za *LAAC* na *PAC* zinajadili na baadaye taarifa zinaletwa Bungeni, Bunge linajadili na kutoa maagizo juu ya mambo yaliyopatikana, tunatumia miezi 17.

Mheshimiwa Spika, huu ni muda mrefu mno, kwamba fedha za umma zimetumika na mtu ambaye ametumia vibaya fedha za umma anakuja kujua kwamba ametumia vibaya na maagizo yanatoka baada ya miezi 17. Muda huu ni mrefu mno na kuna haja ya kufanya mabadiliko. Maafisa ambao sio waoga wanakuwa na ujasiri wa kufanya matumizi mabaya ya fedha za umma kwa sababu wanajua mpaka aje agundulike na maelekezo yatoke ni miezi 17 ambao ni muda mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ilivyo sasa ni kwamba mwaka wa fedha unaisha tarehe 30 Juni na baada ya hapo, Sheria ya Ukaguzi wa Umma kifungu cha 31 kimewapa Maafisa Masuuli wa Taasisi zote za Serikali miezi mitatu kuanzia tarehe moja Julai mpaka tarehe 30 Septemba kuandaa hesabu za mwaka ili wazipeleke kwa *CAG* kukaguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hali ilivyo sasa ya kiteknolojia, taasisi zote za Umma zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa zinafanya *transactions* zote za kifedha kwenye mifumo. Kama ni makusanyo ya mapato, kwa mfano, Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ni makusanyo ya ushuru wa mazao, ushuru wa masoko, ushuru wa stendi, yote yanafanyika kwenye mifumo. Kama ni malipo ya wakandarasi, wazabuni, yote yanafanyika kwenye mifumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tujiulize, kwa hali ilivyo sasa, pengine hii Sheria ya Ukaguzi wa Umma ilitungwa wakati hii miamala inafanyika *manually* kwa mikono, lakini kwa hali ya kielektoniki ilivyo sasa, kuna haja gani ya Afisa Masuuli ambaye amemaliza mwaka tarehe 30 Juni, kuna haja gani

ya kumpa miezi mitatu yote hiyo kufunga hesabu? Wakati sasa hivi kwa mifumo ya kihesabu iliyopo kwenye taasisi za umma unaweza ukafunga hesabu za mwaka kwa siku mbili tu au siku moja, *is a just* ku-*press burton* tu. Kwa hiyo, hakuna sababu yoyote kwa *level* ya teknolojia iliyopo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuboresha mifumo, na sasa hivi taasisi zote zinatumia mifumo. Kwa hiyo, hakuna sababu yoyote ya Maafisa Masuuli kupewa miezi mitatu kufunga hesabu za mwaka, ni muda mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ushauri wangu kwenye eneo hili ni kwamba tubadili kifungu Na. 31 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ambacho kinampa Afisa Masuuli miezi mitatu, turudishe mpaka angalau mwezi mmoja, ingawa najua hata siku mbili zinatosha kuandaa hesabu ambazo zimeandaliwa kwenye mfumo, lakini tumpe mwezi mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi baada ya miezi mitatu, taarifa ikifika kwa *CAG* anatumia miezi sita kufanya ukaguzi mpaka mwishoni mwa mwezi Machi ambapo ndiyo anakabidhi taarifa kwa Mheshimiwa Rais na baadaye inakuja Bungeni. *CAG* sasa hivi amewezeshwa na naipongeza Serikali kwamba imeji- *commit* kumwezesha na kumpa fedha. Kwa hiyo, akiwa na *workforce* ya kutosha na mifumo mizuri ya kufanya ukaguzi, hana haja tena ya kutumia miezi sita, anaweza kutumia miezi mitatu na kufanya ukaguzi na baada ya hapo kwa Mheshimiwa Rais na baadaye Bungeni na Kamati zetu za *LAAC* na *PAC* kuweza kuchakata na baadaye kujadiliwa na kutolewa maagizo ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yangu ambayo yatapunguza hii *process* kutoka miezi 17 mpaka miezi nane, ni kwamba tubadilishe kifungu cha 31 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Maafisa Masuuli wapewe mwezi mmoja badala

ya miezi mitatu, CAG apewe miezi mitatu badala ya miezi sita na taarifa ije Bungeni na *immediately LAAC* na *PAC* waanze kukagua na maagizo yatoke. Kwa hiyo, tutakuwa tunatoa maagizo kwa muda wa miezi nane badala ya miezi 17 ya sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza bajeti hii kwa kuongeza bajeti ya kilimo. Sisi Wabunge tunaotoka vijijini shughuli yetu kuu ya wananchi wetu ni kilimo. Kwa hiyo, kuongeza bajeti kutoka Shilingi bilioni 294 mpaka Shilingi bilioni 954 ni jambo la kupongezwa na hapa nawapongeza sana. Shilingi bilioni 150 ya ruzuku ya mbolea itakwenda kuwasaidia wakulima wetu kupata mbolea hii kwa bei nafuu na kuongeza tija ya kilimo chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nimeliona ni mapendekezo ambayo yamo kwenye hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri ambayo yamependekeza kubadilisha kifungu cha 6(1) ambacho kinapendekeza kuhamisha majukumu ya usimamizi wa mifumo ya mawasiliano kutoka *TCRA* kwenda *TBS*.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwa Mbunge mimi nilikuwa mtumishi wa *Airtel* ambayo ni Kampuni ya Simu. Ushauri wangu hapa ni kwamba jukumu la kusimamia mifumo ya mawasiliano libaki *TCRA* na kama kuna maboresho yanahitajika, basi yafanyike huko huko *TCRA* badala ya kupeleka *TBS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niungane na Waheshimiwa Wabunge, hotuba imezungumzia kuwezesha kampuni zetu binafsi ili ziweze kushindana na kampuni nyingine kwa mfano Shirika la Bima la Taifa ambalo linashindana na kampuni nyingine binafsi za bima, liwezeshwe kimtaji na kiuwezo kwa maana ya watumishi ili Shirika hili la Bima la Taifa liweze kutoa huduma za tija ambazo zinaweza kushindana na kampuni

binafsi na hatimaye kuweza kutoa huduma za kiufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono uamuzi wa kufuta ada Kidato cha Tano na Kidato cha Sita, jambo hili litapunguza mzigo kwa wazazi ambao wanahangaika sana kuhakikisha kwamba watoto wao wanapata elimu ambayo inahitajika sana, pia naungana na Wabunge wote ambao wamependekeza asilimia 10 ibaki vilevile ilivyo, labda kama yatatoka maelekezo ya kutosha lakini kama yalivyo kwamba asilimia tano zitumike kujenga miundombinu ya ujasiriamali, kwa tunaotoka Halmashauri za eneo kubwa la vijiji ambavyo viko mbalimbali hoja hiyo haiwezekani kabisa. Kwa hiy,o tunashauri asilimia 10 zibaki kama zilivyo na ikiwezekana hata ziongezwe.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nipongeze pia Serikali kupandisha bajeti ya mifugo na uvuvi, wote tunafahamu kwamba mwaka huu ambao tunamaliza tulikuwa na Bilioni 168 lakini tunakwenda kupata Bilioni 268.

Mheshimiwa Spika, nakushuru naunga mkono hoja asilimia 100, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Eric James Shigongo atafuatiwa na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mheshimiwa Anton Albert Mwantona ajiandae.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kunipa nafasi ya kuwa ndani ya Bunge hili Tukufu, nafahamu dhahiri kabisa kwamba siko hapa kwa sababu nina akili nyingi na uwezo mkubwa, bali niko hapa kwa sababu Mwenyezi Mungu aliamua niwe mahali hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mabadiliko anayoyafanya katika Taifa letu, ukitembelea Buchosa leo utashangazwa na uzuri wa barabara, utashangazwa na miradi mingi ya maji yenye thamani yenye karibu Shilingi Bilioni 15, utashangazwa na madarasa mazuri vijana wetu wakisoma katika hali nzuri kabisa, napenda nimpongeze sana Rais wetu na ninaipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, mimi huwapima watu na uwezo wao wa akili kwa matendo, nirudie tena uwapima watu uwezo wao wa akili kwa matendo yao. Mara ya mwisho niliongea hapa nikasema tuna *best President, intelligent President and clever President*, nilisema! Narudia tena leo maneno haya leo kuyasema na nitatoa sababu mtu yeyote ambaye ana mashaka na uwezo wa Rais wetu anisikilize kwa makini.

Mheshimiwa Spika, Rais wetu amefanya jambo moja kubwa sana kuonesha kwamba ana uwezo mkubwa, jambo hilo niuwekaji wa *post code* bajeti ya *post code* ilikuwa Bilioni 720 samahani, lakini alivyopelekewa mezani bajeti ile alikatakata mpaka Bilioni 28, ni mtu mwenye akili peke yake anaweza akafanya jambo la namna hiyo. Katika hali ya kawaida ukiletewa ripoti mezani huwa tuna tabia ya kupitisha tu, lakini Rais wetu alikata mpaka ikabaki Bilioni 28.

Mheshimiwa Spika, ninapozungumza na wewe leo tayari mradi wa kuweka *post code* nchi nzima umekamilika kwa asilimia 95. Narudia tena kusema kwa matendo haya nina kila sababu ya kusema *we have the best President, intelligent President, clever President na smart President*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwa bajeti yake, nimeona ni bajeti ya kimapinduzi ameenda kuendelea kufanya mambo makubwa katika Taifa letu, nimuombe Mheshimiwa Waziri ajiepushe na kufanya vitu vinavyofanya awe *popular*

badada ya kufanya vitu ambavyo vitamfanya vitu sahihi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri asiguse kabisa ile asilimia 10 aiache kama ilivyo hilo la kwanza, asiguse kabisa asilimia 10 aiache kama ilivyo na ikiwezekana aiongezee. Jambo lingine la muhimu sana ambalo nataka nilichangie katika bajeti hii ya leo ni kwamba tunakusanya fedha nyingi sana tunakopa fedha tunakusanya fedha kwenye kodi tunapeleka kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu, lakini kuna kitu kimoja muhimu sana ambacho mimi naona kama tunakisahau ni ufuatiliaji wa fedha zetu tunakozipeleka, *monitoring and evaluation*.

Mheshimiwa Spika, Dada yangu Mheshimiwa Eng. Ulenge aliwahi kuzungumza siku moja hapa ndani suala la *monitoring and evaluation,* ufuatiliaji na tathmini ni changamoto kwenye Taifa letu. Tunakusanya fedha nyingi tunapeleka huko kwenye Halmashauri zetu tunasahau kwamba kuna watu ambao hawaogopi fedha ya umma kabisa! Wanasubiri fedha ya umma ije waitafune. Niseme bila kupindisha maneno kwamba Halmashauri zetu ni mchwa wa fedha za umma narudia tena halmashauri zetu ni mchwa wa fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawaomba kama Taifa ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, tujue kabisa ya kwamba tunao wajibu wa kufuatilia fedha zetu ambazo tumezipeleka kwa wananchi, Rais wetu ana nia njema ya kuleta maendeleo lakini hatufuatilii fedha zetu. Mfano, mdogo wangu Mheshimiwa Aweso alienda Handeni, nikamsikia anasema nionyeshe bwawa akarudia nionyeshe bwawa hakuna bwawa akaoneshwa dimbwi Milioni 600 zimeliwa.

Mheshimiwa Spika, sijakaa sawa nikamuona Kaka yangu Mheshimiwa Prof. Mbarawa na yeye analalamika kwenye

*television* ya kwamba nioneshe *temporary office, temporary office* imekuja kuonekana ya Milioni 100 ni kibanda cha mabati! Sijakaa sawa nikamuona ndugu yangu Mheshimiwa Musukuma Kaka yangu Kasheku analalamika kwamba kule kwake bati ya kununuliwa Shilingi 40,000 imenunuliwa Shilingi 72,000. Sijakaa sawa nikamuona Kaka yangu ambaye ninamheshimu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Kassim yuko *MSD* anasema vifaa vinavyotakiwa kununuliwa kama sijui ilikuwa Milioni 20 kimenunuliwa kwa Milioni 129.

Mheshimiwa Spika, hii ni mifano michache tu ambayo tumeiona kwenye *television,* iko mifano mingi sana ambayo hatuioni ya pesa za umma zinatafunwa na watu wenye nia mbaya na maendeleo ya nchi yetu! *Monitoring* na *evaluation* naungana na Dada yangu Mheshimiwa Ulenge leo hayupo kuiomba Serikali yangu iimarishe ufuatiliaji na tathmini ya pesa zinazoenda vijijini, tofauti na hapo tutakuwa tunapeleka fedha zinaishia mikononi mwa watu wachache, zinatafunwa, hakuna kinachofanyika. Hatuwezi kutimiza ndoto ya nchi yetu kama watu wachache wanatuvurugia *movement* yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilisoma ripoti moja na ilinisikitisha sana ripoti hiyo ya *transparence international* ambayo walisema dola bilioni 50 zinatoka Afrika kila siku kwenda mabenki ya Ulaya, nikasoma chini yake nikakuta wanatamka jambo la kusikitisha kabisa kwamba kiasi cha dola bilioni 4.5 zinapotea kama mapato katika Taifa la Tanzania, fedha ambazo zingethibitiwa zisipotee zingejenga Vituo vya Afya 1,730 kwa kituo kimoja milioni 600. Zingethibitiwa zisipotee zingeweza kujenga kilometa 5,300 za lami. Najenga hoja ya kwamba fedha zinazopotea zikidhibitiwa zisipotee maendeleo yetu yatakwenda kwa kasi kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunafanya nini kama Taifa; Kwanza, nilizungumza tulipoitwa Ikulu na Mheshimiwa Rais kule Chamwino, nikasema Tanzania kama mataifa mengine

ya Afrika yalivyo yanasumbuliwa na ugonjwa mmoja mbaya unaitwa *Institutional failure*. Taasisi zetu zime-*fail*, zime-*fail* tafsiri yake ni lazima ziimarishwe, kama taasisi zinafanya kazi zinavyotakiwa Mheshimiwa Aweso – Waziri wa Maji asingeweza kulalamika pale kuhusu bwawa, pale alipolalamika Mheshimiwa Aweso hakuna Mkurugenzi? Hakuna *DC?* Hakuna TAKUKURU?

**SPIKA:** Sasa ngoja Mheshimiwa nilikuwa nimekuacha ili uende na huo mtiririko lakini sasa wacha nikuongoze kidogo, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Aweso ni Mheshimiwa Aweso awe shemeji yako, kaka yako humu ndani ni Mheshimiwa, kwa sababu la sivyo tutafika mahali watu wanaanza kama mke wangu alivyosema. Sasa ngoja tuite kwa kadri Kanuni zinavyotuongoza humu ndani wote ni Waheshimiwa kwa sababu ukisema tu neno Aweso bila Mheshimiwa Baba yake anaitwa Aweso, sasa tunakuwa hatujui unamuongelea yupi unamuongelea huyu Waziri au yule mwingine. Ahsante sana.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, naomba nimuombe sana radhi mdogo wangu Mheshimiwa sana Jumaa Aweso kwa kumtaja tu kama Aweso na Mheshimiwa Spika nimeyapokea maelekezo yako vizuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niseme *what do we do?* Nilizungumza alipotuita Mheshimiwa Rais Ikulu kwamba, tatizo kubwa la Tanzania na nchi za Afrika ni *Institutional failure,* taasisi zimeferi taasisi zingefanya kazi yake zisingemsubiri Mheshimiwa Aweso- Waziri wa Maji, zisingemsubiri Mheshimiwa Waziri Mkuu, palepale kuna DC, Mkurugenzi, kuna watu wa TAKUKURU wangefanya kazi yao sawasawa wasingemsubiri Mheshimiwa Waziri Mkuu au Mheshimiwa Waziri wa Maji aje.

Mheshimiwa Spika, naomba sana tuimarishe taasisi zetu zitimize wajibu wake kule chin,i tunafanyaje kwenye suala zima la mapato ya umma? Kwenye mapato ya umma tuimarishe TAKUKURU. Nilikaa wiki mbili zilizopita na Mkurugenzi wa *PCCB* ofisini kwake nikawa nazungumza naye nabadilishana naye mawazo, tunafanyaje tuweze ku-*control* tuweze kudhibiti rushwa katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, tulipoanzisha TAKUKURU ilianza mwaka 1974 lakini hata 1991 ilikuwa inaitwa *(PCB) Prevention of Corruption Bureau,* kazi yake ya kwanza TAKUKURU kabisa ya mwanzo kabisa ilikuwa ni kuzuia rushwa mwaka 2007 tukabili sheria tukaita *Prevention and Combating of Corruption Bureau (PCCB)*. Tukaongeza suala la *combating* maana yake sasa ni kuzuia na kupambana na rushwa, TAKUKURU wamesahau suala zima la *prevention* wamejielekeza kwenye *combating* kwenye kupambana, wanazo kesi nyingi sana hivi sasa lakini bado kuna kesi nyingi zinatokea.

Mheshimiwa Spika, nataka TAKUKURU wawezeshwe, tuwawezeshe kufanya suala la *prevention* kuzuia rushwa wamelisahau hiyo *task.* Mheshimiwa Waziri amezungumza juzi hapa, akasema amewawezesha *CAG* kwa kuwapa fedha nyingi, namuomba Mheshimiwa Waziri hizo fedha badala ya kuzipeleka *CAG* awapelekee *PCCB* ili wawezeshwe kwa mafunzo, kwa idadi kubwa ya watu wa kufanya kazi maana yake *labor force,* mwisho wa siku tuweke sheria ya kwamba fedha inapokwenda kwenye Halmashauri yoyote iwe *mandatory* iwe ni lazima *PCCB* wapate kopi kwa ajili ya ufuatiliaji. Narudia tena iwe ni lazima *PCCB* kupata *copy* kwamba tumepeleka fedha Milioni 600 na isome ya Kituo cha Afya kwa hiyo TAKUKURU wapokee kwa ajili ya ufuatiliaji.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa ninavyozungumza ni hiyari kuwapelekea TAKUKURU. Naomba niunge mkono hoja ahsante kunisikiliza.*(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah Mheshimiwa Anton Albert Mwantona Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo ajiandae.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa uwasilishaji wa bajeti yake ya Wizara ya Fedha na Mipango ambayo imeelekeza nguvu kubwa katika sekta ya kilimo, mifugo, uvuvi, nishati lakini kutekeleza miradi ya kielelezi, tunajua ya kwamba Serikali ina lengo kubwa la kukuza uchumi lakini hatimaye kukuza ajira katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kwanza kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuridhia kutekeleza mradi mkubwa wa *LNG* lakini kwa kuridhia kusaini mikataba kwa wabia wetu kwa makubaliano yale ya awali. Wananchi wa Lindi tumepata faraja kubwa sana na tumepata matumaini makubwa ya kutekelezwa kwa mradi mkubwa ambao utanufaisha Taifa letu katika kukuza uchumi, lakini katika kukuza ajira katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tuna kila namna ya kuhakikisha kwamba tunaendelea kumuunga mkono Mheshimiwa Rais wetu kwa yale mema mazuri anayotuletea kwa faida ya Taifa letu. Katika mkutano wa kusaini mkataba yako maagizo ambayo Mheshimiwa Rais aliyatoa, naomba niwakumbushe watakao simamia katika utelekezaji.

Mheshimiwa Spika, katika agizo lake la kwanza alisema kwamba wahakikishe kwamba barabara zinaboreshwa katika eneo la mradi wa *LNG*, katika agizo lake la pili aliagiza ujenzi wa hospitali za kisasa katika eneo la mradi. Ninashukuru ya kwamba Manispaa yetu ya Lindi tuliiongeza baada ya kupata fedha za ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, tulielekeza moja kwa moja ikajengwe katika eneo hili la Kata ya Mbanja kule Kikwetu ambako mradi wa *LNG* utatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, pia agizo lake lingine aliagiza ujenzi wa shule nzuri za kisasa lakini na agizo la nne ni huduma ya maji kupelekwa katika eneo hili ambako mradi wa *LNG* utatekelezwa, mimi ninaamini kwamba Mheshimiwa Waziri wa Maji ni msikivu sana na hata hakikisha kwamba maji yanafika katika eneo la Kata ya Mbanja. Agizo lake la tano ni kuhakikisha kwamba huduma ya umeme inafika katika eneo la mradi wa *LNG,* pia sekta ya mawasiliano kuhakikisha kwamba mawasiliano pale yanafika na agizo lingine la mwisho ni kuhakikisha kwamba upimaji wa ardhi kwa ajili ya matumizi bora ya ardhi ufanyike.

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru sana Serikali kupitia Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan kuridhia katika Halmashauri ya Manispaa ya Lindi kupata mkopo wa Bilioni Moja katika kuhakikisha kwamba tunakwenda sasa kupima ardhi kwa ajili ya matumizi bora ya ardhi na fedha hizi zimefika wakati muafaka sasa wa kuhakikisha kwamba Lindi Manispaa sasa tunakwenda kuwekeza katika upimaji wa ardhi na kukaribisha sasa uwekezaji katika maeneo ya Lindi Manispaa.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo hayo yakuboresha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, tunazo Km. 2.4 tumefanya maombi maalum kuhakikisha kwamba kutoka barabara kubwa ya lami kwenda ilikojengwa Hospitali ya Wilaya tuweze kupata fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Km.

2.4 tunaboresha na huduma ya afya iweze kufikiwa kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, bado tuna ujenzi wa hospitali ya Rufaa ya Mkoa, nayo kutoka barabara kubwa kwenda kule ndani ni kilometa 2.5 tumefanya maombi maalumu kuhakikisha kwamba barabara hiyo inaboreshwa. Pia tuna ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Mkoa ambayo imeshakamilika tuna Km. 300 kutoka barabara kubwa ya lami kuekelekea kule kwenye Mahakama hiyo, tumefanya maombi hayo maalum kuhakikisha kwamba tunaendelea kuboresha eneo hilo kuhakikisha kwamba wananchi wetu waendelee kupata huduma bora lakini tuhakikishe kwamba uwekezaji huu wa mradi mkubwa wa *LNG* tunakwenda nao sambamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufuta ada, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wenzangu wameongelea kuanzia Darasa la Kwanza, *Form Four, Form Five* mpaka *Form Six* ni jambo jema sana kuhakikisha kwamba watoto wetu sasa wanapunguziwa mzigo wa mkubwa wa kushindwa kumaliza masomo kwa kushindwa kulipa ada, kwa hiyo mimi ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti yetu tunajua kwamba mwaka huu ni mwaka wa sensa, na muda siyo mrefu mwezi wa Nane Tarehe 23 maana yake tunaingia kwenye sensa, muda uliobakia kufanya maandalizi ni muda mfupi sana na siyo muda mrefu, tukimbizane na wakati uliobaki tuhakikishe kwamba fedha inafika kwa wakati na vifaa ili kuhakikisha kwamba tunafanikiwa wananchi wetu kuingia kwenye kuhesabiwa ili tuweze kupata takwimu halisi.

Mheshimiwa Spika, ninasema hivi kwa sababu Lindi Manispaa tumeathirika na sensa ya mwaka 2012, wananchi

wengi hawakuhesabiwa tuliingia kwenye matatizo makubwa na ndiyo maana hatupati fedha nyingi za maendeleo katika eneo letu la Lindi Manispaa, kwa hiyo nina kila namna ya kusisitiza fedha pamoja na vifaa vifike kwa wakati kuhakikisha kwamba tunajipanga kuingia katika tukio hili la sensa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la haki na usalama wa raia wetu. Kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutuwezesha fedha zaidi ya milioni 900 kujenga Kituo cha Polisi Daraja A. Wilaya ya Lindi ina Majimbo Matatu na tulikuwa hatuna Kituo cha Polisi cha Daraja A, kwa hiyo nimshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais wetu, kutuwezesha fedha hizi kujenga Kituo kikubwa cha Polisi cha Daraja A. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, licha ya hayo, bado tuna changamoto, ni muhimu sana kuweka Vituo vya Polisi kwenye Tarafa, Vituo vya Mahakama kwenye Tarafa ili iwe rahisi wananchi wetu kuweza kupata huduma hizo kwa wakati. Inapotokea kwenye Tarafa kunakosekana kuwa na mahakama, ni mzigo mkubwa na kumfanya mwananchi huyu asafiri umbali mrefu kwenda kupata huduma ya mahakama. Kwa hiyo nina hakika yako maeneo mengi ambayo hayana mahakama na hayana vituo vya polisi.

Mheshimiwa Spika, tunaona sasa hivi wezi na vibaka wamekuwa wengi sana kwa kukimbilia hatuna kwa wakati, kwa sababu vituo vya polisi vimekuwa mbali mno na maeneo ambayo wananchi wanaishi. Kwa hiyo tufanye kila namna kuhakikisha kwamba katika maeneo yetu ya Tarafa tupate vituo vya polisi lakini tuwe na mahakama zile za mwanzo kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanaendelea kupata haki na huduma huko wanakoishi bila kutembea umbali mrefu.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la *TRA*, suala la kulipa kodi ni uzalendo na bila kodi maana yake hatuwezi kuendesha nchi bila kuwa na mapato ndani ya nchi yetu. Hata hivyo, niseme kwamba maduka mengi ukipita kununua vifaa suala la utoaji wa risiti wa *EFD machine* hazipo, limetoweka kabisa. Niwaombe sana ndugu zangu wa *TRA* kuhakikisha kwamba wanafanya kazi kupita huko na kukumbushana na kuhakikisha kwamba wafanyabiashara wanaendelea kutumia mashine hizi za *EFD* kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, tumeona changamoto kubwa ya makadirio ya viwango vya kodi, mathalani mtu ana mtaji wa milioni 50, lakini kwa mwaka mzima anapelekewa kodi ya milioni 200. Sasa unajiuliza nina mtaji wa milioni 50, nawezaje kulipa milioni 200! Kwa hiyo, kwanza nashukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameliona hili na kwenye taarifa yake ameliandika, tuhakikishe kwamba tunalisimamia suala la uzalendo ni suala muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika eneo ninaloishi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Muda umeshaisha Mheshimiwa kengele ya pili imegonga.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nizungumzie suala la kodi ya mabasi ya abiria na malori ya abiria, hili linatupa maswali mengi

**SPIKA:** Kengele ya pili imegonga Mheshimiwa.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wakati ana-*wind up* atuambie ni kwa

namna gani tunaweza kusimamia hili kwa sababu mabasi yanatofautiana ukubwa wa mabasi na abiria na mizigo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, atafuatiwa na Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo na Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, ajiandae.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Spika, nami pia niungane na wenzangu kumshukuru Mungu kwa kutupatia afya, lakini pia nimshukuru Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan, Waziri wa Fedha, Naibu wake na watumishi wote wa Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kutoa shukrani za pekee, wananchi wangu wameniambia nije nitoe shukrani kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miradi inayotekelezwa katika Jimbo langu la Rungwe. Ni miradi mingi inatekelezwa, lakini kwa upekee sana naomba nitaje miradi michache kwa sababu ya muda ili wananchi wangu wasikie kwamba nimewafikishia salamu zao.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Rungwe pamoja na mimi mwenyewe tumefurahi sana hasa baada ya Serikali kusikia kilio chetu, Mbunge mimi wa Rungwe wa Kyela, lakini pia Wabunge wa Viti Maalum dada zangu pale wa Mbeya tulivyokuwa tunapigania Mradi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira. Serikali imeshapata mteja ambaye atanunua makaa ya mawe kutoka Kiwira tani 60 kila mwezi. Upatikanaji wa mteja huyo utatusaidia sana watu wa Rungwe, Kyela, Ileje kupata ajira lakini pia kupata uchumi katika maeneo yetu. Vijana wengi ambao wako katika maeneo yetu walikuwa hawana ajira, tunategemea kwamba baada mradi huu kuanza ajira nyingi zitapatikana katika maeneo yetu na vijana wengi wataajiriwa.

Mheshimiwa Spika, pia wameniambia nilete salamu na shukrani pekee kwa Mradi wa Maji katika Mji wetu wa Tukuyu kwa Wizara ya Maji, tumepewa juzi milioni 402 kufikia bilioni moja na milioni 102 ambapo mradi mzima una bilioni 4.5. Sasa hivi tutapata mabomba ya kutosheleza kutoka moja kwa moja katika chanzo mpaka Tukuyu Mjini. Kwa hiyo tuna uhakika sasa hivi maji yatapatikana ndani ya muda mfupi, hiyo ni shukrani ya pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, katika bajeti hii tumewekewa milioni 90 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu kwa barabara inayotoka Kimo kuelekea Iponjola, Ikuti mpaka Ileje. Wananchi pia wanashukuru sana kwamba hii barabara ni dalili njema, kwamba inaanza kujengwa barabara hii kwa kiwango cha lami kutoka pale Kimo – Iponjola - Ikuti mpaka Ileje, hiyo ni shukrani ya pekee pia kwa Serikali hii.

Mheshimiwa Spika, pia kwa upande wa *TARURA* tumepewa tayari milioni 880 kwa barabara ambayo ilikuwa ni sumbufu sana kutoka Kijiji cha Kata ya Malindo, Kijiji Kapugi, kuelekea Lienje mpaka Kihobo Juu kwenye Kata ya Ikuti. Hizo ni shukrani za pekee sana kwa Serikali hii kwamba ni sikivu lakini pia imewafikiria wananchi kutatua matatizo yao ambayo yapo katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, niongee kidogo kwenye bajeti hii ya 2022/2023, nikipongeza Serikali kuongeza bajeti kwenye upande wa kilimo. Ongezeko ni kubwa ambalo litaenda kufanya mapinduzi makubwa kwenye kilimo. Mwaka jana tumepata shida kubwa sana kwa wananchi, tulivyokuwa tunafanya mikutano katika maeneo mbalimbali ya wananchi wetu tulikuwa tunaulizwa sana kuhusu bei ya mbolea. Bei ya mbolea kwa wastani laki moja mpaka laki moja na arobaini na hiyo imepelekea mwaka huu kilimo kikawa kigumu, watu wachache ndio waliweza kulima na hivyo tunategemea mwaka huu mazao yatakuwa ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, katika suala hili naomba niishauri Serikali kwamba, tudhibiti chakula hicho kidogo tulichokipata, tuhakikishe kwamba utoaji wa chakula chetu cha nje kinatoka katika hali ambayo ni nzuri tukizingatia hasa usalama wa chakula hapa nchini. Hilo nimeona niseme, lakini kwa mwaka huu sasa kwa sababu tumeweka ruzuku kwenye mbolea uwezekano mkubwa ni kwamba mbolea itashuka na wananchi wengi watalima na hivyo tutapata chakula kingi cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, Rungwe ni wafugaji wakubwa sana wa ng'ombe wa kisasa, tunafanya *zero grazing*, tunafugia ng'ombe ndani katika mazizi kwa kuwaletea chakula ndani, lakini tatizo kubwa la Rungwe na maeneo mengine ambayo wanafanya utaratibu huo wa ufugaji ni kwamba bei ya maziwa ni ndogo kwa wafugaji wetu. Tunaomba Serikali iangalie kwa jinsi gani itaongeza thamani ya mazao ya maziwa, lakini pia kuongeza soko mazao ya maziwa katika maeneo yetu. Rungwe ukifuga ng'ombe, lazima utumie lita 100 kununua mfuko mmoja wa pumba, pumba wanauza shilingi 70, maziwa yanauzwa kwa Sh.600 mpaka Sh.650. Sasa ukiangalia, kwa kweli wananchi wanapata shida, wanafuga mifugo yao katika gharama za juu lakini bei za maziwa ziko chini, kwa hivyo inawakatisha tamaa wengi katika ufugaji wao.

Mheshimiwa Spika, niende katika Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani. Mheshimiwa Waziri amesema hapa kwamba Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kinaongezewa *independence* zaidi kwa kupewa *vote* yao, lakini pia kwamba wao watakuwa wanaripoti moja kwa moja kwa *Internal Auditor General* ili *at least* zile ripoti zao ziweze kwenda vizuri na zisiingiliwe na mtu yoyote, ni jambo jema. Hata hivyo, naomba tuangalie pia katika utaalam wa kihasibu kwa sababu *Internal Auditor* ni sehemu ya menejimenti ya taasisi husika.

Mheshimiwa Spika, hapo lazima tuangalie jinsi gani ya kutenganisha *Internal Auditor Unit* lakini na kule anakoenda kuripoti, tusije tukatengeneza ugomvi mkubwa zaidi, halafu mambo yakazidi kuwa mabaya, kwa sababu *Internal Audit* kazi yake kubwa ni kushauri hiyo taasisi ambayo ipo ili kuhakikisha kwamba *internal control* ya taasisi inakaa vizuri na hakuna matatizo yoyote ambayo yanaweza kutokea kama mambo ya wizi na kadhalika. Kwa hiyo tuweze kuangalia vizuri hapo, ni jambo jema kuanza kutenganisha hapo.

Mheshimiwa Spika, mwisho niongelee watumishi ambao Mheshimiwa Waziri amesema kama wakiondolewa kwenye madaraka yao, kama alikuwa ni Mkuu wa Taasisi, tuchukulie labda ni Mkurugenzi, akiondolewa kwenye nafasi yake anatakiwa aende akatumikie mshahara wake ule wa awali, kama alikuwa ni Mtendaji wa Kata akachukue mshahara wake wa Mtendaji Kata. Naona hili kwangu sikubaliani nalo.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali waangalie upya katika hili kwa sababu tutakuwa tunawaonea watu wengi sana, kwa sababu watu wengi ukiangalia kutokana na historia wanaondolewa katika sehemu zao za kazi bila kuzingatia utaratibu. Anaweza akaja Mkuu wa Mkoa, akaja Mkuu wa Wilaya akamsimamisha mtu kazi kwa muda miaka sita, miaka saba, lakini hapati haki zake, anakuja mtu mwingine anachukua nafasi yake anachukua ule mshahara, halafu unasema kwamba tunamrudisha kwenye mshahara wake wa kipindi cha nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tuzingatie sheria iliyopo, kama tunataka kuanzisha sheria nyingine ambayo itawafanya watu wapunguziwe mishahara yao, basi tuanze sasa hivi lakini ajira basi ziwe za mikataba kama ajira zingine, lakini si ajira zile ambazo mtu anapewa barua ya ajira inakuwa ni *permanent and pensionable* lakini wanamwambia kwamba arudi kwenye mshahara wa

zamani, nafikiri tutakuwa tumewaonea na itakuwa sheria kandamizi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye bajeti ya Serikali. Nimepitia taarifa ya hali ya uchumi iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri na kwa kweli nataka niipongeze Serikali kwa dhati, imepigana kwa nguvu zote kuhakikisha uchumi wetu upo katika hali nzuri. Fedha yetu imeimarika, lakini vilevile tumepambana na mfumuko wa bei kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye suala zima la mfumuko wa bei na kuongezeka kwa pato la Taifa, Mheshimiwa Waziri ameongelea habari ya miradi yetu mikubwa tunayoendelea nayo. Kokote duniani *construction industry* inaleta matokeo makubwa zaidi katika kukua kwa pato la Taifa na hata ukipima *GDP* unaangalia na miradi ambayo inatekelezwa. Katika mchango wangu nataka nijikite kwenye namna gani viwanda vyetu vya ndani hasa viwanda vya simenti na niseme tu duniani kote Taifa ambalo linatumia simenti nyingi ni mataifa ambayo yana uchumi mkubwa. Katika Afrika Misri ndiyo inaongoza kwa matumizi makubwa ya simenti na hiyo vilevile hata *GDP* yao inaongezeka, lakini vilevile ni kipimo kwamba nchi hiyo ina uchumi mzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo na sisi katika suala zima la simenti hapa nchini, ni jambo la muhimu na lazima twende nalo hivyo hivyo. Shida iliyopo kwa sasa simenti yetu na bei yake imekuwa inaongezeka kila wakati badala ya kushuka.

Kikubwa zaidi kinachotokea ni kwamba, lipo tatizo la malighafi inayoenda kutengeneza simenti na bahati mbaya viwanda vingi ambavyo vinatengeneza simenti vinanunua *materials* yale ya kutengeneza simenti kwa wafanyabiashara wadogo. Hakuna kampuni kubwa mahsusi ambayo inalisha viwanda hivi, lakini kibaya zaidi ipo Tume ya Madini ambayo inatoa bei elekezi za malighafi hizi ambazo zinalisha viwanda hivi.

Mheshimiwa Spika, mwezi Aprili mpaka mwezi Juni, Tume ya Madini imetoa bei elekezi za *materials* hizi ambazo zinatumika kutengeneza simenti. Kwa mfano, *gypsum* inauzwa kuanzia Sh.38,000 mpaka Sh.100,000. Sasa uchuke *gypsum* kutoka Itigi uipeleke Tanga kwa ajili ya simenti, uipeleke Mtwara au uipeleke Dar es Salaam lakini bei ya tani moja kuisafirisha ni Sh.123, bei iliyopo sasa hivi katika *transport*. Kwa hiyo unakuta hakuna mtu ambaye anataka kuwekeza katika biashara hii.

Mheshimiwa Spika, naomba ku-*declare interest* nafanya kazi ya ku-*supply feldspar* katika kiwanda mojawapo kinachotengeneza *tiles*. Bei hiyo ambayo tunapangiwa na Tume ya Madini inatuumiza kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo huwezi ukaingiza mtaji wako mkubwa uwe na magari ya kusafirisha, kazi iliyofanyika wafanyabiashara weni wanadaka gari kwenye barabara hizi Msamvu pale, wanadaka gari maeneo mbalimbali, hakuna kampuni mahsusi. Kwa hiyo Waziri katika hotuba yake ukienda katika ukurasa wa 10 amegusia habari ya kuondoa mrabaha katika makaa ya mawe na anasema ni Sura 123 ya Sheria ya Madini, kwamba kupunguza kiwango cha mrabaha kutoka kwenye makaa mawe yanayotumika kama malighafi ya kuzalisha nishati viwandani kutoka 3% hadi 1%. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uzalishaji viwandani, kuchochea uwekezaji zaidi na kukuza ajira.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni jema, lakini naomba Serikali iondoe malighafi kwenye viwanda ambavyo vinazalisha simenti na kama hili nililosema kwenye *tiles* na watoe kodi tunayolipa ya *VAT* kwa sababu *VAT* tena inakuja kulipwa kwenye kiwanda baada ya kuuza zile bidhaa, lakini kufanya hivyo unachochea *supply* ya *materials* kwenye viwanda kuwa kubwa. Kufanya hivyo italeta ahueni kwa wafanyabiashara wanao-*supply* kule kwenye viwanda lakini vilevile na kupunguza bei ya simenti.

Mheshimiwa Spika, ukienda katika Sheria ya Madini, Sura 123, kwenye *regulations* za mwaka 2019 wameongelea habari ya kuondoa kodi kwenye baadhi ya madini, lakini kwa makusudi kabisa sheria inasema sheria hii haihusishi, *that trading of building all industrial energy minerals shall not apply to these regulations*. Kwa hiyo naiomba sana Serikali na Mheshimiwa Waziri aangalie jinsi ya kuondoa kodi kwenye malighafi hizi na kufanya hivyo kutachochea kwa kiasi kikubwa kwamba viwanda vyetu hasahasa vya ujenzi viweze kupata malighafi na hivyo kuweza kushusha bei ya simenti hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala lingine kuhusu Shirika la Bima la Taifa. Kama unavyojua biashara ya bima imekua hapa nchini, lakini na sisi tuna Shirika la Bima la Taifa. Bahati mbaya shirika hili bado linaendeshwa katika muktadha wa Kiserikali, nataka niishauri Serikali iajiri watu ambao wanaenda kufanya biashara ya bima, lakini vilevile walipe fedha shirika hili. Tunavyojua kwamba Serikali haiyawekei bima magari yake, lakini zipo taasisi ambazo zinafanya biashara nazo zipo *exempted* kwenye bima. Ninachotaka kusema ni kuwa, si kwamba hili Shirika la Bima la Taifa wapendelewe na Serikali, hapana lakini wawezeshwe ili waweze kufanya biashara kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la kubadilisha matumizi ya *Ranch* ya Kongwa sasa ianze kulima alizeti na

unaweza kukuta si tu alizeti na watataka walime na mahindi na vitu vingine. Mimi napinga jambo hili kwa kiasi kikubwa. Nimesoma kwenye hotuba ya Waziri katika sehemu ya masuala ya mifugo kwenye *importation* ya *product* kutoka nje na Waziri alisema kwamba nyama yetu bado haina ubora, lakini kinachotuzuia ni kwamba hatujaamua kama Serikali kuwekeza katika suala zima la kutoa nyama zenye ubora.

Mheshimiwa Spika, *Ranch* ile ya Kongwa ina *capacity* kwa sasa ya kuwa na ng'ombe 11,400, lakini na hiyo tumetoa nusu tumewapa baadhi ya wananchi wanachunga mle, vijiji vinavyozunguka, lakini ukija katika *capacity* yake nzima ina uwezo wakuwa na ng'ombe 40,000 kwa wakati mmoja. Nataka niseme Serikali iliangalie jambo hili, yapo mapori mengi wasikimbilie kupeleka alizeti sehemu ambayo haihusiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie kwenye Wizara hii muhimu ya Fedha na Mipango. Nianze kwa kusema, wakati naanza kuwa Mbunge tuliambiwa maneno yafuatayo: Ukiwa kama Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, la kwanza ni maslahi ya Taifa lako, la pili ni maslahi ya wananchi wako Jimboni kwako, la tatu ni maslahi ya chama chako, na la mwisho ni maslahi yako binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ameinuka leo Mbunge mmoja, tena Mbunge Mwandamizi ndani ya Bunge hili Tukufu akamnukuu Baba yetu wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage

Nyerere, nami nimeona tu nimnukuu Hayati Kambarage Nyerere kwenye Azimio la Arusha la mwaka 1967. Alisema kwamba, "ili kuhakikisha kuwa uchumi wa wananchi unakwenda sawa, Serikali lazima iwe na mamlaka kamili juu ya njia muhimu za kukuza uchumi.@ Akaenda mbali akasema, "Mheshimiwa Mbunge anaposimama, (ukurasa wa 11) kuomba barabara, au shule, au hospitali, au vyote; je, Serikali ina mpango gani?" Majibu, anategemea Serikali iseme, anasema, "naye pia jibu ambalo anagependa kupewa ni kuwa, Serikali inao mpango safi kabisa wa kutengeneza barabara au kujenga shule au hospitali au vyote kwa wananchi wa sehemu Mbunge Mheshimiwa huyo na watafanya hivyo kwa kutumia fedha." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunajadili bajeti ya Wizara ya Fedha. Sisi Wabunge moja kati ya jukumu letu kubwa ni kuisaidia Serikali kupata vyanzo vya fedha. Tutafanya hivyo kwa namna yoyote ile ikiwa ni pamoja na kuwaruhusu wananchi wetu kuachia maeneo muhimu ambapo maeneo hayo yataipatia Serikali fedha. Sheria ya Ardhi ya nchi hii Kifungu cha 4 kinasema, ardhi ni mali ya umma na Rais ndio mwenye dhamana; na inaruhusu Rais huyo huyo kuweza kutwaa ardhi ile kwa ajili ya maslahi ya umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunalo eneo letu *very potential* na nilisema humu ndani, suala la Ngorongoro atapigwa mwingine, atalia mwingine. Ngorongoro kwa mwaka 2018/2019 imeipatia Serikali yetu mapato ya Shilingi bilioni 150. Ngorongoro ndiyo urithi wa dunia. Leo wananchi wa Ngorongoro wanahamishwa kwa namna ambayo Wabunge wengi humu ndani tunaona wivu, wanahamishwa. Anasimama Mbunge anasema, wanateswa, wanaonewa.

Mheshimiwa Spika, ipo haja ya kupima uzalendo wa Watanzania ambao tunawawakilisha sisi humu ndani, tupimwe uzalendo wetu kwenye Taifa letu. Haiwezekani tuungane na raia wa kigeni kulichafua Taifa letu kwa

*propaganda* zinazofanya tushindwe kukuza uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania tunajuana. Viingereza vyetu vya Rasi Simba, tunajuana. Leo anasimama mwanaharakati eti Mmasai wa Ngorongoro, wa Loliondo, eti mwanaharakati anaongea Kiingereza cha Malkia. Kiingereza cha ndani kabisa yaani, anasema anawatetea Wamasai wenzie wa Ngorongoro. Tanzania ni yetu, tutaachia rasilimali. Kama kwa kufanya hivyo inasaidia kujenga nchi, inasaidia kukuza uchumi, inasaidia kuongeza biashara, inasaidia kuboresha maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 1999 wananchi wa Kata ya Bulyanhulu, Kakola kule, uliko Mgodi leo wa Barrick ambao sasa hivi unaitwa Twiga, walihamishwa kwenye maeneo yao, wakakiri kuhama kwenye maeneo yao. Leo wananchi mwaka 2008, 2010, wananchi wa Mgodi wa Buzwagi ambao leo ndiyo upo mgodi ule walikubali kuhama kwenye maeneo yao. Wengine mpaka leo wanadai fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hali ndiyo hiyo, mimi wananchi wa Shinyanga wamenituma, wanamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kauli yake aliyoitoa ya kusema anawapa pesa wananchi wa Ngorongoro kwa kuhama, anawajengea nyumba na kuwakabidhi hati, eti mpaka mtu mwenye wake wa tatu atapewa hati tatu, wananchi wa Shinyanga Mwendakulima na wenyewe wanataka hiyo *privilege* waliyopewa watu wa Ngorongoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni yetu sote. Haya mambo ya kubembelezana; Mgodi wa *North Mara* watu waliondolewa pale kwa mabomu. Haiwezekani leo jamii moja ya Watanzania iwe *very much privileged,* ionekane yenyewe ndiyo kila kitu, *propaganda* ziendelee kufanyika eti tunawabembeleza watu kupisha eneo ambalo ni *potential,* ni urithi wa dunia, eneo ambalo ni rasilimali kubwa duniani, siyo

Tanzania. Tunawagopa kwa sababu ya *propaganda*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi wakati najifunza siasa, niliambiwa *propaganda* hujibiwa kwa *propaganda*. Hawa wanasema leo eti Mawakili, wanakwenda Mahakama ya *ICC* kwenda kuishtaki Tanzania kwa kuwapiga watu wanaoenda Ngorongoro, tutapambana nao Mahakamani. Wale watu wa *propaganda* wapambane nao kwa *propaganda.* Haiwezeki tukae kimya ardhi yetu inatumika vibaya, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wa Shinyanga na sisi tunataka haki yetu. Wananchi wa Shinyanga, ilifika hatua, Kahama peke yake imekuwa ya nne Kitaifa kwa kuchangia pato la Taifa kwa sababu wananchi wa Shinyanga walikubali kutoka kwenye maeneo ya madini na kuwaachia wawekezaji ambao leo hii tunapiga kelele hapa, lakini ndiyo pesa za watu wa Shinyanga waliyotoa kwenye maeneo yao wameachia nchi inapata kipato. Nasi tunaidai haki hiyo kwa wivu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, wanatoa sababu eti maeneo yale wameyazoea. Wale maeneo wameyazoea walikuwa wanakaa tu na kuchunga ng'ombe. Shinyanga wananchi wa Mwime, Mwendakulima, Chapua, hawana shughuli nyingine yoyote ya kuwaingizia kipato zaidi ya kuchimba dhahabu. Hawana shughuli nyingine. Ukienda Ibadakuli, Bulyanhulu, wananchi wa Bulyanhulu kule Nyangalata, Namba Tatu, Namba Nne, hawana shughuli yoyote ya kuwaingizia kipato. Asilimia 99 ya wananchi wale shughuli yao ilikuwa ni uchimbaji. Kama suala ni maeneo waliyazoea, na sisi tuliyazoea. Hoja hizi ni batili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaposimama ndani ya Bunge hili sisi kama Wabunge, kazi yetu ni kutafuta vyanzo vya mapato. Tumesikia hapa Wabunge wanasema, wale watu walikuwa

wananufaika, tumeinua Taifa hili kwa sababu wanawake walikuwa wanapewa asilimia nne, vijana wanapewa asilimia nne, watu wanaoishi na ulemavu wanapewa asilimia mbili. Leo inapunguzwa mpaka asilimia mbili, mbili, moja, pesa nyingine wanapelekewa Wamachinga. Kakeki kenyewe ni kadogo, tunakagombania, watu wengine wanatetea maslahi binafsi kwenye maslahi ya umma, hiyo haikubaliki. *(Makofi)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salome Makamba, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Tabasam.

**T A A R I F A**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, Sengerema wananchi wanaachia eneo la *Sotta Mining*, kaya 1,600 mpaka sasa hivi tunavyozungumza wanatakiwa kuondoka, wapishe mgodi bilioni 740. Wao siyo watu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Salome Makamba, unapokea taarifa hiyo.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, taarifa ya mjomba wangu Mheshimiwa Tabasam Hamis naipokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mustakabali huo, na bahati nzuri wewe ni Mwalimu wetu mzuri sana. Kanuni za Bunge zinakataza kujadili jambo ambalo limeshajadiliwa na mjadala wake ulishafungwa. Mjadala wa Ngorongoro tulizungumza humu ndani, tukajadili na huo mjadala umeshafungwa. Naomba kwa Mwongozo wako suala hili lisisemwe tena, kwa sababu watu wameshakubali kuhama, watu wameshakubali kwenda kwenye maeneo yao mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasisitiza, zile ng'ombe za wale wawekezaji ambazo wameziweka kwenye Hifadhi, wale watu watoe. Nimeangalia kwenye taarifa ya Habari, zile ng'ombe mlizoziweka kwenye malori ni chache mno. Wekeni zile ng'ombe zote zilizoko kwenye Hifadhi ziende na wale watu kule Handeni. Ndiyo utajua, tangu lini Mtanzania wa kuzungumza Kiingereza cha Malkia, eti amekuwa Mmasai wa Ngorongoro, eti amekuwa Mmasai anatetea wananchi wa Ngorongoro! Hiyo haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya *issue* ya Ngorongoro natumai umeifunga, nami naishia hapo, sitaisema tena. *(Kicheko/Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Muda umeshaisha Mheshimiwa. *(Makofi)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa shughuli zetu za siku ya leo. Nawapongeza na kuwashukuru Wabunge wote walioshiriki mjadala huu wa Bajeti Kuu ya Serikali. Japo nimesikia kuna Wabunge wanasema Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango, hii ni Bajeti Kuu ya Serikali. Ile ya Wizara ya Fedha na Mipango ilishapita. Kwa hiyo, hii ni Bajeti Kuu ya Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.48 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 21 Juni, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*